ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.

10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

46.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
49.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
64.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
65.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

66.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
67.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
68. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
69.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
70.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
71.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
72.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
73.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
74.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
75.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
78.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Pili – Tarehe 21 Januari, 2010

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA BARAZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani hotuba kuhusu mswada wa sheria kuweka masharti ya uanzishaji na uendeshaji ya Ofisi ya Mkaguzi wa Mashtaka na mambo yanayohusiana na hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu mswada wa sheria ya Kuweka Masharti ya Uanzishwaji wa Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mambo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha mezani maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uanzishaji na Uendeshaji Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mambo yanayohusiana na hayo, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 96

Daftari la Wapiga Kura

(Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 87

Marekebisho ya Katiba na Baadhi ya Sheria za Zamani

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza**:-**

Mhe. Waziri Katiba yetu ya Zanzibar ilifanyiwa marekebisho mara ya mwisho mwaka 2002.

(a) Je, Mhe. Waziri, huoni haja ya kufanyika marekebisho mapya ya Katiba ili kuondoa kasoro zinazojitokeza katika sehemu mbali mbali za Katiba hiyo.

(b) Kwa kuwa zipo sheria ambazo ziko nyuma ya wakati kutokana na mabadiliko mbali mbali ya ndani na nje ya nchi yetu, kwanini Tume ya Kurekebisha Sheria inashindwa kufanya kazi zake ipasavyo katika kupitia sheria hizo ili zifanyiwe Marekebisho.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora – Alijibu**:-**
Mhe. Spika, ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.87 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba Katiba ya Zanzibar, 1984 ilifanyiwa marekebisho kwa mara ya mwisho mwaka 2002.

Hata hivyo, tukumbuke kwamba Katiba ndio sheria mama ya Nchi; na marekebisho yake yanahitaji kufanywa kwa muangalifu mkubwa ili kutoathiri mfumo wa mwenendo wa Nchi. Pamoja na hayo, serikali imekuwa ikichukua hatua ya kufanya marekebisho kila panapohitajika. Aidha, hivi sasa serikali ipo katika mchakato wa kuangalia maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa marekebisho kulingana na mahitaji yalivyo. Lakini Mhe. Spika, marekebisho haya hayatahusu hili suala linalozungumzwa mitaani.

(b) Inafahamika kwamba Tume ya Kurekebisha Sheria ni chombo kinachopitia Sheria mbali mbali za nchi na kupendekeza serikalini kufanya marekebisho muafaka kwa baadhi ya Sheria zinazohitaji marekebisho hayo.

Hata hivyo, kutokuanza kazi kwa Tume hiyo sio kushindwa kwa serikali kufanya marekebisho kwa sheria zinazohitaji kufanyiwa marekebisho. Serikali kupitia Taasisi zake ambazo zinazo simamia sheria hizo, imekuwa ikiwasilisha marekebisho ya Sheria mbali mbali kulingana na mahitaji yanapojitokeza.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri wa wizara hii kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna masuala zaidi ya 21 katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano na ukiyatizama ni mengi masuala haya yanalenga katika masuala ya

kuimarisha uchumi. Lakini katika Katiba ya Zanzibar kwa tokea Muungano hadi miaka 10 ya Muungano kwa kweli kwa Zanzibar sasa hivi tumeshajimudu vizuri na tumeshajidhatiti vizuri ili kuimarisha uchumi na kuendeleza maelendeleo mbali mbali ya nchi hii.

Mhe. Spika, haoni kuna haja katika masuala yale 21 ya ndani ya Katiba ya Muungano ambayo ni mengi yao ni ya kufufua uchumi yakiwemo kama masuala ya kuchimba gesi asilia pamoja na mafuta na masuala ya biashara za nje na masuala ya masomo ya nje ambayo ni masuala ya kiuchumi ikifanyiwa marekebisho ili wakaachiwa katika Katiba ya Zanzibar ili na wao wakajiimarisha kiuchumi kwa ajili ya wananchi wake. Je, Mhe. Waziri haoni kuna haja ya kufanya hivyo ili na sisi katika Katiba ya Zanzibar ikiwa na mbawa za kurusha maendeleo yake ya kiuchumi kwa wananchi wake.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kumkumbusha tu kwamba kwa sababu masuala haya yamekuwa yakitajwa katika vikao vingi kabisa. Hivi sasa kuna kikao cha pamoja kinachoshughulikia masuala ya kero za Muungano na kama alikuwepo Pemba juzi au alisikiliza kwenye vyombo vya Habari alipomsikia Mhe. Rais wa Zanzibar aliposema kwamba suala la Mafuta na Gesi hivi sasa liko katika utaratibu wa kutaka kuondolewa katika Katiba na mchango huu ulijitokeza ndani ya Baraza hili.

Kwa hivyo, tunaendelea moja baada ya moja kila tutakaloliona linafaa katika kujenga uchumi, tunaona sasa tumeshakuwa tunajimudu basi tutafanya wenyewe, ahsante.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametujibu kuwa Tume ya Kurekebisha Sheria imeshafanya sheria nyingi ambazo zimeshaletwa katika Baraza hili.

(a) Mhe. Spika, minavyofahamu mimi Mwenyekiti wa Tume hii ya Sheria bado hajateuliwa. Je, sheria hizi zimefanywa na Tume au na wanasheria wetu tu wa serikali.

(b) Mpaka hivi sasa hatujui Ofisi maalum ya Tume ya kurekebisha sheria hatujui wapi ilipo, sijui Mhe. Waziri anaweza kutueleza wapi ipo ambapo wanafanyakazi hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:

(a) Mhe. Spika, marekebisho ya sheria mbali mbali yanafanywa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wanaofanya miongoni mwao ni hao Wafanyakazi wa Tume ya Kuchunguza sheria , hiyo kazi wanaendelea nao kufanya.

(b) Mhe. Spika, suala la Ofisi nakumbuka kwamba katika Baraza hili hili liliulizwa swali la kwamba jitihada ifanyike ili watu wa Tume ya Kutunga Sheria wajengewe Ofisi na ikafanywa lakini kwa bahati Baraza hili likatoa ushauri kwamba ile haifai na tukalazimika sisi tutoe mpango wa kuhama katika Ofisi ambayo tunatumia sisi tuingie kule ambako tuliwajengea wao na wao wabakie katika jengo letu kubwa na aliwahi kutoa ushauri Mhe. Haji Mkema kwamba labda tungeomba lile jengo dogo la Wizara ya Afya pale pembeni lilioko karibu na Makumbusho kuihamishia ofisi hii, masuala hayo tunayafanyia kazi Mhe. Spika.

Nam. 36

Tatizo la Kukatika Umeme Zanzibar

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza**:-**

Zanzibar inategemea huduma ya umeme wa *TANESCO* kutoka gridi ya Taifa Tanzania Bara. Umeme huo katika miaka ya karibuni umekuwa na matatizo ya kukatika kutokana na uchakavu wa miundombinu ya kuvushia umeme huo baharini, pamoja na tatizo la uzalishaji wa umeme huo kutoka kwenye vianzio vya *TANESCO*.

(a) Je, Mhe. Waziri serikali yetu ina mipango gani ya kupata umeme mbadala utakaosaidia kupunguza tatizo la umeme litakapotokea tatizo la kukatika umeme kutoka Tanzania Bara.

(b) Kwa kuwa kuna Makampuni mengi ya kuzalisha umeme kibiashara kwa njia mbali mbali duniani. Je, Mhe. Waziri, kuna Kampuni ngapi ambazo serikali imewasiliana nazo kwa lengo la kuwekeza hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nam. 36 lenye kifungu (a) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Wizara kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Shirika la Umeme wanaendelea na juhudi za kutafuta umeme mbadala kwa kuzingatia gharama za uzalishaji, uhakika wa kuwepo umeme huo kwa matumizi ya kila siku na wenye kutunza mazingira.

Vyanzo muhimu ambavyo vinafanyiwa utafiti ni:-

1. Kuzalisha umeme kwa kutumia upepo ambapo Shirika la Umeme limewasiliana na Makampuni mbali mbali kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina ili kuhakikisha kama Zanzibar inao upepo wa kutosha kwa ajili hiyo.

2. Kuzalisha umeme kwa kutumia mawimbi ya bahari *Wave Power Generator*. Wataalamu kutoka Shirika la Umeme tayari wametembelea Nchini Israel kwa lengo la kufanya mazungumzo na Kampuni ya *SDE* ya huko Israel. Mhe. Spika, watalaamu wetu wa Shirikika la umeme walipokwenda Israel mimi ndio niliongoza msafara huo.Kwa hiyo, nataka niwahakikishie kwamba juhudi hizo zinaendelea.

(b) Serikali imewasiliana na Makampuni yafutayo ambayo yanazalisha umeme kwa njia mbali mbali:-

i) AGGRECO ya Dubai – umeme wa Diesel Generator na Turbine.

ii) CATAPILA MANTRACK – Umeme wa Diesel Generator

iii) CATAPILA USA RING POWER – Umeme wa Diesel Generator.

iv) CUMMINS YA DUBAI – Umeme wa Diesel Generator.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, katika suala langu mama niliuliza kwamba kwa kuwa harakati hizi za umeme kutoka Tanzania Bara kukatika

mara kwa mara au kukosekana kabisa kama tulivyo sasa hivi giza katika nchi yetu na hii ni historia ambayo itakuwemo katika kumbukumbu zetu.

(a) Lakini tuseme kwamba katika hayo makampuni ni makampuni mangapi yameonesha imani au nia ya kuekeza hapa Zanzibar.

(b) Hivi sasa kuna taarifa rasmi kwenye vyombo vya habari vilivyotolewa leo kwamba Tanzania huenda ikakumbwa na kukosa umeme mkubwa sana na kukawa na mgao mkubwa kuliko tulivyotarajia kwa kukosa megawati zaidi ya 200. Je, kwa dharura hiyo na mara baada tunategemea umeme urudi ili wananchi uwasaidia tumejiandaa vipi kwa hili kwa dharura.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:

(a) Mhe. Spika, karibu makampuni yote haya yameonesha nia ya kikweli kweli kwa mfano moja ya kampuni hii ya *Solar Power* wao wakati tunaongea tuliwambia kwamba sisi hatuna fedha za kufanyia *study* hiyo na wao walikubali kuja kufanya *study* hiyo kwa gharama zao mara baada ya kufanya *study* hiyo watakaa na Shirika la Umeme na kuona nini kifanyike baadae.

(b) Mhe. Spika, kwa bahati mbaya mimi sikuwa na taarifa hiyo iliyotolewa leo na vyombo vya Habari vya Tanzania Bara kuhusiana na tatizo la umeme ambalo litaikumba Tanzania. Lakini kama hivyo ndivyo iliyo basi hiyo itatufanya tuengeze kazi ya kuhakikisha Zanzibar tunakuwa na vianzio vyetu wenyewe vya umeme.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Mhe. Spika, na mimi naomba kumuuliza suala dogo tu Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Spika, kwa kuwa Zanzibar kuna watu watiifu sana na wanaheshimu viongozi wao wameanza kujitafutia wenyewe umeme mbadala kwa kununua *Generator*. Lakini kwa bahati mbaya majenereta hayo yanakwenda kwa mafuta ikiwa ni petrol ikiwa dizeli na sasa hivi mafuta yenyewe yana tabu. Lakini isitoshe kwamba mafuta yana tabu, mafuta hayo yakitolewa kwenye vituo vya mafuta yanatolewa kidogo halafu wanapewa vijana wanauza kwa bei ya juu.

Je. serikali hamuoni kwamba kuna haja ya kuwasaidia wananchi hawa na kuchukuwa hatua kali kwa wale wambao wanauza mafuta kwa bei ya kuruka. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, napenda nimjibu Mhe. Aziza Nabahan Suleiman dada yangu huyu. Ni kweli

Mhe. Spika, wananchi wa Unguja kwa hakika ni waugwana na ni wastaarabu na ni wavumilivu na kwa kweli sisi kama viongozi wa vizara na serikali tunawapongeza sana kuwa na ustahamilivu huo. Wote tuna imani kabisa tatizo kama hili lingetokea katika nchi yoyote basi pangekuwa hapakaliki.

Ni kweli baada ya tatizo hili wananchi wetu wengi wale wenye uwezo wamenunua majenereta kwa kiwango chao, wale wenye uwezo mdogo kama Mhe. Aziza na mimi basi tumetafuta vijenereta vile vidogo leo kizima kesho kibovu lakini kinakwenda na wengine na wengine ili viweze kuwasaidia, tunawapongeza. Na ni kweli majenereta haya yanakwendea mafuta na mengi yanatumia *petrol* ni kweli katika wiki hii kumetokea tatizo la upungufu wa mafuta ya *petrol.*

Mhe. Spika, nataka nikiri hilo na wizara yangu tunaendelea kuwasiliana na wenzetu hawa waletaji wa mafuta kuona tatizo hili linaondoka na tatizo hili limejitokeza mara baada ya Kampuni ya *GAPCO* ambayo ilikuwa ni moja ya waletaji mafuta wakitumia meli ile ya MV. Ukombozi. Meli kuharibika kwa hiyo kumekuwa na tatizo kidogo kwa kampuni ile kupata meli nyengine ya haraka haraka kuweza kuleta mafuta. Kwa kweli hili nalo limechangia lakini tutajitahidi kuona tatizo hili linaondoka.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa maelezo ya ziada baada majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi Nishati na Ardhi.

Mhe. Spika, jana nilifanya juhudi za makusudi kuwatembelea hawa waagiziaji mafuta wote watatu. Tulianza kwa *GAPCO* tukenda Zanzibar *Petroleum* na tukamalizia na *United GAPCO* na *ZB* hawa ni waagiziaji wakubwa wa mafuta watatu.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwa kweli wote kimsingi wamekiri kwamba wameshindwa na *volume* kubwa ya mafuta hivi sasa na wao wametuhakikishia kwamba yanakuwa kidogo siku 3 au 4 yamekwisha. Na nikawaambia kwamba hiyo sasa sio faida kwenu kwamba kuna soko kubwa na nyie muongeze *speed* ya kupata mafuta. Wakakiri kweli huo ni ukweli lakini sasa wanasema kuyapata hivi sasa siku mbili, tatu hapa kidogo kuna matatizo huko wanakoagiza. Lakini nitatoa mfano mmoja mmoja *United Petroleum* ana dezeli ya kutosha na hii Petroli tunayokwenda nayo sasa hivi yake na mpaka jana alikuwa na lita kama mia moja na hamsini elfu, Jana katoa hamsini zilibaki laki moja, wiki hii hizo laki moja ndio anawagaia na hao wengine wanakwenda nazo kidogo kidogo ndio tunaona matatizo hayo, na haya wamenambia

wenyewe nimekwenda kituoni sio kuhadithiwa maana namuona Mheshimiwa mmoja anatikisha kichwa sio uongo huo nimekwenda mwenyewe.

Pili, Mhe. Spika, huyo wa *GAPCO* ni kweli kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba ni kweli Meli ya Ukombozi ambayo anaitumia ni mbovu lakini nikawaambia hiyo sio sababu kama wewe mtu wa biashara meli ni mbovu kodi nyengine. Sasa huo tumeuona ni udhaifu wake wa tatu, huyu *Zanzibar Petroleum* ndie tunae tamaa nae sasa hivi, meli yake ndogo ya mafuta iko Mombasa hapa ambako anapaswa apate mafuta. Kuna tangi kutoka nje ina charge lakini bado kuna mvutano na wao wenyewe wakenya wanataka nafasi hiyo.

Lakini Mhe. Spika, tunawabana hawa wawekezaji kwamba kuna sheria yetu kila wakati wawe na mafuta yasiopungua asilimia 40 kwenye matangi yao. Kwa nini hasa yanapungua hapo tunawabana sasa na tuna sheria zetu na tunaweza kuwapiga hata faini.

Hilo nataka kuwahakikishia Waheshimiwa kuwa serikali inalijua na inalifuatilia kwa makini zaidi kuona kwamba tatizo hili linaondoka hata wao jana wakatushauri kwamba hebu tueke kizingiti au taratibu wauziwe watu labda 20 tu kwa sababu wengine kama nilivyosema yakitoka pake wananunua na wanauza magendo. Sasa hilo kidogo ni gumu tutachukuwa mbinu kwa askari kushirikiana nao na kuona kwamba hawanunui pale na kuuza pembeni. Hilo ni gumu lakini serikali itajitahidi na kulisimamia ipasavyo. Ahsante.

Mhe. Spika: suala limechukuwa muda kidogo twendeni kwenye suala linalofuata.

Nam. 48

Utandazaji wa Waya za Umeme chini ya Bahari

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Mnamo siku ya Ijumaa tarehe 04/12/2009, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Amani A. Karume alizindua kazi ya ulazwaji wa waya wa umeme baharini *Sub Marine Cable* kutoka Tanga hadi Pemba kwa ajili ya kukipatia umeme Kisiwa cha Pemba.

(a) Waya huu uliolazwa baharini una urefu gani na kila kilomita moja ina uzito wa kilogram/tani ngapi.

(b) Waya huu unatarajiwa kuishi baharini (*life span*)kwa muda gani.

(c) Waya huo umetengenezwa kwa maadini gani na je madini hayo yana uwezo wa kutosha kuuzamisha na kuufikisha chini ya bahari ili usielee na kusababisha madhara.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swala lake nam. 48 lenye kifungu a, b na c kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, waya uliolazwa baharini baina ya Tanga Tanzania Bara hadi Mkumbuu katika ksiwa cha Pemba una urefu wa kilomita 71.439, na una uzito wa kilogram 42 kwa kila mita moja sawa na tani 42 kwa kilomita moja.

(b) Waya huu kwa mujibu wa watalaamu unatarajiwa kuishi kwa muda wa miaka 40 ikiwa utatumika katika viwango na uwezo uliowekwa.

(c) Waya huo umetengenezwa kwa madini ya shaba na umehifadhiwa kwa kuzongwa waya nyembamba zilizotengenezwa kwa chuma cha pua. Kutokana na uzito wa waya huu, hivyo waya huu hauelei na umelazwa chini ya bahari na umefukiwa kwa chombo maalum.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Rais kwa kuamua kuambatana na viongozi wa Baraza la Wawakilishi akiwemo Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwenda kupokea waya ule Tanga. Lakini hapo kabla Shirila la Umeme liliiahidi Kamati ya *PAC* kwamba wangekuwa wa mwanzo kwenda kupokea waya huo.

(a) Je, ahadi hiyo kwa sababu haikuwa ni lini *PAC* itapata fursa ya kutoa baraka kwenye waya huo.

(b) Muda huu Shirika la Umeme limekuwa likikabiliwa na waya wa wizara wa umeme wahalifu wamekuwa wakilihujumu shirika hili kwa kuiba waya. Je, hakuna uwezekano wahalifu hawa kuamua kupiga mbizi kwenda kuchukuwa waya huo.

(c) Tumeambiwa kwamba waya huo uliolazwa kutoka Tanga ni wa kisasa na umetengenezwa kwa njia 3, njia moja ikiwemo ya Mawasiliano ya Simu, lini serikali itaamua waya huo kutumia kwa huduma ya simu.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:

(a) Mhe. Spika, ni kweli kama alivyosema miongoni mwetu kama alivyosema Mhe. Abubakar Khamis Bakary, wamepata fursa hiyo na bahati mbaya Kamati ya PAC hawajapata lakini nataka niwaambie sio PAC tu, Wawakilishi wote. Tulikuwa tunajaribu kuangalia uwezekano ili Wawakilishi wakati wa sherehe za kuzindua umeme huu pale Pemba basi waweze kupata fursa ya kwenda kushiriki, hili ikiwezekana wote tutaweza kupata fursa hio kwa sababu jambo hili ni la kihistoria na utekelezaji wake umetekelezwa chini ya uongozi wenu. Kwa hiyo, ni busara zaidi kwenda mkashuhudia kwa macho yenu.

(b) Ni kweli kumekuwa na wimbi kubwa la wizi wa waya za umeme huku, hili jambo linasikitisha kwa sababu nchi imo katika tatizo kama hili linatokea na wenzetu wawili watatu kwa sababu ya ujinga na upumbavu wanaharibu miundombinu hii kiasi kwamba hata huo umeme ukija kesho maeneo mengi waya hazimo.

Hivi sasa karibu wafanyakazi wengi wa umeme wamekuwa wakifanya zoezi hilo angalau kupita huku na kule usiku wakifanya doria. Lakini wito wangu natoa kwa wananchi wote tusaidiane kuhakikisha kwamba tunailinnda hii miundombinu. Lakini haitawezekana kabisa ule waya kule uliko hawa kwenda kuiba hicho sio kitu rahisi.

(c) Ni kweli waya huu ni wa kisasa zaidi unaweza ukatumika matumizi haya ya mawasilinao. Mhe. Spika, Zanzibar kama ilivyo nchi nyengine imekuwa ikipiga hatua kubwa kabisa katika masuala ya mawasiliano na mengineyo basi wakati tukifikia wakati huo basi tayari tumekuwa tumejiandaa na hatutosita kutumia waya huu kwa shughuli hiyo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba Zanzibar na Pemba bado tunatumia umeme wa kutegemea kutoka Bara. Tunasikia kwamba kuna mfadhili amekuja anataka kuwekeza umeme wa upepo wa kudumu hapa hapa nchini na tayari ameshafanya majaribio ya awali kwa gharama zake na hivi sasa anaishi nchini kwetu kwa gharama zake lakini kibali bado hajapewa. Je, hilo analijua ?

Swali (b) kuna Waisrael walikuja kufanya utafiti wa kuwekeza umeme wa kutumia mawimbi ya bahari, lakini ripoti yake imesema kwamba umeme huo una gharama kubwa wananchi wetu watashindwa kuununua. Je, hilo ni kweli ?

Swali (c) kwa kuwa hivi sasa hapa petu pana magari mengi sana pamoja na majenereta yanayotumia mafuta. Haoni kwamba sehemu zetu za kuwekea mafuta hivi sasa zimekuwa ndogo. Je, wizara ina taratibu za kuweza kuongeza pakuhifadhia mafuta ili pasiwe na kero ya upungufu wa mafuta hayo ?

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, mimi binafsi sina taarifa ya kwamba kuna mwekezaji huyo wa kuzalisha umeme kwa kutumia upepo na ameshafanya *study* kwa gharama zake na yupo hapa anaishi kwa gharama zake lakini kuna kikwazo. Kwa kweli mimi sina taarifa hiyo na ninaamini taarifa hiyo sio ya kweli.

Jibu (b) kampuni ya *SDE* ya Israel umeme wake haukuweza kutekelezwa si kwa sababu ungekuwa una gharama kubwa hata kidogo. Lakini nataka niseme wakati tunafanya mazungumzo na wenzetu wa Israel kwa ajili ya umeme huu wa mawimbi ya bahari na ilikuwa ufanyike kule Pemba jimboni kwa Mhe. Hija Hassan Hija, tatizo halikuwa kwamba umeme huu ungekuwa na gharama hata kidogo. Lakini uwezo wa umeme huu kwa kuanzia ilikuwa ni *megawatt* 10 wakati matumizi yetu kule Pemba ni *megawatt* 5. Wakati huo huo, tulikuwa tunafanya mazungumzo na yalikuwa yamefikia pahala pazuri na wenzetu wa Norway.

Kwa hiyo, Wanorway kwa kweli baada ya kupata taarifa hii walianza kusuasua na walionesha hofu ya kuacha kuendelea kusaidia mradi huu wa *cable*. Kwa hiyo, ilikuwa lazima tuwe waangalifu sana katika kuamua. Kwa kweli tulisita kwa wakati ule kuendelea na mazungumzo na *SDE* ya Israel na tukawa tunaendelea na wenzetu hawa wa Norway ambao wao *cable* yao ina uwezo kama nilivyosema wa *megawatt* 20 yaani karibu mara mbili zaidi kuliko ile ya *SDE* ambayo ilikuwa ni *megawatt* 10.

Jibu (c) nataka nikiri kwamba ni kweli sasa hivi tumekuwa na magari mengi kuna haja ya kuangalia tuwe na maeneo mengine ya kuhifadhi mafuta ambayo ni wazi kabisa yataondoa hili tatizo la kwamba leo *diesel* ipo kesho hakuna, leo mafuta ya taa yapo kesho hakuna.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nimeona niweke jambo moja sawa. Mhe. Spika, nalazimika kufanya hivyo kwa sababu ya taswira pengine isiyo sahihi ambayo hasa kipindi cha dhiki huwa inajengeka, hasa kwa huu wakati ambao tunaupitia hivi sasa.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Abdalla Ali, aliuliza swali kwamba yupo mwekezaji ndani ya nchi anakaa hapa kwa gharama zake, ameshafanya tafiti lakini kibali hajapewa. Upande mmoja ni sahihi, upande mmoja si sahihi.

Nakuja kwenye mambo yasiyo sahihi. Mtu huyo yupo lakini kaoa hapa kwa hiyo anakaa kwa sababu kaoa hapa, hakai kwa sababu anatutafutia sisi umeme si kweli.

Pili, hakuna utafiti wa aina yoyote uliofanywa kwenye nchi hii juu ya nguvu za upepo bado. Tafiti hizo zinahitaji kama mwaka mzima kufanywa miezi 12 kwenye maeneo zaidi ya moja yaliyokuwa ya mnyanyuko Unguja na Pemba, hakuna mtu aliyefanya tafiti hizo. Zipo tafiti za awali zilizofanywa tangu kipindi cha miaka ya 90 na kina *SIDA* hao lakini haijafanya utafiti wa kina.

Tatizo lililokuwepo kwa huyu bwana na wengine waliojitokeza ambao wanataka kuzalisha umeme kwa nguvu za upepo kila mmoja anataka serikali impe *exclusive right*, kwa maana impe uhalali pekee kuzalisha umeme ule kwa anavyotaka yeye na kwa bei ambayo anataka kutuuzia sisi. Sio hivyo tu, wanataka kuitumilia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sasa kuwapa kibali ili wakakope kwa niaba yetu, sisi tunajua kukopa. Kama waziri siwezi kumpa mtu mmoja kibali kuweka hatima ya nchi kuwa juu ya shida tulizokuwanazo tukaingia kwenye shimo kubwa zaidi. Sasa hapo unakuja huo ufisadi.

Ninachoagiza mimi Bodi ya Shirika la Umeme ifanye upembuzi wa maombi yote yaliyokuja ili hilo nilipeleke Baraza la Mapinduzi siwezi kuamua peke yangu.

Juu ya hayo na nitazungumza wakati ninawasilisha Sera ya Nishati, tumeshapata wafadhili ambao sasa kuna mwelekeo wa kuweza kutusaidia kufanya tafiti hizo bure. *SIDA* na Norway kuna mwelekeo kwamba watatusaidia kwa gharama zao kufanya tafiti ya nguvu za upepo Unguja na Pemba kwa mwaka mzima. *Document* hizo sasa zitatupa unafuu baada ya hapo, aidha kuwakaribisha wawekezaji binafsi au sisi wenyewe kwenda *World Bank* na kwengineko kuomba fedha hizo kuzalisha umeme wa upepo bila ya kujifunga na kuweka hatima yetu ya mahitaji ya nishati ya umeme mikononi mwa mtu mmoja.

Sasa hivi tunapaswa kuwa waangalifu kwa sababu ya mitihani mikubwa tuliyoipata, hatuwezi tukatoka kwenye shida moja tukaingia kwenye mashaka mengine ikawa tena tunazidi kujiangamiza. *(Makofi)*

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, kwa mujibu wa maneno ya Mhe. Naibu Waziri ni kwamba *cable* hii ina uhai wa miaka 40 kama itatumika vizuri. Kwa sababu ya jitihada ambayo wizara yake inafanya ya kuzalisha umeme mbadala, tamaa ya kibinadamu ipo kabla ya miaka hiyo 40 tunaweza kuwa na umeme wetu mwingi.

Je, *design* ya waya hii ya Tanga/Pemba inayofanywa na hii inayotegemewa ya Unguja nyengine. Inawezesha kupokea na kusafirisha kwa maana ya ile ziada tutakayopata baadaye kuuza au ni ile ya kupokea tu. Kama hiyo haijafanywa. Je, ana mpango wowote wa kufanya ili kuona kwamba baadaye hizi waya tulizonazo ziwezeshe pia kutusaidia kuuza umeme mbadala ambao tutaupata.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ni kweli ule waya ambao upo Tanga si tu kwamba una uwezo wa kuleta umeme pale. Lakini pindipo tutakuwa na umeme wa ziada basi una uwezo vile vile wa kwenda kuuza umeme kule. Hivyo hivyo tunategemea na huo mwengine ambao tumefanya maandalizi yake ya kutoka hapa Ras Kiromoni kuja Fumba utakuwa katika hali hiyo.

Nam. 6

Wanaojitolea kusaidia Wanafunzi wa Sekondari

Mhe. Amina Iddi Mabrouk – Aliuliza**:-**
Hivi sasa kuna vijana wengi mitaani waliomaliza masomo yao kufikia Kidato cha Sita *(Form VI)* ambao wanafanya kazi ya kujitolea kuwasaidia wanafunzi wa sekondari katika skuli mbali mbali, Unguja na Pemba. Vijana hawa bado Wizara haijafanya utaratibu wowote wa kuwaajiri, kuwalipa posho la kujikimu, au angalau kuwaorodhesha na kuwajua.

(a) Je, Mhe. Waziri, Wizara yako ina mpango gani wa kuwasaidia vijana hao.

(b) Kwa kuwa wengi wao walisoma kwa kujitegemea *(private)* Wizara itawasaidiaje wale wenye sifa za kujiendeleza.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijajibu swali lake naomba nitoe maelezo mafupi.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imewapa ajira ya muda baadhi ya vijana waliomaliza Kidato cha Sita na kufaulu masomo ya Sayansi na Hesabati kwa ajili ya kusaidia kupunguza uhaba wa walimu wa masomo hayo katika skuli za sekondari. Wengi wa vijana hawa hujiunga na masomo ya juu na huomba ajira hiyo kwa kujishikiza tu.

Vile vile, baadhi ya vijana waliomaliza Kidato cha Sita hujitolea kufundisha katika skuli za maeneo wanayoishi kwa moyo wa kizalendo wa kuwasaidia wenzao. Utaratibu huo umekuwepo muda mrefu kwa maelewano kati ya vijana na skuli zenyewe na bila ya kuingiliwa na Wizara. Wizara yangu inawapongeza kwa dhati vijana wote waliomaliza Kidato cha Sita ambao huamua kuwasaidia wanafunzi wenzao ili waweze kufanya vizuri katika masomo yao.

Mhe. Spika,

(a) Wizara itaendelea na utaratibu wake wa kuwapa mikataba ya ajira za muda vijana waliomaliza Kidato cha Sita ambao wanasaidia kufundisha madarasa ya sekondari kila hali ya fedha inaporuhusu. Kwa wale wanaojitolea maskulini, tunawaomba waendelee kufanya hivyo kwa utaratibu ambao wanakubaliana na uongozi wa skuli.

(b) Wizara inawashauri vijana wote waliomaliza Kidato cha Sita ama watahiniwa wa skuli au wa faragha *(private)* wajiendeleze zaidi kwa kutafuta nafasi za masomo ya juu na serikali itaendelea na utaratibu wa kuwapatia mikopo ya kuwawezesha kusoma katika Vyuo Vikuu na Taasisi nyengine za elimu ya juu.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, wanafunzi hao wa sekondari ambao hupata masomo yao kupitia vijana hao wa mitaani na kwa hao wanaochukuliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa makubaliano, baadhi ya watoto hao wanategemea kufanya mitihani yao ya mwisho mwaka huu.

(a) Je, Mhe. Waziri unafahamu kuwa wanafunzi hao ambao hupata mafunzo kupitia vijana hao wanatakiwa kutoa ada ya shilingi hamsini elfu kwa ajili ya mitihani.

(b) Ni kwa nini miaka ya nyuma ada hiyo ilikuwa inalipwa na wizara na sasa hivi wanachangishwa wanafunzi ikiwa kwa maana ya wazazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, mimi binafsi sina taarifa ya ada ya shilingi hamsini elfu. Mhe. Spika, jibu (b) ninachokielewa ni kwamba serikali imekuwa na utaratibu wa kulipia ada ya mitihani kila mwaka na sikumbuki kwamba tumeamua hivyo kwa siku za karibuni labda nilikuwa sipo katika vikao ambavyo lilikuwa limeamuliwa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri alikiri kwamba vijana hawa wanaomaliza kidato cha sita huenda katika maskuli kwa kujitolea kwa ajili ya upungufu wa walimu.

Je, kwa mujibu wa viwango vya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, walimu wa sekondari ni mwalimu na wanafunzi, ni uwiano gani unaotumika kujua kwamba pana upungufu wa walimu. Mwalimu mmoja anatarajiwa asomeshe wanafunzi wangapi. Je, wilaya gani inayoongoza katika Unguja na Pemba kwa upungufu wa walimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza sikusema kwamba vijana hawa ambao wanamaliza kidato cha sita hupelekwa maskulini kwa kuwasaidia hawa wanafunzi. Isipokuwa nilizungumza kwamba kuna baadhi ya vijana hujitolea wenyewe binafsi kwa makubaliano ya walimu pamoja na wanafunzi wenyewe. Lakini pia tuna utaratibu wa kuwaajiri kwa muda vijana waliomaliza kidato cha sita, ndicho nilichokizungumza.

Mhe. Spika, tunajua kwamba walimu wa sekondari kuna matatizo na kigezo kinachotumika ni idadi ya wanafunzi kwa walimu. Sina uhakika kwa sasa hivi lakini nadhani nitautafuta huo uwiano wa walimu na wanafunzi. Nasema sina uhakika nachelea kutoa jibu ambalo likaja likaenda kinyume.

Mhe. Spika, wilaya ambazo zinaongoza katika uhaba wa walimu ni Wilaya ya Kaskazini ‘A’ na Wilaya ya Micheweni na ndio maana tukafanya maamuzi ya kuwaajiri vijana hivi karibuni katika wilaya hizo.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa walimu wanaofundisha kwa kawaida huwa wanapewa mafunzo ya ualimu ama ya muda mrefu au ya muda mfupi. Kwa kuwa vijana hawa walioulizwa katika swali hili ni watu wanaojitolea wenyewe tu kwenda kufundisha. Kwa kuwa ualimu una maadili yake na walimu hupewa leseni kwa ajili ya kuwa wafundishe.

(a) Je, Mhe. Waziri kawahi angalau kuwapa mafunzo japo kidogo hivi ya ualimu na maadili yake.

(b) Lakini kama hajawapa mafunzo hayo na hawa wanakwenda skuli kusomesha, haionekani kwa kutokujua kwao maadili ya ualimu wakaharibu zaidi kuliko kutengeneza.

(c) Je, kuanzia hivi sasa wana mpango gani wa kuwafundisha vijana hawa kama hawajafundisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya walimu au vijana ambao wanamaliza masomo kidato cha sita na kama nilivyosema tunawaajiri kwa muda kwenda kufundisha katika maskuli yetu kwa ajili ya kupunguza tatizo la uhaba wa walimu katika maskuli yetu.

Mhe. Spika, tunafanya hivi kwa ajili ya kusaidia vijana ambao hasa katika masomo ya sayansi. Ni kweli kwamba vijana hawa wanakuwa hawajasomea ualimu lakini wanapopelekwa maskulini kunakuwa na utaratibu mzima wa kufanyia *orientation*. Baada ya hapo nadhani kunakuwa na usimamizi mzuri wa kuhakikisha kwamba wanachokifundisha na maadili yanafuatwa ili vijana wetu wasiharibikiwe.

Mhe. Spika, jibu (b) kama nilivyosema kwamba tunakuwa na utaratibu wa kuwasimamia vijana hawa ili tuone kwamba wanakwenda katika mstari unaotakiwa. Kila skuli tunao wasimamizi wa madarasa ya msingi lakini vile vile tunaita *section leader* ambao kazi yao kubwa ni kuwaangalia hawa walimu ambao wanafundisha. Kwa maana hiyo, kila siku mwalimu anatakiwa afanye *preparation* ambayo inatakiwa ikaguliwe na huyu *section leader* na mwalimu mkuu. Kwa hiyo, tunategemea sana kwamba kama ma-*section leaders* watafanya kazi zao vizuri basi maharibiko hayatatokea.

Lakini kuhusu mpango wa kuwafundisha vijana hawa. Mhe. Spika, tunatoa fursa mbali mbali za vijana ambao waliomaliza kidato cha sita kwenda kujiunga na mafunzo ya diploma katika vyuo vyetu mbali mbali. Mhe. Spika, tunao utaratibu wa kila mwaka kuwaruhusu walimu wetu kwenda kuchukua mafunzo hayo katika vyuo vya ualimu vilivyopo hapa nchini lakini hata pengine Tanzania Bara kwa wale ambao watapenda kwenda huko.

Kwa hiyo, mpango wa kuwafundisha tunao lakini pia tuna mpango maalum ambao tunauita *TAP* yaani *Teacher Advancement Program* kwa ajili ya walimu wetu ili kuweza kukuza viwango vyao. Hizo ndio juhudi ambazo tunazichukua katika kuhakikisha walimu wanafundisha vizuri na viwango vyao vinakua.

Nam. 29

Ugonjwa wa Malaria Zanzibar

Mhe. Haji Mkema Haji – Aliuliza**:-**

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imetangazia umma kwamba Zanzibar hakuna Malaria. Wakati huo huo dawa nyingi za kutibu Malaria ziligaiwa kwa ndugu zetu wa Tanzania Bara. Hivi sasa wananchi wetu wengi wanafika hospitali na katika vituo vya Afya wakilalamika kusumbuliwa na homa kali za vipindi zikiambatana na kichwa, kutapika na kutetemeka.

(a) Je, Mhe. Waziri hizi sio dalili za Malaria.

(b) Je, tangu kutoka tamko la kuwa Zanzibar hakuna Malaria, kuna utafiti wowote uliofanywa kuthibitisha kuwa Malaria bado haijarejea nchini.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika,

(a) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kuumwa na kichwa, kutapika na kutetemeka hizo ni dalili na ishara za ugonjwa wa Malaria. Aidha, napenda kuwaelewesha Wajumbe kwamba ishara na dalili hazitoshi kutoa uamuzi kwamba mtu ana ugonjwa wa Malaria bila ya kuchunguzwa damu. Wizara yangu imetoa wito kwa madaktari wote kutomtibu mtu kwa ishara na dalili bila ya kuhakikisha kuwa kweli ana vimelea vya ugonjwa wa Malaria.

(b) Naomba kusisitiza kwamba ugonjwa wa Malaria umepungua kwa kiasi kikubwa hadi kufikia chini ya asilimia moja na hakuna haja kwa kipindi hiki kufanya utafiti wa kuangalia kama ugonjwa umerejea. Bado mbu wa Malaria wapo ingawa wamepungua sana, vimelea vya Malaria hivi husambazwa na mbu na binadamu bado tupo. Jambo la muhimu linaloikabili nchi yetu hivi sasa ni kuhakikisha kuwa wananchi wetu wanaendelea kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa Afya kuhusu Malaria ili kutokomeza kabisa maradhi haya hatari na kuhakikisha kuwa hayarudi tena kama zamani.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza na mimi nikubaliane nae kwamba kwa kiwango kikubwa ugonjwa wa Malaria umetoweka, lakini yamejitokeza maradhi yanayofanana sana na Malaria. Kwa mfano *flu* kwa wingi, kuumwa na kichwa kikali na kwa hali ya kawaida mgonjwa hufikia kwamba ana Malaria. Je, Mhe. Naibu Waziri habari hii anayo, kama anayo utafiti gani umefanywa kuona kwamba tatizo hili linaondoka ?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, ninayo taarifa ya kuwa kuna *flu* kwa wingi na kuumwa na kichwa kikali na tunaielewa. Tunachoshauri kwamba wagonjwa wanapopata dalili hizi zote waweze kufika hospitali na kutibiwa.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, unapokwenda hospitali ukiwa na dalili zote za Malaria unapotolewa damu Malaria si aghlabu sana kuonekana, haionekani kabisa tena katika vituo vyote vya Mnazi Mmoja mpaka katika vituo vya binafsi.

Lakini mara nyingi daktari anatoa dawa baada ya kuona zile dalili na mtoto au wewe mwenyewe unapata homa kali na unapopewa zile dawa unapona. Sasa hii inakuwaje, Malaria haionekani lakini ukipewa dawa za Malaria unapona. Kuna sababu gani za kitaalam zinazosababisha mambo haya ?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kama nilivyosema kwenye jibu mama kwamba Malaria sasa hivi imeshuka sana kwa hivyo hata kuiona kwake wakati mwengine ni shida. Lakini inawezekana katika kupima damu kwa kipindi kile unajua tone linalochukuliwa ni moja, lakini mzunguko wa damu ni mkubwa katika mwili. Inawezekana kwa wakati ule haikuonekana lakini baadaye akiendelea kupima pengine ingeweza kuonekana.

Kwa hivyo, madaktari wakati mwengine wanatumia busara zao na kuona kwamba dalili hizi zimejitokeza ni za Malaria japokuwa sio kila dalili tulizozieleza ni za Malaria. Kuna dalili nyingi mojawapo alikuwa ameisema Mhe. Ame Mati Wadi. Kwa hivyo, wao wanachofanya ni kumpa mgonjwa huyu dawa za Malaria.

Lakini siku moja mimi nimekaa na wataalam wangu wakasema kwamba kuna pia maradhi mengine yapo yanatibika kwa kutumia hizi dawa za Malaria. Kwa hivyo, hiyo pia inachangia kwamba mtu anaweza kuwa hana Malaria, lakini kuna maradhi mengine yamejiingiza humo ndani.Kwa hivyo, anaweza kutumia dawa ya malaria.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza natanguliza shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Naibu Waziri kwa kutibu maradhi ambayo sio malaria kwa dawa za malaria, huu ni utaalamu mkubwa sana.

Mhe. Spika, swali ni kwamba imeondoka au kupungua malaria kwa kiwango kikubwa kwa sababu ya dawa inayotiwa majumbani. Kwa bahati mbaya kutokana na sababu maalum Mji Mkongwe hautiwi dawa hii ya kuondoa malaria na huo Mji Mkongwe kutokana na hali halisi ulivyo unaweza ukawa ni *store* ya mbu wa malaria kukaa na kusababisha kueneza maradhi hata mule ambamo dawa imeshapitishwa. Kwa sababu dawa inayotiwa ni ya kuuwa mbu wa malaria, sio kinga ya malaria katika kiwiliwili.

Sasa sijui Mhe. Waziri kachukua hatua gani ya kuwasaidia wananchi wanaoishi katika Mji Mkongwe kupata njia nyengine mbadala ya kuondoa hii malaria kama sehemu nyengine ili isiwe ni sababu ya kueneza ugonjwa huu kwa mule ambamo dawa imeshapita.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwa kweli hatua tulizochukua katika Mji Mkongwe, hivi karibuni tumegawa vyandarua vyenye dawa kwa Mji mzima kwa kila koo vyandarua viwili na tumewapa masheha wawagawie vyandarua hivyo. Katika kila ukoo ikiwa ni zaidi ya mtu mmoja basi tumewapa vyandarua viwili, ikiwa ni mtu mmoja peke yake basi ni chandarua kimoja. Ikiwa kuna mwananchi yeyote wa Mji Mkongwe ambaye hakupata chandarua au vyandarua basi aende kwa sheha wake akachukuwe na vipo.

Vile vile, tutachukua hatua za kufukiza kwenye mji wote dawa ya pairethram au na cambination pamoja na carocine, ili kuhakikisha kwamba wale mbu wenye kuwasumbua sumbua watu wa Mji Mkongwe basi tunawaondosha kabisa. Pamoja na hayo dawa tunazo za kutibu, wakati wowote waje na hakuna tatizo lolote Mhe. Spika.

Nam. 14

Nambari za Vyombo vya Moto

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kupitia Bodi ya Mapato, ilianzisha zoezi la ubadilishaji nambari za vyombo vya usafiri wa barabarani kwa ajili ya usalama na kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Lakini hivi sasa lipo tatizo la ukosefu wa nambari ambalo linazorotesha maendeleo ya zoezi hilo.

(a) Mhe. Waziri tatizo hilo linatokana na nini.

(b) Kwa kuwa baadhi ya watu wanatumia ukosefu huo kuweka nambari za vyombo vidogo (pikipiki) kwenye magari, Wizara yako inachukua hatua gani kuondoa tatizo hilo.

Mhe.Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.14 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba katika mwezi wa Novemba kulitokea upungufu wa vibati vya nambari (*number Plate*) kwa gari za binafsi (*Private*) kutokana na mtengenezaji wa vibati hivyo kufanya makisio madogo ya gari zitakazosajiliwa katika mwezi huo, ambapo walitarajia wapate nambari mpya. Makisio hayo hayakuzingatia magari yaliyoingia nchini.
Hali hiyo pia ilisababishwa na tabia ya baadhi ya wenye magari ya aina hiyo kusubiri tarehe za mwisho za usajili, ambapo magari mengi yalijitokeza kusajiliwa katika kipindi hicho kinyume na utaratibu uliowekwa wa kwenda kwa mujibu wa walivyosajiliwa nyuma.

Ukosefu huo Mhe. Spika, wa vibati ulidumu kwa wiki moja tu, vibati vilikuwa njiani kutoka China na vikafika nchini. Nathubutu kusema kukosekana kwa vibati hivyo hakukuzorotesha zoezi zima la usajili wa vyombo vya moto. Zoezi liliendelea kama kawaida na tatizo hili hivi sasa limemalizika kabisa.

Mhe. Spika, naomba kusisitiza kwamba tatizo lilitokezea zaidi kwa gari za *private* waliokuwa wanatumia vibati vyeupe. Naona nije na aina za hivyo vibati kabisa, ili waheshimiwa wapate kuviona. Vibati vyenyewe ni hivi vyeupe (kavishika mkononi waziri), hivi ndio *private* ambavyo vilikosekana. Hivi ndivyo vinavyokuja, yaani vinakuwa ni vyeupe kabisa (hebu vipitishe kwa waheshimiwa ili waweze kuviona). Kama nilivyosema vibati hivi vinaagizwa China moja kwa moja.

Kwa hivyo, baada ya yule mkandarasi wetu wa yule aliyefanya kazi hii ndugu Said Buda, baada ya kuzitia kwenye mashine ndio zinaandikwa nambari kwa kitaalamu kabisa. Kwa kweli ni *computerized*. Nilikwenda mwenyewe nikaona, kwa kweli ni ufundi mkubwa kabisa na kama wale wenyewe wataalamu walivyotuambia kuwa hii *technology* wameshaitwa na TRA kwenda kutoa utaalamu kule, wenzetu wanainunua hii *technology* na tutawauzia hatutowapa bure.

Kwa hivyo, hapa nambari zimeshatolewa kwa *private* vinakuwa vibati vyeupe. Kwa gari za taxi, daladala na gari za watalii vinakuwa vibati vyekundu hivi, kwa kweli vinavutia ni *technology* ya hali ya juu kabisa. Yale magari ya mizigo, nafikiri sote tunayajua njiani tunayaona, vibati vyake vinakuwa ni vya njano. Kama nilivyosema ni teknolojia ya hali ya juu ni *computerized* kabisa.

Mhe. Spika, nimesema katika ziara za kamati zako, nafikiri katika mzunguko ujao nimeshazungumza na ndugu Said Buda kwamba tuwapeleke kule washuhudie ile *technology* inayotumika ni jambo la kufurahisha kabisa.

Mhe. Spika, sambamba na hilo hata vibati vya vespa vya moto, mheshimiwa aliuliza kwamba kuna kuchanganyika, hapana. Vibati vya vespa ni vidogo ni vidogo kama hivi nilivyowaonesha hapa. Sasa hao wanaochukua hivyo vya vespa wakatia kwenye gari, basi hao wanadanganya na tumewaamuru *traffic* wawakamate mara moja.

(b) Mhe. Spika, kuhusu suala la kwamba kuna baadhi ya watu wanatumia ukosefu huo wa kuweka nambari za vyombo vidogo, yaani pikipiki kwenye magari. Mhe Spika, katika kutatua tatizo la ukosefu wa vibati kwa gari binafsi, bodi ya mapato Zanzibar kwa kushirikiana na mtengenezaji wa vibati hivyo ilichukua jitihada za kuondoa usumbufu kwa wananchi wanaotaka kusajili vyombo vyao, iliamua kutolewa stika ambazo wenye magari walitakiwa kuzibandika kwa muda hadi vibati hivyo vitakapotolewa. Stika hizo ndio zile kama ambazo tunaziweka kwenye vioo. Kwa kweli stika zile zinakwenda sambamba na *plate number* na hii iko *permanent* kabisa kwenye kioo, labda kioo ukivunje ndio itatoka hii. Kwa hivyo, walikosa vibati, lakini walipewa stika hizi wakaweka.

Mhe. Spika, hivi sasa tumefanya utaratibu tayari *traffic* Malindi wana mtambo wao maalum, nambari zote za magari kule wanazi-*monitor* na wanazo wao. Kwa hivyo, sasa kudanganya ukatia nambari nyengine *traffic* wakikukamata wanajua tu kwenye mtandao wao. Tumeendelea na tumefanya mtandao mzuri sana na mashirikiano nao vizuri kabisa kwa suala hili.

Mhe. Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba tatizo hilo hivi sasa limekwisha, vibati kwa ajili ya magari binafsi vipo tena kwa wingi na vinatolewa kama kawaida. Naomba nitumie fursa hii kuwaomba na kuwataka wananchi wote ambao bado wanatumia stika hizo kwenye magari yao kwamba vibati vyao vipo tayari na waende Ofisi za ZRB kuvichukua na kuvibandika kwenye gari zao. Ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri. Naona hivyo vibati vizunguke na upande huo, naona haviondoki hapa. Hebu tusaidie na huku vifike.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kwa majibu yake ambayo ni ya vitendo. Kuna majibu ya maelezo na majibu ya vitendo tumeona.

Mhe. Spika, swali langu ni dogo kabisa. Nimuulize Mhe. Waziri, hivi sasa Zanzibar ni kisiwa ambacho kina magari kiasi kwamba idadi imekuwa kubwa kuliko mahitaji ya wananchi, lakini ni maendeleo ambayo yanatafutwa katika nchi.

(a) Je, kwa kuwa kampuni hii iliyopewa kutengeneza vibati hivi vya nambari za magari, kwa nini haikutegemea kwamba kwa mtiririko wa magari yanaongezeka na muda walioweka wa usajili unakaribia kwisha wakaweka bajeti ndogo, je, walikusudia nini.

(b) Mhe. Spika, hivi sasa katika barabara zetu hasa nyakati za usiku kuna mapikipiki mengi, vespa na magari ambayo hutembea bila ya nambari ni kosa kisheria. Je, Wizara ina mpango gani wa kuliondoa hili, hasa tukizingatia kwamba ajali nyingi zinatokea kwa magari hayo.

Mhe.Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kama nilivyosema ilikuwa ni bahati mbaya, unajua siku zote kukadiria inapokuja hali halisi inakuwa hali ile tena huwezi kuiepuka. Kwa hivyo, tukubali hilo lilikuwa ni mambo ya kiufundi. Lakini tumsifu kwamba huyu fundi wetu alichukua hatua za dharura akaagiza hivyo vibati vikaletwa kwa ndege na tatizo lile likaondoka ndani ya wiki moja, halikudumu kabisa.

Mhe. Spika, hali hiyo ilitokezea kwa zile gari za *private* kwa vile vibati vyeupe tu, kwa sababu kama ulivyosema Mhe. Ali Suleiman Ali kwa kweli tunashukuru *Alhamdulillah*, gari za *private* zimekuwa ni nyingi mno. Tena aliwahi kusajili gari 800 kwa siku kwa wakati ule, maana yake walizidiwa na ule mzigo wakati ule. Kwa hivyo, kwa upande mmoja ni lazima tuisifu hii kampuni. Kama nilivyosema mkenda kuona zile mashine zao wenyewe mtafurahi ni *highly computerized* kabisa, sio kule kuandika kwa mkono na kwa njia hii huwezi kudanganya kabisa Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Spika, kuhusu suala la mapikipiki na vespa kutembea wakati wa usiku. Hili ni kweli, nafikiri sote ni mashahidi tunaona barabara zetu na vichochoro wenye mapikipiki wengi wanapenda kuharibu sheria. Nafikiri suala hili tutashirikiana na wenzetu wa Jeshi la Polisi hasa *traffic*. Kwa sababu kwanza wanawakoseshea mapato serikali na wanahatarisha usalama pia wa raia wakati wa usiku.

Sio wenye vespa tu hata wenye baskeli wengine hawana taa na wana dai haki sawa sawa njiani kama mtu mwengine yeyote. Kwa hivyo, hilo tutalichukua kwa pamoja tushirikiane ili kuweza kuliondoa. Ahsanate.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kweli kwanza nampongeza waziri kwa kuweza kulijibu swali kwa ufafanuzi kabisa mpaka kubeba mizigo ya vibati hivyo akaja nayo kwenye ukumbi huu.

Mhe. Spika, mimi napenda nimuulize ikiwa ni lake, kwa kuwa ZRB ilipofanya hivi ilitaka kuweka utaratibu mzuri wa matembezi ya gari njiani na usalama wa raia kwa jumla.

Je, suala la taxi kwa usiku hawajaliona kwa kuwa huna njia ya Zanzibar kusimamisha taxi usiku hasa katika siku kama hizi. Je, suala hili halijaonekana kwamba kuna haja ya taxi kubainika wakati wa usiku.

Mhe.Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nafikiri ushauri wake ni mzuri, anachokusudia yeye ni kwamba taxi zibainike wakati

wa usiku. Lakini moja tayari limeshafanyika, labda pengine kwa juu sasa, kwa sababu kwa nambari nafikiri *plate* zake ni nyekundu, wewe ukiona *plate number* nyekundu basi ujuwe hiyo ni gari ya abiria. Kwa hivyo, utaangalia mwenyewe kuna taxi nyengine ni kubwa siku hizi pengine mtu mmoja Mhe. Rashid unaingia mule peke yako na kama una mizigo yako. Lakini kama unataka *saloon* ndogo ndogo basi zile nazo zipo, lakini hata hivyo nafikiri umekusudia kuwe na taa kidogo ya juu inayoonesha *taxi.* Zipo baadhi ya *taxi* moja au mbili nimeziona tayari zimo mitaani. Sasa kama ulikuwa unashauri tufanye utaratibu kwa taxi zote. Basi nafikiri ni wazo zuri tutalizingatia.

Nam. 9

Miradi ya TASAF na PADEP

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Baadhi ya Miradi iliyoanzishwa kupitia Miradi ya TASAF na PADEP kwa lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi imeanza kudorora na mingine kufa kabisa. Mfano Miradi ya Maduka ya Pembejeo za Kilimo katika maeneo ya Kianga na Bumbwisudi, Jimbo la Dole ambayo iligharimu kiasi cha TZS 27,375,900/=.

(a) Je, Mhe. Waziri unajua kuwa maduka hayo yote yashakufa.

(b) Kwa kuwa dhamira ya miradi hiyo ni kupunguza umaskini katika hali hiyo, umaskini utapungua vipi.

(c) Kwakua palitumika fedha nyingi bila ya mafanikio Wizara imechukua hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijajibu naomba kutoa maelezo.

Miradi ya maduka ya Pembejeo za kilimo na mifugo yanalenga kutoa huduma za kuwasogezea wanajamii pembejeo za kilimo na mifugo karibu na maeneo yao ili kupatikana kwa wakati unaohitajika, ili waongeze uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo. Jumla ya Maduka 17 ya kuuzia Pembejeo za Kilimo na Mifugo yameanzishwa na Wanajamii wenyewe kupitia mradi wa PADEP kwa Unguja na Pemba. Maduka haya yamekuwa yakiwasaidia sana wanajamii wa

shehia hizo na shehia jirani kujipatia pembejeo wanazozihitaji na hata kuzipata kwa njia ya mkopo pindipo mkulima au mfugaji atakuwa hana pesa kwa wakati ule. Hivyo, naweza kusema kuwa kupitia maduka haya wanajamii wameweza kuongeza uzalishaji kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika, sasa naomba kujibu swali.

(a) Mhe. Spika, napenda kujibu kwamba maduka haya hayajafa bado yanaendelea kutoa huduma kwa wanajamii isipokuwa kuna changamoto zilizojitokeza katika uendeshaji wa maduka haya kama zifuatavyo :-

Baadhi ya viongozi wa maduka katika shehia hizi kutokuwa waadilifu katika usimamizi na uendeshaji wa maduka haya na hivyo kupelekea upungufu wa fedha za kuendesha biashara.

Pia, gharama kubwa za uendeshaji za kumlipa Mjumbe wa bodi ya udhamini wa madawa na muuzaji mwenye cheti halisi (*Pharmacist*) kiasi ambacho kimepelekea kutofikiwa kwa lengo halisi la miradi hii.

(b) Dhamira ya kupunguza umaskini bado ipo pale pale kwani utumiaji wa pembejeo kutokana na maduka hayo umeongeza uzalishaji kwa yale maduka yalioonyesha uongozi uadilifu . Mfano duka la Kombeni na mengineyo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira, naomba nimuulize kama ifuatavyo. Katika jibu mama amekiri kwamba yapo maduka hayana uadilifu, tukisema hayana uadilifu ina maana pameibiwa.

Je, hao waliobainika kuiba fedha za wenzao kwenye miradi hiyo wamechukuliwa hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwa kweli tulichokibaini labda ni maduka kama mawili, duka moja la Kianga na duka la Bumbwisudi. Kwa hivyo, tumo katika hatua za kuhakikisha kwamba tunashirikiana na Mkuu wa Wilaya na Wizara yetu ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa kupitia ma-*auditors* wetu watafanya kazi za ziada kwa sababu tayari kuna hitilafu zimejitokeza kwenye maduka haya mawili na baadae hatua zitachukuliwa. Kwa sasa hivi hatua za kisheria bado hazijachukuliwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nashukuru kunipatia nafasi hii kujibu swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwamba haya maduka ni ya wananchi wenyewe. Mradi wa PADEP umefanya utaratibu wa kuwasaidia hawa wananchi na wana kamati yao, kila duka au mradi katika shehia hizi wana kamati yao. Kwa hivyo, wanahusika na mambo yote yanayohusika na ununuaji, uendeshaji na kadhalika.

Kwa hivyo, kama kutakuwa na tatizo kama hili wenyewe hao ndio wa kwanza wanaohusika, sisi kama ni wizara tunakuja kwa mara ya pili. Kwa hivyo, sisi kama hatujapata shitaka lolote kwamba labda wizara tutatakiwa msaada gani tufanye.

Pamoja na hayo kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba tutayafuatilia sisi kwa upande wetu kama serikali ili kuona kwamba uadilifu unakuwepo na ikiwezekana hatua za kisheria tukishirikiana na kamati zile ziweze kuchukuliwa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Spika, hivi sasa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa sababu msimu wa mpunga umeanza wametoa mbegu za mpunga ambazo zinauzwa kwa Shs. 500/- kwa kilo, lakini mbegu hizo wamepeleka kwenye maduka ya pembejeo kwa bei hiyo ya Shs. 500/-, maduka hayo wanasema wao hawana faida maana wanapokea Shs.500/- warudishe Shs.500/-

(a) Je haoni kuwa hiyo ndio sababu ya kuua maduka hayo.

(b) Kwa kuwa maduka hayo ya pembejeo wamekataa kuzipokea hizo mbegu, je, wana utaratibu gani wa kuzisambaza kwa wakulima kwa bei hiyo ya Shs.500/-

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, hili suala ni kweli tumelipata kwamba wana matatizo hawa wanashindwa kununua. Serikali imepunguza kwa asilimia 50 pembejeo, lakini serikali haikufikiria wakati zoezi hilo linafanyika. Kwa hivyo, suala hili tumelichukua na hivi sasa tunalifanyia kazi kuhusu maduka hayo, tuweze nao kuwasaidia ili na wao waweze kufaidika na punguzo hilo la asilimia 50.

Nam. 23

Usafirishaji Maliasili za Misitu Baada ya Saa za Kazi

Mhe. Haji Mkema Haji - Aliuliza:-

Serikali ilitoa tangazo rasmi kwa wananchi na nakala za tangazo hilo zikasambazwa katika vyombo vya dola hasa Polisi ya kuwa ni marufuku kusafirisha bidhaa za maliasili za misitu kama vile Makaa, kuni, majengo, magogo na chokaa, baada ya saa 12.00 jioni.

(a) Je, Mhe. Waziri, amri hiyo ambayo mwanzoni ilitekelezwa vizuri sana, sasa imefutwa.

(b) Wakati wa mchana askari Polisi hushirikiana na Maafisa wa Misitu katika kuhakikisha amri hiyo inatekelezwa, lakini kwa sababu baada ya saa 12.00 jioni Maafisa wa Misitu hurudi majumbani, Polisi hawajishughulishi ipasavyo na kazi hiyo. Je, kwanini Polisi hawasimamii amri hiyo ya serikali wakati wa usiku.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ari hiyo bado haijafutwa na inaendelea kutekelezwa, lakini mashirikiano ya pamoja yanahitajika katika kufanikisha suala hili.

(b) Mhe. Spika, Askari Polisi hushirikiana na Maafisa Misitu katika kuhakikisha amri hiyo inatekelezwa kwa wakati wa mchana. Lakini kwa sababu baada ya saa 12.00 jioni Maafisa wa Misitu hurudi majumbani, Polisi huwa ndio wasimamizi wa amri hiyo ya serikali wakati wa usiku na wanaitekeleza. Ingawa kuna malalamiko ya kupitishwa kwa baadhi ya magari kwa nyakati hizo. Aidha, wizara itahakikisha kuwa na mashirikiano zaidi na polisi ili kuleta ufanisi mzuri katika kazi hii.

Hata hivyo, wizara kwa upande wake pia inafanya doria za usiku kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi ili kuona amri hiyo inatekelezwa. Pia, tunaomba viongozi wa Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Masheha, Madiwani, Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wote kushirikiana na Wizara yetu ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ili kuhakikisha kwamba suala hili tunalifanyia kazi sote kwa pamoja, ili kupambana na wale wahalifu wachache ambao wanajitokeza katika nchi yetu.

Mhe. Spika, hitilafu nafikiri tunaiona wenyewe, tumekata miti sana kwa hivyo sasa hivi Zanzibar tunachoambulia ni joto jingi, kuna

tofauti ukiangalia hali ya hewa ya Pemba na hali ya hewa ya Unguja. Tulipokwenda na Mkuu wetu mmoja kutoka Misri, alishangaa kuona hali ya hewa ya kule iko vingine na huku iko vingine. Nikamwambia labda hitilafu inayojitokeza ni kwamba Unguja sehemu kubwa kuna maheka, sasa watu wa maheka wanakuwa na wao pia sio watu wazuri, wanakata miti kila siku. Ukiangalia kule Pemba kidogo watu wanakaa katika mashamba yao kwa hivyo sio watu wengi ambao wanakata miti.

Pia, kuna tatizo lile ambalo linajitokeza nje ya nchi Europe na Asia, wao wana viwanda ambavyo wameharibu sana mazingira ya dunia na hitilafu wanayoipata sasa hivi.Kwa hivyo, wao wenyewe wanashindwa kuishi kule kutokana na baridi. Hapa kwetu namuomba Mwenyezi Mungu ajalie umeme urudi haraka ili utalii uzidi kuimarika zaidi. Amin.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Hivyo kukatwa miti na kuharibika mazingira haoni inasababishwa na misumeno ya moto, yeye anachukua hatua gani ya kudhibiti hivi sasa imekithiri.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, sote tunaisha Unguja na Pemba, misumeno hii ambayo imejitokeza hivi sasa imeingia katika kipindi hiki cha karibuni. Lakini kuna watu kila wanapoamka asubuhi wanahakikisha wanakata miti mitatu, minne mpaka mitano kwa siku moja. Lakini watu hao hao hawajitokezi kupanda miti pamoja na jitihada kubwa za serikali kwamba kila mwaka kwa kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira tuna siku ya upandaji wa miti kitaifa hapa Zanzibar, lakini pia serikali inazalisha miti zaidi ya laki tatu kwa ajili ya kuwagaiya wananchi bure ili tuweze kupanda, lakini watu wengi huwa hawapandi.

Kuna maeneo ambayo tumepanda miti, halafu bado wanatokea watu wahalifu ambao wanakwenda kuchimba kule mashimo ya mchanga na ile miti wanaitupa. Kwa hivyo, narudia kusema kwamba jukumu la kuhakikisha kwamba Zanzibar miti inaendelea kuwepo kwa wingi basi ni jukumu letu sote, tuhakikishe kwamba Waheshimiwa Wawakilishi na watu wengine tuanzishe na zile kamati za mazingira kwa wingi katika maeneo yetu, ili kuhakikisha jamii tunailinda na kuhakikisha miti haimaliziki.

Lakini pia suala la kuwepo kwa misumeno hii ya moto, kama tulivyosema katika kipindi cha nyuma, niliwahi kuulizwa swali la nyongeza hapa, kwamba tutatoa fidia gani kwa watu ambao wameleta misumeno hii. Nikasema Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira haijawahi kutoa amri kwamba tuletewe

misumeno tunashida ya kukata miti, miti tuliyokuwanayo ni kidogo hatutaki kukatwa miti. Kwa hivyo, msumeno wowote tukiukamata unafanya uhalifu, basi tutaufilisi na hatuwezi kuurejesha kwa fidia ya aina yoyote. Kwa hivyo, tunaomba kwa mashirikiano ya pamoja Masheha, Wakuu wetu wa Wilaya basi tuhakikishe kwamba tunawakamata wale watu ambao wana misumeno hiyo wakiifanyia uhalifu katika maeneo yetu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Haji Faki Shaali: Nakushukuru Mhe. Spika. Kwanza Mhe. Spika, na mimi nataka niungane na muuliza swali, kwa sababu hivi karibuni nilitembelea Bumbwini nikaona vile minazi inavyokatwa tulikuwa kwenye kamati, kwa kweli inasikitisha sana.

Mhe. Spika, jibu la nyongeza la Mhe. Naibu Waziri ni zuri, anasema kwamba misumeno wataikamata na wataifilisi. Je, sheria ipo itakayowapa uwezo wa kuikamata na kuifilisi hiyo misumeno. Kwa sababu vyenginevyo kama hakuna sheria basi baadae watakuja kushitakiwa wao. Je, ipo sheria inayowapa uwezo wa kuikamata na kuifilisi hiyo misumeno inayoangamiza nchi hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, alivyosema Mhe. Naibu Waziri ni kweli, lakini pamoja na hayo sisi wenyewe tu kama ni wizara hili suala linatuumisha vichwa tangu kuingia kwa hiyo misumeno ya moto hivi karibuni.

Mhe. Spika, wizara imefikiria kukaa pamoja na *counter party* wetu yaani Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji kuweza kufikiria kwa kina hatua gani za kuchukua kwa ajili ya kudhibiti suala la uingizaji wa misumeno, lakini zaidi ni ukataji wa miti ambayo inakatwa kwa misumeno ya moto.

Kwa hivyo, tutakaa pamoja na Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa ajili ya kuweza kufikiria njia au hatua gani ambazo zitatusaidia katika kudhibiti hali hiyo.

Nam. 3

Kuongeza Eneo la Hoteli ya *Manta Resort*

Mhe. Amina Iddi Mabrouk – Aliuliza:-

Manta Resort (zamani *Manta Reif*) iliyoko Makangale Mkoa wa Kaskazini Pemba, ni miongoni mwa Wawekezaji wa mwanzo kisiwani Pemba. Mwekezaji huyu takriban mwaka wa tatu sasa ameomba apewe eneo la ziada, ili aongeze nyumba za hoteli yake. Mpaka sasa mwekezaji huyo hajapata majibu ya ombi lake.

Mhe. Waziri nini sababu ya ombi la mwekezaji huyo kutopatiwa ufumbuzi?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusu yako naomba kujibu swali Nam. 3 la Mhe. Mjumbe kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa mwekezaji huyo ya *Manta Resort* alifanya maombi ya kuongeza ardhi, kwa ajili ya utanuzi wa mradi huo kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi *ZIPA* tangu tarehe 29 Agosti, 2006.

Baada ya kulifanyia kazi ombi hilo na kuangalia kiwango cha mradi, Mamlaka ya Uwekezaji ilizingatia ombi hilo na kuona ipo haja na uwezekano wa mradi huo kutanuliwa.

Tarehe 12 Machi, 2007 *ZIPA* iliwasilisha rasmi ombi hilo Idara ya Ardhi na Usajili ambayo ndiyo inayowajibika kwa ajili ya kumshauri Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi na Ardhi katika masuala yanayohusu ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji.Katika kulifanyiakazi suala hilo eneo lililoombwa lilibainika kuwa na mzozo wa umiliki.Hivyo, Idara ya Ardhi iliendelea kulifanyiakazi na haikuwezekana kwa *Manta Resort* kupewa eneo hilo. Ahsante.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kuhusu huu mradi wa *Manta Resort* mbali ya kupewa eneo, lakini wanaendesha shughuli kwenye lile Pango la Watoro ambalo ni mali ya wanakijiji. Je, kutokana na hali hiyo wananchi wale wanapata chochote kutokana na lile Pango kuendesha wale wawekezaji?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, si kweli kwamba Hoteli ya *Manta Resort* wanaendesha Pango la Watoro. Isipokuwa ni Kamati ya Maendeleo ya eneo lile wakiwezeshwa na Hoteli ya *Manta Resort* ndio wanaoendesha mradi ule pamoja na miradi mingine kadhaa ikiwemo kilimo na mambo mengine.

Kwa hivyo, katika hoteli ambazo tutazipigia mfano kwa kufanyakazi na jamii inayoizunguka ni hoteli hii.Kwa hiyo, wananchi wale wanafaidika vizuri na Pango la Watoro pamoja na miradi mingine.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Afisi ya Mkurugenzi wa Masharti

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liujadili pamoja na kuupitisha Mswada wa Sheria wa Kuweka Masharti ya Uanzishaji na Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na Mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha mswada nilioutaja hapo juu katika kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuimarisha ujenzi wa taasisi muhimu ya utawala bora.

Vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa hatua yake aliyoichukua ya kuwateua Wajumbe wawili kutoka upande wa Upinzani, Mhe. Juma Duni Haji na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kuwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu, ili tushirikiane nao katika kujenga maendeleo ya nchi yetu ikiwa ni moja ya kutekeleza kifungu cha Katiba ya nchi.

Pia, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe hao kuwa tunaye tena Mhe. Juma Duni Haji na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui tunamkaribisha, kwa ajili ya kufanyakazi nzuri ya kujenga mstakbali wa nchi yetu.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kuishukuru Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala ya Baraza hili tukufu, chini ya uongozi wa Mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Haji Omar Kheir kwa kuupitia mswada huu kwa makini sana na kutoa maoni pamoja na michango ambayo imesaidia sana kwa ajili ya kuufanya mswada huu uwe bora zaidi.

Baadhi ya michango yao ilikuwa ya kitaalamu kabisa, ambayo naamini tusingeweza kuipata hata kutoka kwa wanasheria wazoefu *(Makofi).*

Mhe. Spika, kuwepo kwa Afisi Huru ya Uendeshaji wa Mashtaka ni moja ya misingi muhimu ya kusimamia sheria za nchi na kujenga utawala wa sheria. Jambo hili limesisitizwa na Tamko Rasmi la Umoja wa Mataifa la mwaka 1990 ambalo maarufu linalojulikana kama *Havana Declaration.*

Afisi hiyo huwa kama mezani ya kupima aina ya utekelezaji wa utawala wa sheria kwa upande mmoja, nakuhakikisha kuwa mamlaka ya dola ya kushtaki,

yaani *precaution and desecration* hayatumiki vibaya kwa upande wa pili. Takriban nchi zote zenye mfumo wa kidemokrasia na unaojali utawala wa sheria zimeanzisha afisi huru za uendeshaji wa mashtaka.

Mhe. Spika, ili afisi hiyo iwe huru ni lazima iwe sio tu na watendaji mahiri na waadilifu, Lakini ni muhimu muundo pamoja na mfumo wake wa kitaasisi uwe wazi wenye kufahamika. Pia, unaoweza sio tu kutekeleza uhuru huo, bali pia kuwajibika pale uhuru huo unapotumika vibaya.

Kama tunavyoona mswada huu madhumuni yake makubwa ni kuimarisha utendaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kuweka mfumo unaotazama masharti na matarajio niyotangulia kuyataja *(Makofi)*.

Mhe. Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilianzishwa chini ya kifungu cha 56 A cha Katiba ya Zanzibar mwaka 1984, kilichoingizwa kwenye Katiba kupitia marekebisho ya nane ya Katiba ya mwaka 2002. Kwa hivyo, zaidi Katiba inaeleza utaratibu wa uteuzi, sifa, muda wa utumishi, mamlaka, kazi, uhuru na kinga ya uteuzi wa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye yupo sasa aliteuliwa Julai mwaka 2002 kwa muda wa miaka mitano, baada ya kumaliza muda wa miaka mitano aliteuliwa tena kwa kipindi cha miaka mitano hapo mwaka 2007.

Mhe. Spika, tokea mwaka 2002 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imekuwa ikiendeshwa kwa kufuata zaidi Mamlaka ya Mkurugenzi aliyopewa ndani ya Katiba, masharti ya sheria ya nyendo za jinai Nam. 7 ya mwaka 2004, pamoja na taratibu zilizozoeleka za uendeshaji wa afisi za serikali.

Hadi sasa hakuna sheria mahsusi au muongozo rasmi unaoeleza uendeshaji wa kazi za afisi hiyo kitaasisi. Kwa sababu hizo na kuwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni muhimu sana katika usimamizi wa sheria za jinai. Kwa kweli inafanyakazi kwa karibu sana na Mahakama na Polisi, kuhusiana na mambo mbali mbali ya kiutawala pamoja na uendeshaji yamejitokeza katika kipindi cha miaka 7 iliyopita, ambayo yanahitaji msimamo wa wazi wa kisheria.

Mambo hayo ni pamoja na uanzishwaji wa afisi yenyewe kama taasisi, muundo wa afisi pamoja na upeo wa uhuru katika kazi zake. Pamoja na hayo, suala la mahusiano baina ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Polisi katika kazi zao linahitaji kuwekwa bayana zaidi *(Makofi)*.

Aidha kazi, mamlaka na uwajibikaji wa Mkurugenzi vinahitaji kuwekwa wazi zaidi.Kutokuwepo kwa muungozo rasmi wa kitaasisi, kumepelekea baadhi ya matatizo yakiwemo mgongano wa majukumu na baadhi ya kazi kuonekana kama hazina mwenyewe, kwa vile Polisi wanadhani ni za Mkurugenzi wa Mashtaka na yeye anafikiri kuwa ni za Polisi.

Mhe. Spika, eneo jengine muhimu ambalo linahitaji kushughulikiwa ni pamoja na Kanuni za Maadili ya Watumishi, umuhimu wa afisi na namna ya kuzisimamia. Baadhi ya watumishi wa afisi hii kama vile wanasheria na waendesha mashtaka wamepewa mamlaka na majukumu nyeti yanayoendana na uhuru wa watu pamoja na maslahi ya jamii kwa jumla.

Kwa hivyo, hapana budi mamlaka na majukumu hayo yasimamiwe kwa uadilifu, ambao si wa kutiliwa mashaka. Hivyo, lazima suala hili liwekwe bayana na usimamizi wake uwe wazi.

Mhe. Spika, uzoefu uliopatikana kutoka nchi zenye afisi kama hii, zikiwemo Tanzania Bara, Afrika ya Kusini, Uingereza, Canada, Australia, Denmark na kadhalika unaonesha kuwa wametunga sheria maalum za kueleza uanzishwaji, utendaji pamoja na muundo wa kiafisi wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kwa kweli nchi zote hizo zimefanya hivyo baada ya kuona matatizo yaliyojitokeza kwa kutokuwepo sheria mahsusi ya Afisi Huru ya Mashtaka.

Kwa mfano Tanzania Bara Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imekuwepo tokea mwaka 1906, lakini sheria mahsusi ya afisi hiyo imetungwa mwaka 2006. Nchini Australia nayo ingawa taasisi hiyo imekuwepo tokea mwaka 1950, lakini sheria mahsusi za Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika ngazi ya majimbo na serikali kuu zimetungwa kati ya miaka ya 1983 na 1986.

Vile vile, nchini Afrika ya Kusini ingawa Afisi ya Taifa ya Uendeshaji Mashtaka imeanzishwa chini ya ibara ya 179 ya Katiba ya Afrika ya Kusini ya mwaka 1996, lakini sheria mahsusi ya uendeshaji wa afisi hiyo imetungwa mwaka 1998 kupitia sheria Nam.32 ya mwaka 1998.

Uingereza nako ingawa afisi hiyo ilianzishwa rasmi mwaka 1880 kwa majina tofauti, lakini sheria mahsusi ya afisi hiyo imetungwa mwaka 1985 baada ya nchi hiyo kuunda tume mnamo mwaka 1978 ya kuchunguza na kupendekeza namna ya kuimarisha uendeshaji wa mashtaka.

Mhe. Spika, mswada huu umezingatia uzoefu huo wa nchi nyengine kadhaa na mazingira halisi yaliopo Zanzibar *(Makofi).*

Mswada kwa ujumla unazo sehemu tano. Sehemu ya kwanza ni juu ya masharti ya awali ambayo inaeleza jina la sheria, matumizi yake pamoja na tafsiri ya maneno yaliyotumika.

Sehemu ya pili inaeleza uanzishwaji na uendeshaji wa afisi, mambo hasa yaliyoshughulikiwa na sehemu hii ni pamoja na kuanzishwa kwa afisi, uteuzi wa Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi, muundo wa afisi, watumishi, kazi pamoja na bajeti ya afisi.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu inaeleza utaratibu wa utendaji wa afisi, yaani mambo yanayohusu udhibiti pamoja na utaratibu wa mashtaka. Mambo hasa yaliyotajwa ni pamoja na kazi, mamlaka ya Mkurugenzi, uteuzi wa waendesha mashtaka, taratibu za kukasimu mamlaka ya Mkurugenzi, utoaji wa sera na miongozo ya mashtaka, utaratibu wa upelelezi, mambo yanayohusu mashtaka ya watu binafsi pamoja na utekelezaji shughuli zinazohusiana nazo.

Kwa kweli mengi yaliyoelezwa kwenye sehemu hii hivi sasa yanatekelezwa kwa kutumia sheria, kama vile nyendo za jinai na baadhi ya mambo yanatekelezwa bila ya kuwepo sheria, isipokuwa kufuata mazoea ya utekelezaji.

Sehemu ya nne ya mswada imeeleza uwajibikaji katika kutekeleza mamlaka na kazi za Mkurugenzi pamoja na afisi. Mambo hayo ni pamoja na uwazi katika maamuzi ya kimashtaka, utekelezaji wa mamlaka kwa nia njema, Kanuni za Maadili na tathmini ya utendaji.

Madhumuni ya masharti hayo ni kuweka misingi ya uwajibikaji ambayo itasaidia kujenga imani kwa wananchi juu ya usimamizi wa sheria za nchi yetu.

Mhe. Spika, sehemu ya tano ambayo ni ya mwisho ya mswada inaeleza mambo mbali mbali, ambayo yanajumuisha Kinga kwa Maafisa wakati wanapokuwa kazini, uendelezaji wa ufanisi katika Mfumo wa Usimamizi wa Jinai, uanzishaji na utendaji wa Kamati ya Mashauriano, Makosa na Adhabu, Utungaji wa Kanuni, Marekebisho ya Lazima na Masharti ya Mpito.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba mswada huu wameupata na kuusoma, basi wachangie mswada na hatimaye kuupitisha, ili iwe sheria itakayosaidia kuimarisha juhudi zetu za kujenga utawala bora katika nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uanzishwaji na Uendeshwaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mambo mengine Yanayohusiana nayo.

Mhe. Spika, awali ya yote, nachukua fursa hii muhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa neema zake zisizo na ukomo kwetu, ikiwa ni pamoja na kutujaalia uhai na afya njema, kiasi kwamba tumemudu kukutana hapa leo, ili kujadili mambo mbali mbali yenye manufaa kwetu binafsi na kwa wananchi wetu kwa ujumla.

Kwa hakika kama si taufiki na rehema za Mwenyezi Mungu juu yetu, basi huenda muda huu tusingekuwa hapa tukipitia Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uanzishwaji na Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mambo Yanayohusiana Nayo. Lakini kwa vile rehema za Mwenyezi Mungu zimeenea kwa waja wake, basi ndio maana muda huu tuko hapa tayari kujadili na hatimae kupitisha mswada huu.Mhe. Spika, pili napenda kuendeleza shukurani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuniruhusu nitowe mchango kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na wananchi wa Jimbo la Tumbatu.

Mhe. Spika, napenda kuchukuwa nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Aman Abeid Karume, kwa kutumia haki yake ya kikatiba kwa kuwateuwa Wajumbe wa Baraza la Wawaklishi kutoka Kambi ya Chama cha Upinzani, CUF ambao ni; Mhe. Juma Duni Haji na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar *(Makofi)*.

Kwa kweli kama ambavyo imeelezwa katika kifungu cha 66 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kwa hakika kuteuliwa kwa Wajumbe hawa kunaleta matumaini makubwa ya maendeleo, umoja na mshikamano mzuri, kwa ajili ya mstakabali mzuri wa nchi yetu na maslahi ya taifa zima kwa ujumla.Mhe. Spika, napenda pia, kuwapongeza Wajumbe wetu walioteuliwa na nathubutu kusema kwamba kuteuliwa kwao haikuwa bahati tu, ila ni kutokana na sifa zao na uzowefu wao mkubwa waliokuwa nao, hususan katika nyanja ya kisiasa ambapo hata Mhe. Rais kawakubali na kuweza kuwateuwa *(Makofi)*.

Hatuna budi kuwapongeza kwa hilo na nimatumaini yetu kwamba kuwepo kwao, kutaongeza chachu ya Baraza la Wawakilishi katika kutekeleza majukumu yake mbali mbali, kama yalivyoelezwa kwenye kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Spika, sitomtendea haki hata kidogo iwapo sitompongeza Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi CUF Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kumtambua Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hatua ambayo ni muhimu sana katika ujenzi mpya wa taifa letu, hasa katika suala la kuleta umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi wa Zanzibar, hali ambayo itapelekea kuimarika kwa amani na utulivu wa nchi yetu *(Makofi)*.

Vile vile, akiwa ni kiongozi aliyeonesha mfano mzuri wakuigwa na wananchi wa kawaida. Kwa hakika hatua hii inaleta faraja na matumaini mazuri juu ya mwelekeo wa siasa ya nchi yetu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, wakati wa kupitia na kuchambua mswada huu uliyopo mbele yetu katika kamati, nathubutu kusema kuwa kamati yetu ilipata ushirikiano wa kutosha kukamilisha majukumu yake kutoka kwa watendaji wote wa wizara hii pamoja na Kaimu Waziri wa Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora Zanzibar ambaye pia ni Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, Mhe. Hamza Hassan Juma. Hivyo, kamati yetu inawashukuru wote hao kwa pamoja kwa mashirikiano mazuri waliyotupa kwa muda wote *(Makofi)*.

Mhe. Spika, tutakuwa wezi wa fadhila tusipoipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kwa kuutangaza mswada huu kwenye Gazeti la Serikali, hatimaye kufikishwa katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi mapema. Jambo hili limezidi kuzipa imani Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, kuwa maoni na mapendekezo wanayoyatoa yanathaminiwa na serikali hii.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ina Wajumbe 10, ambao walihusika kikamilifu katika kuupitia mswada huu. Wajumbe wenyewe ni:-

1. Mhe. Haji Omar Kheri	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Haji Mkema Haji	-	M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Zahra Ali Hamad	-	Mjumbe
4. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Mjumbe
5. Mhe. Abdalla Juma Abdalla	-	Mjumbe
6. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin	-	Mjumbe
7. Mhe. Fatma Abdalla Tamim	-	Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
9. Mhe. Najma Khalfan Juma	-	Mjumbe
10. Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	-	Mjumbe
11. Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
12. Ndg. Abdalla Ali Shauri	-	Katibu

Mhe. Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilianzishwa kama Taasisi Huru ya Serikali kupitia Marekebisho ya nane ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, yaliyofanywa mwaka 2002, kufuatia kuingizwa kifungu Nam. 56 A cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Miongoni mwa kazi za Afisi hii ni kuanzisha mashtaka katika kesi za jinai katika Mahakama yoyote Zanzibar, isipokuwa Mahakama za kijeshi.

Mhe. Spika, utaratibu huu mpya umeweza kusaidia kujenga mfumo bora wa uendeshaji kesi Mahakamani, kwa kiasi kikubwa kupunguza mrundikano wa kesi Mahakamani. Aidha, kuanzishwa kwa afisi hii kumewapunguzia kazi Askari Polisi ambao ndio waliokuwa wakibeba jukumu la kufungua mashataka na kufanya upelelezi.

Kwa hivi sasa kazi kubwa ya Askari Polisi katika kusimamia mfumo wa upatikanaji wa haki ni kufanya upelelezi. Mhe. Spika, hali hii kwa kiasi kikubwa imechangia kuimarika kwa utawala bora na utawala wa sheria nchini.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uanzishwaji na Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mambo Yanayohusiana Nayo, umetungwa ili kutoa maelezo zaidi ya kiutendaji, kutokana na kuwa Katiba ya Zanzibar haikuzungumzia masuala haya.

Kamati yetu imegundua kuwa Miswada ya Kiswahili inayowasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi huandikwa bila ya kufuata mpangilio maalum wa herufi *"alphabetical order"* kwenye kifungu cha Tafsiri ya Maneno, wakati, ile ya Kiingereza huandikwa kwa kufuata mpangilio huo.

Kwa kuwa mpangilio wa herufi kwenye kifungu cha Tafsiri ya Maneno ni miongoni mwa kipengele muhimu cha kuzingatiwa na Muandishi wa Sheria *"Legislative Drafter"* wakati anaandaa mswada, na kwa kuwa kifungu cha 87 (2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinaelekeza Mhe. Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 87 (2) kinasema hivi:-

> "Kuwa Miswada inayowasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi itaandikwa kwa lugha ya Kiswahili na ikihitajika kwa lunga ya Kiingereza"

Hivyo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inawashauri Waandishi wa Sheria kukitilia maanani kipengele hiki, ili miswada yetu isionekane na dosari hili. Aidha, itapelekea kuonekana kuwa miswada inayowasilishwa mbele ya Baraza

hili imeandaliwa na watu mahiri na wenye uzoefu wa kutosha kuhusiana na mambo haya ya kiuandishi wa sheria.

Pamoja na maelezo yangu hayo, endapo tafsiri za maneno zitaandikwa kwa mpangilio wa herufi, kutamsaidia mtumiaji wa sheria husika kuona neno analolihitaji kwa haraka zaidi.Hivyo, itamuondoshea usumbufu mtumiaji huyo.

Mhe. Spika, kawaida Mswada wa Kiswahili kuandikwa ikiwa ni tafrisi ya Mswada wa Kiingereza. Kwa mnasaba huo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inashauri kuwa kwa upande wa kifungu cha Tafsiri ya Maneno, basi maneno yapangwe kutokana na mpangilio wa herufi na sio ufuatwe Mswada wa Kiingereza kama inavyofanyika hivi sasa. Kamati inazidi kusisitiza hili kutokana na sababu ilizozieleza hapo kabla.

Mhe. Spika, kwa kuwa mswada na hatimaye sheria inayotungwa na Baraza la Wawakilishi hutumiwa pia na wananchi wa kawaida, tunakiri kuwa maneno *"terminologies"* za kisheria ni za kitaalamu zaidi *"very technical"*, sambamba na kufuata maelekezo ya Katiba ya Zanzibar.

Kamati yetu ilishauri ni busara Mhe. Rais wa Zanzibar akatia saini nakla zote mbili za miswada, ili kuondosha usumbufu kwa wananchi pamoja na kuimarisha utawala bora na misingi ya utoaji haki. Aidha, jambo hili litaonesha ni kiasi gani nchi yetu inatii maelekezo yaliyokuwemo ndani ya Katiba tuliyoitunga sisi wenyewe *(Makofi)*.

Mhe. Spika, katika kifungu hiki cha 3 cha Mswada huu, Kamati yetu ilipendekeza pia, kuongezwa tafsiri ya neno "kamati" ambalo lilipendekezwa litafsiriwe kama ifuatavyo;-

> "Maana yake ni Kamati ya Mashauriano iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 23 (1) cha Sheria hii"

Hii ni kutokana na kuwa neno hili limejitokeza katika vijifungu mbali mbali vya kifungu cha 23 cha Mswada huu bila ya kuandikwa kwa ukamilifu. Hivyo, ili kuleta urahisi wa uelewa kwa mtumiaji wa Mswada huu Kamati yetu ilipendekeza kutafsiriwa neno hili.

Mhe. Spika, kamati yetu ilitoa pongezi serikalini kwa kumruhusu Mkurugenzi wa Mashtaka kutoa kibali kwa Waendesha Mashtaka Binafsi *"Private Prosecutors***"** ingawa jambo hili sio geni miongoni mwa nchi nyingi za Jumuia ya Madola. Mhe. Spika, katika kutekeleza hili, kutaizidishia nchi yetu kuwa ni mahiri katika kufuata mfumo wa demokrasia, sambamba na kuimarisha utawala bora na misingi ya utoaji haki. Hii ni kutokana na kuwa mfumo huu utatoa

fursa kwa yule aliyeshtakiwa kumchagua Muendesha Mashtaka atakayemhisi yeye anamfaa na itaondosha malalamiko yasiyo ya msingi dhidi ya Serikali. Kwani hivi sasa wananchi wanahisi kuwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Askari Polisi wapo kitu kimoja katika kuzikwamisha kesi jambo ambalo halina ukweli ndani yake.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilipendekeza kuwa neno **"**Kasma**"** liliopo kwenye kifungu cha 8 cha Mswada huu kisomeke kuwa ni **"**Fungu". Kamati ilipendekeza hili baada ya kugundua kuwa neno fungu ndilo hasa linaloleta maana zaidi ukilinganisha na neno lililokuwepo.

Mhe. Spika, tulipendekeza pia, baadhi ya maneno yaliyotokana na makosa ya kiuchapaji. Baadhi ya maneno hayo ni; katika ukurasa wa 151, kifungu cha 11(1) mstari wa tatu kutoka juu neno **"**mamllaka**"** Kamati ilipendekeza lisomeke **"**mamlaka**"**, aidha, mstari wa pili kutoka chini neno **"**mamalaka**"** lilipendekezwa lisomeke **"**mamlaka**"**. Pia, katika ukurasa wa 155, kifungu cha 17(c) mstari wa kwanza neno la kwanza **"**atawasharuri**"** Kamati ilipendekeza lisomeke **"**atawashauri**"**. Mhe. Spika, marekebisho mengine ya maneno kama haya yanapatikana kwenye waraka wetu wa mapendekezo ya marekebisho.

Mhe. Spika, wakati Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaupitia na kuujadili Mswada ulio mbele yetu, iligundua kuna mgongano wa baadhi ya vijifungu. Kwa mfano katika Mswada wa Kiswahili kifungu cha 11 kinaonekana kina vijifungu saba wakati ule wa Kiingereza unaonesha unavijifungu vinane. Mhe. Spika, tunapenda kuliarifu Baraza lako kuwa kifungu cha 11 cha Mswada wa Kiswahili kisomeke kuwa kuna vijifungu vinane. Isipokuwa, kijifungu cha (5) kisomeke cha (6) na vijifungu vinavyofuata vitaathirika kwa kufuata utaratibu huo.

Aidha, kijifungu kipya cha (5) kisomeke "Uteuzi wa Mwendesha Mashtaka hautakuwa batili kwa sababu pekee ya kukiukwa utaratibu katika uteuzi na hakutakuwa na Mwendesha Mashtaka atakayezuiliwa kutekeleza kazi au uwezo wake kwa sababu hiyo isipokuwa kwa amri itayotolewa na Mkurugenzi".

Mhe. Spika, aidha, Kamati yetu ilipendekeza kifungu cha 22(2) cha Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uanzishaji na Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mambo Yanayohusiana Nayo kifanyiwe marekebisho kama ifuatavyo:- Kijifungu (c) kisomeke "kuandaa mkutano au mkusanyiko na kushiriki katika mikutano au mikusanyiko iliyoandaliwa na taasisi nyenginezo". Hivyo, baada ya mapendekezo ya marekebisho hayo kijifungu (d) kimefutwa na kijifungu (e) sasa kitasomeka(d). Aidha, kiongezwe

kijifungu kipya (e) ambacho kitasomeka “kubuni na kutoa mipango ya mafunzo yanayohusika”, na vijifungu vilivyosalia vitasomeka kama vinavyoonekana kwenye Mswada husika.

Mhe. Spika, kwa kuhitimisha, haya ndio maelezo ya uchambuzi wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa muhtasari. Kama yapo maeneo mengine ambayo kwa bahati mbaya sikuweza kuyagusia, natumai Waheshimwa Wajumbe wengine wa Kamati hii watayazungumzia pindi watapopata fursa ya kuchangia katika Mswada huu. Mimi binafsi na kwa niaba ya Wapiga kura wangu pia tunaunga mkono Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uazishwaji na Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mambo Yanayohusiana Nayo kwa asilimia mia.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Mhe. Haji Faki Shaali): Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii lakini kabla ya kutoa maoni yangu nataka nikiri kwamba mara hii nimeathiriwa sana na ukosefu wa umeme kwa hivyo sina mchango mkubwa. Kwa sababu mimi usomaji wangu ni wakati wa alfajiri nikishasali nikae na kompyuta yangu nifanye kazi zangu, lakini vyenginevyo nakuwa napata tabu sana. Kwa hivyo, mchango wangu Mhe. Waziri usifikirie labda nimedharau sikuchukua juhudi ya kukusaidia lakini nimeathirika sana na umeme.

Mhe. Spika, namshukuru Mwenye Mungu kwa kunijaalia afya njema nakuweza kusimama kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya kuweka masharti ya Uanzishaji na Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na mambo yanayohusiana nayo. Aidha, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii muhimu.

Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa katika mswada wenyewe kifungu cha 56 (a) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 ambacho kiliingizwa kupitia marekebisho ya Katiba ya 2002 kimeanzisha nafasi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Katiba imeeleza wajibu wa Mkurugenzi wa Mashtaka lakini haijataja lolote kuhusu afisi yake kama kwamba atafanya kazi peke yake.

Mhe. Spika, nakubaliana na hoja iliomo katika madhumuni na sababu kwamba kutokana na unyeti wa afisi hii, haitoshi kutegemea uhalali na taratibu za kimazoea za uendeshaji wa ofisi za serikali hivyo kuletwa mswada huu ni jambo la lazima.

Mhe. Spika, mswada huu unaelezea mambo makubwa yafuatayo:-

(a) Uanzishaji wa Afisi
(b) Muundo wa Afisi
(c) Wafanyakazi wa Afisi (pamoja na ajira zao)
(d) Kazi za Afisi
(e) Fedha na bajeti ya Afisi
(f) Kazi na mamlaka ya Mkurugenzi
(g) Kukasimu madaraka
(h) Uteuzi wa waendesha mashtaka
(i) Sera na muongozo wa uendeshaji mashtaka
(j) Uratibu wa upelelezi
(k) Kanuni za maadili
(l) Kinga ya maofisa
(m) Makosa na adhabu n.k

Mhe. Spika, mambo haya hayawezi kutekelezwa kwa taratibu za kiofisi kama nilivyosema mwanzo.Kwa hivyo, kuwepo kwa sheria hakuwezi kuepukwa.

Mhe. Spika, chini ya kifungu cha 9 (2) (c) Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa na mamlaka ya kuelekeza Polisi na taasisi nyengine yoyote ya upelelezi wa makosa ya jinai. Lakini Polisi wanafanya kazi chini ya Sheria ya Polisi. Sehemu ya nne ya Sheria ya Polisi (chapter 322 kifungu cha 27 – 43) inatoa maelekezo ya jumla kwa askari kuhusu utekelezaji wa kazi zao likiwemo suala la upelelezi wa makosa ya jinai. Je, Polisi hawatapata mgongano kwa kutumikia Sheria mbili hizi?

Mhe. Spika, katika baadhi ya wilaya bado uendeshaji mashtaka unafanywa na Polisi badala ya waendesha mashtaka kutoka katika Afisi hii. Je, baada ya Sheria hii kupitishwa Afisi hii itaharakisha kupeleka waendesha mashtaka ili kudhibiti tatizo la wananchi kubuniwa kesi na kupelekwa Mahakamani bila ya hata upelelezi kufanyika?

Mhe. Spika, kifungu cha 7 (b) cha Mswada Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ina jukumu la kushauriana na taasisi nyengine za serikali, kutoa msaada na ushauri kwa waathirika wa uhalifu na mashahidi wa kesi za jinai. Je, msaada huu utahusu kuwasaidia mahabusu na wafungwa walioko magerezani ambao wanateswa? Ikiwa jawabu ni hasi huoni kwamba ipo haja ya wafungwa kupata msaada wa ushauri kutoka afisi hii.

Mhe. Spika, chini ya kifungu cha 16 (1) (a) Mkurugenzi wa mashtaka atakuwa na uwezo wa kufanya mashauriano yanayohusiana na maombi ya kusafirisha

washtakiwa wa nchi nyengine waliopo Zanzibar. Suala hili linawezekana bila kuishirikisha Serikali ya Muungano.

Mhe. wa Spika, chini ya kifungu cha 20 cha mswada huu, Mkurugenzi wa mashtaka ataandaa vigezo vya utendaji vitavyopaswa kufuatwa na kufikiwa na kila kitengo cha uendeshaji mashataka na kwamba atateua mtu au taasisi yenye sifa ili ifanye tathmini ya utendaji. Suala ninalopenda kujua mtu au taasisi itakayopewa kazi hiyo ni ya ndani au nje ya nchi?

Mhe. Spika, chini ya kifungu cha 22 (2)(c) Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ina uwezo wa kuandaa mkutano au mkusanyiko wa aina yoyote. Kwa uwezo huo, naiomba Afisi hii ifanye semina moja kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, viongozi wa jeshi la Polisi na viongozi wa vikosi vya SMZ ili tuelimishwe juu ya suala la upelelezi, uendeshaji mashtaka na utunzaji wa wafungwa walioko jela

Mhe. Spika, kifungu cha 23 cha mswada kinazungumzia kuhusu kamati ya mashauriano. Chini ya kifungu hiki mwenyekiti atakuwa Jaji wa Mahakama kuu na sio Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye ndiye Mkuu wa taasisi husika. Kuna sababu zipi za msingi za kufanya hivyo?

Mhe. Spika, licha ya Jaji wa Mahakama Kuu ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati pia Mrajisi wa Mahakama Kuu atakuwa Mjumbe wa kamati, kuna sababu zipi za Idara ya Mahakama kutoa Wajumbe wawili wakati afisi yenyewe ya Mkurugenzi inatoa Mjumbe mmoja tu?

Mhe. Spika, kifungu cha 26 kinarekebisha sheria ya nyendo za Jinai namba 7 ya 2007 kwa kufutwa vifungu cha 96, 98 na 101. Mhe. Spika,kifungu hiki kina mkanganyiko mkubwa. Kwanza kifungu cha 98 cha sheria iliotajwa ni kifungu kinachofuta sheria ya nyuma ambayo haikufutwa bali ilirekebishwa. Pili, kifungu cha 101 hakimo katika Sheria hii namba 7 ya 2004. Hivyo, kwa mtu wa kawaida kama mimi hawezi kuelewa arejee Sheria ili akione kifungu cha 101.

Mhe. Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ina umri wa miaka saba hivyo bado ni mpya lakini yenye mafanikio makubwa. Afisi hii imezaliwa kutoka Afisi ya Mwanasheria mkuu wa serikali kama ilivyo nchi za Jumuia ya Madola.

Mhe. Spika, Uingereza ndio nchi ilioanzisha Afisi ya aina hii tokea 1880, lakini ilikuwa ikishughulikia makosa machache ya jinai mpaka 1986 ndipo Afisi ya *DPP* ndipo ilipopewa uwezo wa kushughulikia makosa yote ya jinai.

Mhe. Spika, Australia walianzisha Afisi ya *DPP* mwaka 1983, Canada 2006 na Afrika Kusini miaka ya hivi karibuni tu. Hivyo, kumbe Zanzibar haikua nyuma kwa kila kitu kwa hili tumewatangulia wengi.

Mhe. Spika, sina pingamizi na sheria hii na natamka rasmi naunga mkono hoja.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo katika wachangiaji, lakini kwanza naomba radhi kutokana na sauti yangu kidogo itakuwa ya mashaka mashaka. Kabla ya hayo Mhe. Spika, naomba nitoe shukurani zangu za dhati.

Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia sote tuliokuwa hapa kuwa hai katika mwaka huu mpya wa Kiislamu na mwaka mpya wa Kizungu.

Mhe. Spika, vile vile, kwa niaba ya wenzangu naomba niwakaribishe Mhe. Juma Duni Haji na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui katika kambi yetu nawaomba na nawatakia kheri na wao watajumuika na sisi katika kusukuma mbele gurudumu hili la taifa. Naomba niwakumbushe kwamba wao wako katika kambi ya upinzani na upinzani sio kwamba kila kitu unapinga, lakini upinzani ni kukosoa serikali, kuielekeza na pale ambapo ni sahihi basi pia tunakubaliana na serikali. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba niende katika mswada wenyewe.

Mhe. Spika, mswada wa Afisi hii ni mzuri na kwa kweli Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni Afisi muhimu ambayo ni lazima ipewe meno na mswada huu unajaribu kwa kiasi kikubwa kutoa meno hayo. Lakini naomba nichangie kidogo kwa mambo ambayo nahisi yangeweza kurekebishwa ili meno hayo yawe makali zaidi.

Nikianza katika ukurasa wa 208 wanasema kwamba:

> *"Office means the Office of the Director of Public Prosecutions established under section of this Act*"

Mimi nafikiri hapa tuna-*establish Office of the Director of Public Prosecutions* lakini vile vile imesha-*establish Office of Director under section 56 (a)* nafikiri. Kwa hivyo, nafikiri tuiache hivi hivi kwamba *Office of Director of Public Prosecutions* ni kama ile ambayo imetamkwa katika Katiba na hii itakuwa haina maana tena, au itakuwa ni *duplication* ambazo hazina maana.

Mhe. Spika, la pili katika ukurasa huo huo wanasema:*"State Attorney" means qualified lawyer employed by the government and assigned to work in the*

Office. Hapa ningeomba nipatiwe maelezo tukishakutafsiri hili kwamba *state attorney is qualified lawyer employed by the government and assigned to work in the office* maana yake wale *state attorney* wengine wote ambao wamekuwa *employed by the government* lakini hawakuwa *assigned* kufanya kazi katika afisi hii watakuwa sio *state attorney* kwa mujibu wa *definition* hii. Mimi nafikiri kuna makosa kwa sababu *states attorney* wengine hawaingii katika afisi hii lakini wako katika maofisi mengine nao ni *state attorney*, lakini ukishasema kwamba *state attorney is qualified lawyer employed by the government and assigned to work in the office*. Kwa hivyo, unazi-*exclude* afisi nyengine zote nafikiri hii pia nayo inataka marekebisho.

Mhe. Spika, naomba tuende katika kifungu cha 4(2) ambacho kinasema kwamba: *"The office shall be an independent and autonomous government agency in the Zanzibar public service".* Mhe. Spika, hii nina wasi wasi vile vile kwa sababu hii afisi tunataka iwe afisi ambayo inajifanyia shughuli zake bila ya kuingiliwa na chombo chochote. Unaposema kwamba *government* itakuwa ni *autonomous government agency* ina maana ni *agent* wa serikali na ukishakusema kwamba ni *agent* wa serikali ina maana kwamba serikali ndio bwana, huyu ni *agent* wake na kwa mujibu wa sheria za *agency* ni kwamba *agent* lazima achukue amri za bwana wake.

Kwa hivyo, ukishakusema kwamba hii ni *independent* lakini halafu ukasema kwamba ni *agency it means* unaihalalisha kwamba idara hii pia ichukue amri za serikali, wakati hiyo pia inapingana na kifungu cha 56(a) (7) cha Katiba ambacho kinasema. Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki Mkurugenzi wa Mashtaka hatalazimika kufuata amri na maagizo ya mtu mwengine yeyote au idara yoyote ya serikali. Kwa hivyo, hiyo ni *contradiction* kwa sababu hapa patakuwa hapana ile *autonomous* wala hakutakuwa na *independence* madhali umeshasema kwamba ni *agency* ya serikali. Kwa hivyo, mimi nafikiri hili neno agency liondoke na tufuate hivi ilivyoelekeza, nafikiri ni sawa sawa.

Mhe. Spika, naomba tuende katika ukurasa wa 211 kifungu cha 8(3c) wanasema kwamba fedha za afisi zitapatikana katika mambo matatu kifungu hicho kinasema kwamba:

> *"Money accrued or earned by the office from publications, trainings, consultancies and other activities conducted by the office through its training centre"*

Mimi suala langu je, *Director of Public Prosecution* na afisi yake watataka kufanya kazi za *consultancies* na *consultancies*, hizi mtu yeyote tu anaweza kwenda kufanya na *it means* wakifanya *consultancies* kwa sababu hapa kuna

faini lazima ulipe. Kwa hivyo, sasa *department* hii ya *public prosecution* tunaifanyia mambo mawili. Kwanza inakuwa ni *prosecutors* lakini halafu wanakuwa ni *consultants* wa watu kwa sababu hapa imeelezwa tu. Kwa hivyo, hata mimi naweza nikenda nikataka ushauri, nikawalipa na wakafanya. Je, hiyo kweli ndio azma na kazi ambayo tunaitaka kwa *public prosecution.*

Mhe. Spika, nikiendelea nakuja katika kifungu cha 11 kinasema kwamba: *State Attorney or Public Prosecution* ambazo *function* zao wamepewa au wanafanya kazi za *director* au zimekuwa *deligeted* na *constitution* kwa sababu ni *public prosecutors*. Kwa hivyo, *State Attorney* kwa mujibu wa utaratibu ni *public prosecutors* labda nielimishwe je, kutokana na sheria hii *States Attorney* wengine si *public prosecutors* tena. Kule Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuna *state attorney* ambao nao kwa mujibu wa taratibu na sheria ni *public prosecutors,* lakini hapa inaonesha kama kwamba hawa hawatokuwa *public prosecutors*. Hapa nilikuwa nataka nipate ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, pia katika kifungu cha 11 (3) wanasema kwamba director anaweza akamteua *advocate* wa Mahakama Kuu au mtu mwengine yeyote awe wa nje au wa ndani awe ni *public prosecutors*. Hii inatendeka ni sawa lakini mimi nafikiri hapa wanapofanya hivi kuwe *on payment surtain fees.* Kwa mfano wamekuja watu kutoka nje wa kesi fulani kwa hivyo tusim-*point* tu kwamba anaweza kwenda Mahakamani, lakini alipe *fees* ambayo itasaidia kuendesha shughuli zetu katika nchi. Hivyo ndivyo wanavyofanya katika nchi nyengine. Kwa hivyo, mimi naomba kuwe *on payment of fees* ambazo tutaziweka.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 13 naomba pia nipate ufafanuzi kwa sababu hapa pana mgongano baina ya *director of prosecutors* na polisi. Polisi wana sheria yao nafikiri ni 322 sasa hiyo 322 ya polisi nayo imewaruhusu polisi kuwa *prosecutors* na wao wanafuata amri za Makamanda wao. Sasa hawa polisi kwa mujibu wa sheria hii watafuata amri za nani sasa, Makamishna wa Polisi au wasaidizi wao au watafuata amri za *director* wa *public prosecutors*. Hii nahisi tutakuwa na mgongano katika utendaji wa kazi.

Mhe. Spika, tukienda katika kifungu cha 16 mimi nahisi kuna matatizo kwa sababu kinasema kwamba *director of public prosecutor* pale anapohisi kwamba kuna ushahidi kutokana na mtu fulani na ushahidi ule utasaidia kuendesha kesi fulani. Kwa hivyo, huyo mtu mwenye ushahidi huo wanaweza wakamfutia mashtaka ili waweze kuendesha kesi ya yule mtu mwengine. Mimi naomba nielezwe hapa.Je, hatuvunji ile *principle* ya sheria ya jinai kwamba wasaidizi na wale wanaofanya wote wako katika chungu kimoja. Kwa sababu ikiwa mimi nina ushahidi wa kitu fulani ambacho kimefanywa na mimi kama sijatoa ripoti. Kwa hivyo, mimi nitakuwa ni msaidizi. Kwa mujibu wa sheria ni kwamba msaidizi ana haki ya kushtakiwa, lakini sasa unataka kumuondoa shahidi huyu

kwa sababu tu akupe ule ushahidi zaidi. Je, hatuoni kwamba hiyo ni kuwafanya wengine waondokane na makosa ambayo wanafanya kwa kutaka mtu mmoja tu ili kumkamata. Nafikiri pengine inaweza ikawa ni tatizo.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 17 anasema kwamba *director* wa *public prosecutor* katika shughuli zake atatoa *regular briefing* kwa waziri anayehusika. Ninavyofahamu mimi ni kwamba unapotoa *regular briefing* waziri atakuwa na jukumu la ku-*direct* kwamba hiki kifanyeni hiki msikifanye au hiki kitekelezwe njia hii. Anapoingia waziri hapo hii *institution* itakuwa ni *independent* au itakuwa inachukua maelezo ya waziri. Kwa hivyo, pendekezo langu ni kwamba *briefing* hizi kwa *institution* kama hizi hazendi kwa waziri lakini *briefing* hizi zinakuwa *submitted* katika Bunge la nchi ile kwa kupata taarifa na Bunge linaweza likajadili na kutoa maelekezo.

Kwa hivyo, hapo ndio kile kitu kitakuwa ni independent kwamba hakiingiliwi na executive organ yoyote ile. Kwa hivyo, hapa mimi nafikiri ripoti za *director of public prosecutor* basi ni vyema zikawa Baraza la Wawakilishi ili kupata taarifa na wao kuelezea katika masuala haya.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 19 kuna suala la *code of conduct*, hapa tumeambiwa kwamba *director* atatekeleza wajibu wake kwa mambo yote yaliyoelezwa pale. Lakini huku kuna *director* na *depute director*. Sasa huyu *depute director* yeye hakuambiwa kwamba ajiheshimu au a-*behave*, au aende kwa mujibu wa utaratibu ule. Mimi nafikiri hii ni kasoro.Kwa hivyo, hapa pawe pana *director* na *depute director* kwa sababu hawa ndio wakubwa wa ofisi hii. Kwa hivyo, na yeye awe ni mtu ambaye anawajibika.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 22(c) cha Kiswahili kinasema' "bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu hiki Afisi ya Mkurugenzi hasa watafanyakazi wote au yoyote kati ya hayo yafuatayo katika kuendeleza madhumuni yaliyotajwa chini ya kifungu cha kwanza". Sasa kuna (a), (b) na (c) wanasema kuandaa mkutano au mkusanyiko wa aina yoyote ile.

Mimi najiuliza *is it proper* kwamba kuandaa mkutano au mkusanyiko wa aina yoyote ile? Mimi nafikiri tungekuwa *specific* ni mikutano gani au mkusanyiko wa aina gani ambao wanaruhusiwa? Lakini tukisema wanaandaa mkutano au mkusanyiko wa aina yoyote ile wanaweza wakenda mbele zaidi kuandaa mikutano kwa sababu tutakuwa hatukuwafunga, mkutano wa aina yoyote ile wanaweza wakaandaa, hata wa *CUF* na CCM wanaweza wakaandaa. Sasa mimi nasema lazima tuwe *specific* kwamba wao tunawapa kitu gani cha kuandaa na mikutano hiyo itakuwa kwa madhumuni gani.

Halafu katika kifungu cha 22(g) ndio lile lile suala langu la *consultancy, provide consultancy or research services to any institution, way the government or non governmental*. Kwa hivyo, *consultancy* hii itakwenda mpaka kwa serikali. Kwa serikali *is no problem,* lakini kwa *non-governmental organization,* kwa nini wawe wana *provide consultancy,* si kuna wanasheria ambao wana-*provide consultancy* kwa nini wao wana-*act* kama ni *private advocate* ambayo itakuwa sio kazi yao. Sasa hiyo nafikiri ina matatizo kidogo.

Kifungu cha 23 pale ni *composition* na *consultative committee*, wanasema kuna *Judge of the High Court* ambaye atakuwa *recommended by the Chief justice* na atakuwa *appointed* na *minister who shall be the chairman*. Halafu *director of public prosecution*.

Mimi Mhe. Spika, hii siikubali kwa sababu kwanza *director of public prosecution* ni mtu mkubwa kuliko jaji na pengine huyu jaji aliyechaguliwa na *chief justice* anaweza akawa ni *junior judge*. Kwa mujibu wa *profession* ya wanasheria ninavyofahamu ni kwamba inakwenda kama kijeshi, yule mkubwa ndiye anayepewa heshima zaidi ambaye ana muda wa kufanya kazi siku nyingi, ni mkubwa wa cheo, sasa ukimuweka *director of the public prosecution* ni Mjumbe tu katika kamati inayokuwa *headed* na *junior officer*, Jaji wa Mahakama ambaye *is not junior in search* lakini katika mantiki hii ambaye pengine atakuwa ndio kwanza kateuliwa kuwa jaji halafu akaja hapa akawa ni mwenyekiti.

Mimi nafikiri hii itakuwa sivyo, bora huyu *director of public prosecution* awe ni *chairman* na hao wengine wawe ni Wajumbe. Lakini pia hapa kuna *register of high court*, ikiwa kuna *presence* ya Jaji wa Mahakama Kuu, kuna haja gani ya kuwepo *register of the high court*, kwa nini? Kwa sababu hii ni *institution* ambayo wanatakiwa waendeleze shughuli fulani, kwa nini hatumuongezi msaidizi wa *DPP*, mtu yeyote aliyeko pale kama ni *prosecutor*, yaani ofisi ya *DPP* wakatoa Wajumbe wawili na huku Mahakamani kukatoka Mjumbe mmoja.

Mhe. Spika, kifungu cha 24 kinasema mtu yeyote *who is appointed* kama ni *public prosecutor* imekuwa *suspended*, halafu akajiingiza katika mambo hayo ya *prosecution* basi atakuwa ni mkosa na akipatikana anaweza akawa *fined not less than one million shillings*, lakini hakueleza *maximum* yake ni kiasi gani. Kwa hivyo, huyu anaweza hata akatozwa shilingi bilioni moja kwa sababu hakuna *limit*. Sasa utaratibu wa kisheria hauandikwi hivyo, ama ni *not less than one million*, lakini *not more than two millions*. Kwa hivyo, itakuwa umeshamfunga, lakini ukiweka tu *not less than one million* halafu ukaweka huku mbele kokote anaweza akapewa adhabu yoyote ile. Kwa hivyo, naomba hiyo irekebishwe.

Mhe. Spika, kifungu cha 26 nacho pia nina wasi wasi nacho kwamba *Criminal Procedure Act* imekuwa *amended* kwa ku-*repeal section* 96-98. Kweli *section* 101 ipo katika *Act* hii? Sina uhakika sana. Naomba itizamwe na irekebishwe.

Mhe. Spika, kama nilivyokwambia hali yangu kidogo sio nzuri naomba nimalizie hapa. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Tunashukuru sana Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa mchango wako huo, sijui kama hali ingekuwa nzuri ingekuwaje. (*Kicheko*)

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu na kuchangia mswada huu wa Sheria ya Kuweka Masharti au Uanzishaji na Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, awali ya yote nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kuhakikisha kwamba umefika wakati hivi sasa wa kuweka chombo hiki muhimu kwa ajili ya wananchi wetu juu ya kuendesha wa kesi na kupata haki zao kwa kila njia inayostahiki. Tegemeo langu kubwa mswada huu tukiupitisha na *Inshaallah* tutaupitisha basi utaleta manufaa makubwa sana kwa wananchi wetu hasa chombo hiki kitapopewa uhuru wa kufanya kazi zake bila ya kuingiliwa.

Mhe. Spika, Mkurugenzi wa Mashtaka ni mtu mwenye dhamana kubwa au ni mtendaji mwenye dhamana kubwa katika shughuli mbali mbali za kutafuta haki za watu. Majukumu haya yanataka utaratibu na umakini ili kila mtu anayepelekwa pale au anayekwenda katika mambo yake ya kudai yapatikane bila ya matatizo. Mhe. Spika, mswada huu umeeleza mambo mengi mazuri na moja wapo ambalo nimelipenda katika nafsi yangu ni uadilifu.

Mhe. Spika, Uadilifu ni jambo la mwanzo katika dhamana hii na kama utakuwa si muwadilifu katika dhamana hii basi mgogoro utakuwa nao wewe na watu wenye kudai haki mbali mbali kwa ajili ya kufanyiwa kinyume na mwelekeo wa vile watu wanavyotaka. Naamini kwenye mashtaka tegemeo la wengi wanapopeleka kesi zao au malalamiko hutaka wafanikiwe bila ya kuangalia sheria kwa baadhi ya wengine. Lakini sio pahala tu pa kusema nakwenda kupeleka malalamiko haya lazima nifanikiwe, bali Mwendesha Mashtaka ataangalia hali halisi ya haki na wajibu unavyotakiwa ili mhusika aondoke pale kapata haki yake kwa manufaa yaliyopo pande zote mbili, upande wa kwanza unawezekana na upande wa pili inakuwa haiwezekani.

Mhe. Spika, migogoro tunaamini imo mingi lakini na mimi nasema tu kwamba, kwa muda huu tunakoelekea, tunakotoka kwa muda mrefu tulikuwa na polisi tu peke yao wanaoshughulikia mambo haya ya kuendesha mashtaka katika Mahakama mbali mbali. Lakini bahati nzuri sasa hivi Afisi yetu hii ilivyoanzia na tunavyoipa sheria nzuri zaidi, basi Mkurugenzi wa Mashtaka akisaidiana na Naibu wake ikiwa atateuliwa na Mhe. Rais, lakini kwa kuwa na yeye atakuwa na uwezo wa kuteuwa watendaji wake ambao watafaa katika kanda mbali mbali, basi naamini harakati za maendeleo zitaendelea vizuri na wananchi wetu wataweka matumaini kwamba kesi zinaendeshwa kwa utaratibu unaofaa na haraka ili mahitaji na haki zipatikane.

Mimi si mwanasheria, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu kwa vipindi vyangu nilivyokuwepo hapa nimepitisha sheria nyingi. Kwa hivyo, uzoefu niliyokuwanao naamini kuna mambo mengi yaliyoelekezwa humu yana vitu ambavyo lazima vitimizwe ili wajibu mzuri upatikane.

Ukurasa wa 149 Sehemu ya Pili, Uanzishaji na Uendeshaji wa Afisi. Nambari 4(1) imeeleza wazi wazi kwamba inaanzishwa Afisi itayojulikana kama Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Spika, Afisi hii ndio itayokuwa muhimili wa kazi zote na shughuli zote za Mkurugenzi pamoja na watendaji wake. Naamini kwamba hapa ndipo penye harakati za mambo yote ya mipango na mengineyo ambayo yatasaidia kuleta ufanisi wa kazi hata katika vitengo vitavyopangwa katika sehemu mbali mbali. Pia, tegemeo langu kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka na watendaji wake ataowaweka katika kanda zake watakuwa na vikao vya mara kwa mara kukutana hapa juu ya kupanga mikakati ya kuharakisha matakwa ya wananchi. Matakwa hayo ni kuhakikisha kwamba kesi zinaendeshwa haraka na zinatafutiwa ufumbuzi wa haraka ili kuleta manufaa kwa ajili ya watu wao.

Lakini Mhe. Spika, pia nambari mbili naomba ninukuu kwamba “Afisi itakuwa taasisi huru yenye mamlaka ya kujiendesha ndani ya utumishi wa umma Zanzibar” hili ndilo nililolisemea mwanzo Mheshimiwa. Mwenzetu huyu na watendaji wake wakipewa uhuru wa kufanya kazi na uhuru wa mamlaka waliyokuwanayo basi kazi zitaendelea vizuri na zitafanyika kwa ufanisi zaidi.

Mimi ombi langu kwa Mhe. Waziri kwamba sheria hii ili ipate manufaa na uhuru wa kufanya kazi zake. Taasisi kama ilivyokuwa huru ijitegemee na iendelee na shughuli zake katika kuharakisha na kuendeleza kesi hapa kwetu. Ukienda Tanzania Bara tatizo hili lilikuwa kubwa sana, walifika watuhumiwa kugoma wakasema hatwendi huko kwenye Mahakama kwa sababu tunarundikiwa kesi ambazo hatuzijui mwisho wake lini, lakini kwa hapa Zanzibar niseme kwamba afadhali tunashukuru, lakini tuwape nguvu wenzetu

hawa na Mkurugenzi apate uhuru wa kufanya kazi zake na watendaji wake ili afanye kazi zake kwa utaratibu unaofaa.

Mhe. Spika, Mkurugenzi huyu ambaye atateuliwa na Rais yeye atateuliwa kwa mujibu wa katiba kama ilivyosemwa hapa, lakini pia suala ambalo zuri na yeye anategemewa kupata Naibu Mkurugenzi kama atavyoona Rais inafaa. Hilo si suala baya ni zuri, isipokuwa ushauri wangu ningemuomba Mhe. Waziri kwa wakati tuliokuwanao pamoja na juhudi ya Mkurugenzi ambaye atakuwa anaandamwa na kazi nyingi bado Mhe. Rais amshauri ni vyema kabisa Naibu Mkurugenzi akateuliwa kama sheria yetu hii inavyosema.

Sababu ya msingi ya kusema hivyo Mkurugenzi ni binadamu anaweza kutokezewa na dharura basi huyo Naibu ataendesha shughuli zilizokuwepo kwa manufaa ya nchi yetu na wale wanaokwenda pale na matatizo yao.

Mhe. Spika, hili namuomba sana Mhe. Waziri aliangalie, tuna matatizo mengi katika maeneo yetu, katika sehemu zetu za kazi masuala kama haya yapo yanajitokeza na yanaathiri utendaji wa kazi katika sehemu hizo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa ni huyo aliyeteuliwa na Rais lakini pia Rais ana uwezo kama inavyosema sheria hii kwamba amtafute mtu atakayefaa kutokana na mambo yaliyotajwa ndani ya sheria hii. Mtu wenyewe awe na shahada ya sheria, uzoefu usiopungua miaka miwili na ni mtu muadilifu. Haya mambo matatu yote ni sahihi na yanafaa kuangaliwa ili tupate faida hiyo.

Suala jengine nitalolizungumza Mkurugenzi katika sheria hii kapewa mambo mengi ambayo atayafanya lakini katika kufanya kwake hatofanya peke yake atakuwa anashauriana na watendaji wake ambao ataona wanafaa katika kuendesha shughuli mbali mbali za kila siku. Mimi ningeomba Mhe. Spika, katika sehemu ya nne uajibikaji na uwazi.

Mhe. Spika, sheria hii imesema wazi kwamba, Mkurugenzi atachukua hatua na kubuni njia muwafaka kufanya maamuzi yake juu ya mashtaka yawe ya uwazi ili kuendeleza imani ya raia juu ya matumizi ya mamlaka ya kushtaki na hasa atafanya yafuatayo:-

Nafikiri kifungu hiki peke yake ndio yale niliyotanguliza kusema kwamba uadilifu ni kitu muhimu na ni mzuri kuwa uwazi. Kwa hivyo, uwazi ni sehemu moja wapo ya kuhakikisha kwamba mdai anapata haki yake anajua na mdaiwa anapata haki yake anaijua, vyenginevyo Mhe. Spika, italeta mgogoro.

Pia, katika mswada huu nimesema kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa anatoa taarifa mara kwa mara kwa Mhe. Waziri anayehusika. Hili ni suala zuri

na sahihi hasa tukizingatia kwamba kuna mambo ambayo yanakuwa yanataka msaada kusaidiwa. Kwa hivyo, akitoka kwenda kwa Mhe. Waziri watatafuta njia ya kufaa ili kuhakikisha uwezekano mzuri unapatikana na taarifa anazozipeleka zinamsaidia kutokana na kupata maelekezo ambayo yatakwenda sambamba.

Naamini Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa na maamuzi lakini pia naamini kuna baadhi yamengine itabidi washauriane na Mhe. Waziri kutokana na sheria hii inavyoeleza.

Sote tunaamini kuwa taarifa ni jambo muhimu sana. Hivi sasa tunachukulia katika nchi yetu hii, tuna matatizo makubwa sana yaliyojitokeza ya kitaifa kuhusu suala la umeme. Suala zuri ninaloipongeza serikali na wizara husika kutoa taarifa bila ya kuogopa, mwananchi au hata mtoto wako nyumbani ukimwambia ukweli leo umekosa kula kutokana na moja, mbili, tatu atakufahamu, lakini ukisema naogopa kusema kwa kupata shutuma nyengine, ni vibaya sana, bora useme mtu akufahamu ili lile alilolipanga mbele ajue aa kumbe kumetokea hili basi itakuwa hivi.

Mimi nafikiri hili ni zuri na uwajibikaji kama huo ndio utawala bora katika nchi. Mhe. Spika, bila ya uwajibikaji wa uwazi hakuna la manufaa katika nchi na uwajibikaji na uwazi ni suala moja wapo ambalo linaleta ukweli na ufasaha kwa mtu yeyote kwa mwenye kudai na kudaiwa. Kwa hivyo, sheria hii naipongeza sana kama ilivyoelezea juu ya suala hilo lililoonekana kwamba pana haja ya kukaa na kuangalia kila kinachofaa wakaleta ushauri mzuri kwa vyombo vinavyohusika.

Mhe. Spika, mimi kwa upande wangu huu mswada umekuja wakati mzuri na wakati tulionao hivi ni wa harakati mbali mbali ambapo harakati moja wapo hivi sasa tukiangalia katika vyuo vyetu vya Mafunzo hasa hapo Makao Makuu Kilimani, utakuta vijana wengi wapo pale wanalalamika wamewekwa muda mrefu na nini. Lakini bado nasema chombo chetu hiki mimi nakiunga mkono kiendeshe kazi zake vizuri na Mkurugenzi asaidiane na wataalamu wake ili kuhakikisha utendaji unakwenda vizuri na kila mwenye kupata haki yake aipate kwa wajibu na haraka ili matatizo haya yasitokee.

Mhe. Spika, mimi kama nilivyotangulia mwanzo kuwa sauti yangu si mbaya kama Mhe. Abubakar Khamis Bakary alivyosema yake yeye, lakini kwa kuwa mimi si mwanasheria niseme tu kwamba mswada huu ulioletwa hapa mbele yako ya Uanzishaji na Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na mambo yanayohusiana na hayo, naunga mkono kwa asilimia mia moja na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wote waupitie na wauangalie ili

kuhakikisha kwamba tunamuwelekeza ndugu yetu ambaye tunataka kumpa majukumu mazito yeye na watendaji wake, hasa tukizingatia haki kuwa ni suala moja wapo la kila muhitaji.

Mhe. Spika, kuna haki sehemu mbili, unaweza kudai haki hujui haki, lakini unaweza kukosa haki kwa kutojua haki vile vile. Kwa hivyo, mwenzetu huyu yeye atakuwa ni mtaalamu na mwalimu kwa mwenye kupeleka malalamiko yake moja, mbili, tatu nimeonewa akasaidiwa maarifa ili kuipata hiyo haki anayoitafuta.

Baada ya hayo machache natamka rasmi mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani naunga mkono kwa asilimia mia moja mswada huu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru nami kunipa nafasi kuchangia kidogo katika mswada huu ambao tunaujadili hivi sasa kuhusu Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kuwapongeza wawakilishi wenzetu wawili ambao wameungana nasi kipindi hiki kwa kuchaguliwa na Mhe. Rais kuja kuungana nasi katika Baraza hili kwa kuwakilisha wananchi wetu na kuendeleza mambo ambayo yanahusiana na maendeleo ya nchi yetu. Nawapongeza sana.

Jambo jengine Mhe. Spika, kabla sijachangia nitangulize kusema kama alivyosema Mhe. Ali Suleiman Ali kwamba, mimi pia si mwanasheria wala si *bush lawyer* na wala si kama Mhe. Ali sina uzoefu wa miaka 10 ambayo mwenzangu amekuwanayo katika kupitisha sheria mbali mbali.

Nasema haya kwa masikitiko makubwa Mhe. Spika, naisikitikia sana ofisi yako kwa upande mmoja. Kwa sababu mswada huu ni wa kitaalamu sana. Mara nyingi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunavyoingia ndani ya Baraza hili, kila mtu tumeingia hapa. Katiba inasema ukijua kusoma na kuandika Kiswahili. Mhe. Spika, nimekuwa nikilisema hili mara kwa mara ili tufahamike uwezo wetu sisi wawakilishi, basi wewe unaweza kuchaguliwa na wananchi kuja kuwakilisha.

Lakini hiyo haimaanishi kwamba wewe sasa usisaidiwe katika kutekeleza majukumu yako. Ndio maana Mhe. Spika, tunakuwa tunaliomba Baraza la Wawakilishi lakini zaidi wakisaidiana na serikali ambao ndio wanaoleta miswada hii watusaidie katika kuifahamu miswada kwa maana ya kutufanyia semina kabla ya kuleta miswada hasa miswada migumu kama hii ambayo ni ya

kitaalamu, ofisi yake haijulikani bado ni mpya, tunaona maneno wewe mwenyewe unajiuliza hili maana yake nini, kwani mashtaka ndio huwa nini.

Kwa sababu Mhe. Spika, mambo yanayohusiana na mashtaka sio kila mwananchi yanamkumba au anaelea ndani yake, ni mambo ambayo ya kitaalamu sana na tungepaswa kupatiwa semina kabla ya kuja kujadili mswada huu.

Mhe. Spika, nayasema haya kwa sababu chombo cha Baraza la Wawakilishi ndicho chombo pekee chenye nguvu cha kuwakilisha mawazo ya wananchi. Sasa inapokuwa sisi hatukupewa taaluma au kuelimishwa zaidi juu ya mswada hushindwa kuwatendea haki wananchi wetu. Kwa hivyo, naomba sana ofisi yako Mhe. Spika, iwezeshwe, Waziri wa Fedha yupo hapa kufanyiwa semina kila inapobidi kwa miswada ambayo itahitaji.

Najuwa wenzetu waliyoko kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala labda wao ni wazoefu wameogelea zaidi mswada huu, lakini sisi wengine kwa kweli Mhe. Spika, tunausoma kama tunasoma tu, halafu labda uone kitu ambacho hujakifahamu tena ndio ujaribu kuuliza na kusema hapa na pale, lakini hayo ni masikitiko yangu na natarajia afisi yako itayazingatia.

Baada ya hayo Mhe. Spika, na mimi nianze kwa kuzungumzia kipengele kinachozungumza juu ya kuwepo kwa Afisi hii na uhuru wake. Imeelezwa hapa kwamba kutakuweko na Afisi hii ambayo itakuwa ni taasisi huru na yenye mamlaka ya kujiendesha ndani ya Utumishi wa Umma wa Zanzibar. Nafurahi kwamba angalau itakuwa na uwezo wa kuajiri wafanyakazi wake pale ambapo Mkurugenzi ataona inafaa, lakini pia kuweza kuwatoa.

Nimeyasoma hayo nimeyaona katika sheria, kuweza kumuondoa au kumfukuza katika Afisi yake mtu yeyote ambaye anajaribu kupotosha au kuharibu masuala mazima ya uendeshaji wa Afisi yake au uendeshaji wa masuala ya uendeshaji wa mashtaka. Hilo nalishukuru sana.

Lakini kama alivyoeleza kiongozi wangu bado nina wasi wasi vile vile juu ya uhuru wa chombo hiki. Ningependa tutafakari sana kwamba chombo hiki basi kisiwe ni wakala wa serikali badala yake kiwe chombo ambacho kina uhuru kabisa kabisa kijisikie huru katika utendaji wa shughuli zake.

Mhe. Spika, nikiendelea na kuangalia yale ambayo nimeyaona katika mswada huu, ningependa sasa niende kwenye kifungu cha 8(1) kinachoelezea juu ya fedha na bajeti ya Afisi. Mhe. Spika, kila tukizungumzia masuala ya fedha pale pale pia tunazungumza uwezeshwaji wa Afisi hii kwamba ipatiwe fedha za kutosha. Tumesoma katika kabrasha hili au mswada huu kwamba majukumu ya

Afisi hii ni mengi mno, ni mengi mpaka mimi naweza kusema hee, huyu jamaa atakuwa na kichwa gani? Kwa sababu kila pahala yeye anahusika, ana shughuli nyingi za kuzifanya lakini hizi shughuli hazitakwenda bila ya kuwezeshwa.

Kwa hivyo, ombi langu kwamba sawa, Afisi itaandaa bajeti yake lakini ombi langu ni kwamba, ili sheria hii iweze kutekelezeka na Afisi iweze kufanya shughuli zake, basi niwaombe sana wenzetu wa Wizara ya Fedha waitizame kwa jicho la rehma. Kwa sababu kazi inazofanya Afisi hii kwa kupitia sheria hii ni muhimu mno, ni kazi ambayo inaisaidia muhimili muhimu wa Mahakama katika utendaji wa shughuli zake kuona kwamba haki inatendeka. Haki inasisitizwa popote pale, kila mwananchi wa nchi hii angependa kuona kwamba anapatiwa haki yake. Kwa hivyo, bila ya kuipatia fedha za kutosha utekelezaji wa sheria hii kama ulivyo na Afisi hii utakuwa mgumu sana.

Lakini jengine katika hili ni muhimu katika kifungu cha 8(1) tumeambiwa kwamba mlipaji mkuu wa serikali yeye atawapangia wafanyakazi ambao wanahusika na kada hiyo, wafanyakazi wa fedha katika kitengo hiki. Ninachotaka kusema ni kwamba kuna kitengo kimoja cha fedha ambacho mara nyingi katika vyombo kama hivi vikipangiwa watendaji wa eneo lile anasahaulika naye ni Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu. Huyu ni mtu muhimu sana na katika mashughuli mengi ya hesabu kama patafanyika makosefu basi ni kwa sababu Mkaguzi huyu wa ndani hayupo.

Hapa nasisitiza tu ili wanaohusika wajue kuwa huyu naye ni mtu muhimu ndani ya kada. Najua wanajua hivyo, lakini kutokana na upungufu labda wa watu hawa mara nyingi huona si lazima anaweza akatoka mmoja wizarani, huyo huyo ndio akenda akafanya ukaguzi. Kwa kweli hiki ni chombo kikubwa hivyo tunataka Mkaguzi na yeye awepo pale pale sio yule wa kuazimwa kutoka sehemu moja kwenda nyengine.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 9(2)(b), nimesoma hapa kwamba, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 56(a)(7)(8) cha Katiba, na kwa kuzingatia sera ya uendeshaji wa mashtaka iliyokubalika na Afisi ataamua kushtaki au kutokushtaki kuhusiana na kosa lolote.

Katika hili Mhe. Spika, mimi niko *concerned* zaidi na hii sera ya uendeshaji wa mashtaka. Afisi ni mpya na kwa kadri ya muda wangu niliyokaa hapa ndani ya Baraza sikumbuki kwamba tuliletewa sera inayohusiana na uendeshaji wa mashtaka. Kama nilivyosema kwa sababu hatukupatiwa semina hatujui kwamba hii sera ipo au haipo. Sasa ombi langu ni kwamba, tutakapokuja kuelezwa tuelezwe hii sera ipo au haipo? Kama haipo basi umuhimu wa kutengenezwa hii sera uonekane mara moja kwa sababu ni kipengele muhimu sana katika utendaji wa sheria hii.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 19 (1) naomba univumilie nifike kwenye hicho kifungu na ninayo pia ile ya Kiengereza nilitaka tu hapa nisaidiwe ndio ule ufahamu tena tunasema ufahamu mdogo na ikiwa si mwana sheria mambo yanakuwa magumu, lakini mimi nimeona kama sisi wanasiasa tumekuwa *offended* katika lugha iliyotumika hapa.

Kifungu cha 19 (1) kinasema:

> "Mkurugenzi atafuata mwenendo ambao ni wa kujiheshimu kwa hali ya juu na hasa hatokuwa mwanachama wa chama chochote cha siasa au mwanachama wa jumuiya yoyote ambayo ni sehemu ya chama cha siasa"

Sasa nikawa najiuliza hivi sisi tuliokuwa wanachama wa vyama hatujiheshimu, sijui Mhe. Spika, kama hili neno liko sawa na nilipoangalia ndani ya mswada huu kwenye mswada wa Kiengereza liko neno zuri na linafahamika hasa linasema hivi:

> *"The director shall conduct himself in a manner which observe highest degree of integrity, and in particular"*

Je, hii ni tafsiri ya hii maana yake Mhe. Spika, hapa nilipoliona hilo neno nemeshituka kweli kumbe nikasema kumbe kuwa mwanasiasa ni kutojiheshimu.

Ningeomba sana kama kuna neno jengine tutalipata zuri, mimi sijalifikiria na labda ndio pia limewapa tabu ambao wanafanya hii *translation*. Lakini vyenginevyo unavyoisoma Mkurugenzi atafuata mwenendo ambao ni wa kujiheshimu kwa hali ya juu na hasa 1 hatakuwa mwanachama wa chama chochote cha siasa. Nataka nifahamike uzuri mimi sipingi haya yalioainishwa na naya-*suport* kabisa kabisa kwamba yule awe mtu wa hali ya juu.

Mhe. Spika, tatizo langu ni kwenye lugha iliyotumika hapo kwamba awe ni mwenye kijiheshumu. Lakini katika kujiheshimu huko hiki kimoja asiwe nacho, ala kumbe ukiwa na hiki wewe huwa hujiheshimu. Mimi hapa katika hili ningependa sana nije nisaidiwe lugha imenipa tabu na nimeona kama imetu- *offend* sana sisi wana siasa.

Mhe. Spika, lakini katika 19(2) kuna kipengelee ambacho kinazungumzia tuhuma za kuvunja kanuni za maadili dhidi ya Mkurugenzi, naomba ninukuu hicho kifungu:-

> “Tuhuma za kuvunja maadili dhidi ya Mkurugenzi zitawasilishwa rasmi kwa Rais ambaye baada ya kutafakari tuhuma zenyewe anaweza kuamua kaunzisha uchunguzi rasmi au kutoanzisha uchunguzi katika hali yoyote hakuna uchunguzi utakaoanzishwa bila ya Mkurugenzi kupewa fursa za kufahamu tuhuma dhidi yake na kupata fursa ya kupata maelezo yake juu ya tuhuma hizo”

Nimekuwa najiuliza hivi sisi hapa Zanzibar tunacho chombo kinachoshughulikia maadili ya viongozi na katika hili najiuliza hivi nani atakaeweza kwenda kueleza hizo tuhuma kwa Rais nani atakuwa nahaki hiyo. Rais ni mtu mkubwa na si kila mtu anafika kwa Rais. Lakini nilifikiri kuna chombo ambacho ndicho kinachoangalia maadili ya utendaji wa viongozi wetu wakiowemo Wakurugenzi, Mawaziri na mambo kama hayo, na hicho chombo basi kinapogundua Mkurugenzi amevunja maadili labda sasa amekuwa hajiheshimu tena amejihusisha na siasa sasa amevunja maadili haya.

Kama kavunja maadili mimi tu kwa kumuona naweza kwenda kumripoti kwa Rais hapa inakuwaje ningeomba nisaidiwe katika ufananuzi wa kifungu hiki, kuna chombo ambacho kinaangalia maadili au wenzetu labda hawa wanasheria na watu wanaohusika nakada hii wanachombo chao wao kinachoangalia utendaji wa shughuli zao kwa sababu Mhe. Spika, napata tabu na kuona kwamba kada hii inahusika na kutoa haki kwa wananchi inalalamikiwa sana kwa mambo ya rushwa.

Mhe. Spika, sizungumzii Mkurugenzi wa Mashtaka lakini nazungumzia shughuli za kutoa kama mtu amefanya kosa na sasa amepewa hukumu hatufanya tafiti na mimi binafsi sina tafiti kwamba kuna rushwa imeenea sana hapo kwa majaji. Lakini na wao ni watu ambao wanafanyakazi kwa maadili, lakini sasa nani basi mwenye haki ya kwenda kuwaripoti, hapa sizungumzii majaji lakini mtu kama huyu ambaye atakuwa ameondoka kwenye maadili ya utendaji wa kazi zake ningeomba hapa atakapokuja Waziri atuelezee kidogo katika suala hili.

Mhe. Spika, jengine liko kwenye kifungu cha 22 (1) na huu ni msisitizo ambao nimezungumzia kwanza kabisa kwamba Afisi itakuwa kituo kikuu cha kitaalamu cha kiserikali katika kuendeleza sera sheria mipango ujuzi na uelewa wa raia katika nyanja zote za usimamizi wa sheria za jinai na Mkurugenzi ataomba fedha na ufundi na kuweza kuutumia katika kutekeleza jukumu hili. Yeye ataomba tu lakini muhimu ni kule kupatiwa kuwezeshwa.Ninachosisitiza hapa tuyaone majukumu ambayo tunamtwika mwenzetu huyu kwa sheria hii na wanaohusika na kuweka *ceiling* waone kwamba majukumu haya kwa kubana mno *ceiling* ya taasisi hii basi itakuwa vigumu sana kuweza kutekelezeka.

Jengine katika kifungu cha 22(2d) kushiriki katika mikutano au mikusanyiko iliyoandaliwa na taasisi nyenginezo. Kwanza huku tulishasema kwamba awe na maadili asijihusishe na siasa na mambo kama hayo. Je, tukimuona DPP amehudhuria mkutano wa chama kwa sababu hapa kushiriki katika mikutano au mikusanyiko iliyoandaliwa na taasisi nyenginezo ziko nyingi za kidini za kisiasa na mambo kama hayo, kidogo hii haitakuwa na uwazi wa kumsema lakini kipengele fulani cha sheria kimeniruhusu kimenambia nisiwe mwanachama tu lakini kumbe naweza kuhudhuria mikutano na mambo kama hayo. Kidogo hii labda ingepaswa kuekwa vizuri zaidi ili isilete utata.

Mhe. Spika, kama nilivyoanza kusema mwanzo si mengi ya kuchangia lakini napenda pia nichukuwe nafasi hii kuipongeza Ofisi hii na Mkurugenzi wake na watendaji wote kwa kutimia kwao miaka 7 karibuni nilipita njiani nikaona mabango ya wanaadhimisha siku yao. Na Kwa kweli miaka 7 kwa watoto wetu ni kama mtoto ananza shule ni *Primary school* . Lakini yanayofanywa na taasisi hii ni kama wako sekondari. Kwa kweli wapo sekeondari wanaelekea kwenda *University* na mambo kama hayo.

Mhe. Spika, kwa muda mfupi sana wanayoyafanya ni mambo ya kupigiwa mfano na kwa maana hiyo na kwa minajili nilivyoufahamu huu mswada naomba tu nichukuwe nafasi hii kukubaliana nao na naomba tuendelee kuujadili. (*Makofi*).

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii kutoa mchango wangu mdogo kuhusiana na mswada huu wa uanzishwaji wa Afisi ya Muendesha Mashtaka Mkuu.

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima tukaweza kuzungumza. Mhe. Spika, mimi si mwana sheria na napenda niungane mkono na mwezangu tulitegemea miswada kama hii ambayo ni mizito ingetanguliwa pengine ikiwa sisemi, basi hata maelezo mazuri yakina kidogo ya kufafanua, ni kwa nini sasa hivi tunahitaji kupata uanzishwaji wa kitengo kama hiki.

Pili, mimi nitajikita zaidi katika mambo niliyoyaona ya uendeshaji wa hii Ofisi yenyewe tokea kuanzishwa kwake na namna gani inavyokwenda. Mhe. Spika, nikianza labda nije kifungu cha kwanza namba 4 ambacho ningemtaja huko kwamba Mkurugenzi atatajwa kwa mujibu wa Katiba. Lakini huyu Naibu Mkurugenzi Mhe. Spika, Zanzibar imekubwa na matatizo mengi ya kiuendeshaji katika maofisi. Moja katika sababu ni kutokujali haki za wafanyakazi. Sasa teuzi kama hizi mimi nina wasi wasi nazo, mimi nilitegemea kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka anateuliwa na Rais kwa mujibu wa Katiba, sasa yeye ndie atakaekuwa na mamlaka ya kumteuwa Naibu Mkurugenzi

kutokana na Ofisi yake aliyonayo, hii ingetoa nafasi zaidi kwa kifungu cha 5 cha mswada huu wakati Mkurugenzi anapoambiwa, naomba ninukuu kifungu cha 5 (1) kinasema:-

> "Mkurugenzi atakuwa na dhamana ya utendaji wenye ufanisi katika Afisi na kwa kufikia hilo anaweza baada ya kushauriana na Idara yenye dhamana ya utumishi serikalini kuweka muundo unaofaa wa Afisi kwa kuunda vitengo kama anavyoona inafaa. Sasa kwa sababu hii Ofisi tayari ilikuwepo na sasa tunaipitisha kisheria. Kwa hivyo, nafasi hii ya Naibu Mkurugenzi nilifikiria zaidi mimi angepewa Mkurugenzi kuteuwa kutokana na dhamana hii na pia kutokana na uendeshaji mzuri wa kiofisi kwamba huyu Naibu Mkurugenzi akawajibika moja kwa moja kwa Mkurugenzi alivyokuwa anajua kwamba yeye ndie aliemteuwa tena kutokana na sifa ambazo alizozichuma pale ofisini"

Lakini utaratibu wa kuteuwa viongozi wawili mkuu na msaidizi wake kwa kupitia Rais, zina hatari ya huyu Naibu kujiona kwamba yeye nae kateuliwa na Rais.Kwa hivyo, ana nafasi sawa na yule wa juu yake. Na kwa hivyo pale pale mwanzo kukaanza mgongano kwa sababu wataalamu wanasema watu wawili hata kama wamesoma sawa sawa au wamefanyakazi sawa sawa lakini mawazo yao yatatafautiana kidogo. Sasa kutafautiana kwa mawazo haya kunaweza kukaleta migongano ambayo siyo ya lazima.

Sasa tukiondoa kifungu hiki tukampa uwezo sasa Mkurugenzi kuteuwa Naibu wake kutaondoa migongano hii na kutaleta ule utaratibu wa kiofisi. Mhe. Spika, imetokea si mara moja wala mbili kwamba nafasi hasa hizi za ukurugenzi au kamishna hawa wanaoitwa amekaimu mtu kwa muda wa mwaka moja mpaka miwili, lakini ilipokuja nafasi sasa ya kupewa anaondolewa yeye analetwa mtu mwengine kabisa wakati yeye amefanya kazi ile kwa ufanisi, sasa mimi nina wasi wasi huo mmoja.

Lakini wa pili ni kwamba hii Ofisi tayari imeshajijenga sasa kwa sababu nafasi ya Naibu amepewa tena Rais kuchangua anaweza akatoka nje na pengine mtu ambae ni mpya kabisa katika ile nafasi, yote mawili inawezekana. Kwa sababu hiyo Mkurgenzi lazima amkubali kwa sababu ameteuliwa na Rais. Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Waziri aliangalie tena upya hili nafasi ya Naibu Mkurugenzi kwa sababu hii Ofisi ipo na sasa hivi tuna eka utaratibu wa kisheria wa kuwa iweze kuendeshwa katika utaratibu huo hilo la pili Mhe. Spika.

Tatu vile katika uendeshaji wa Ofisi kifungu hiki cha 6, pia mimi naomba kupata ufafanuzi. Naomba nikinukuu:

> “Uajiri wa wafanyakazi wa Afisi walio wataalamu na wa kawaida utafanywa kwa kufuata kanuni za utumishi serikalini, isipokuwa kwamba katika hali yoyote taratibu za uajiri zitaandaliwa ambazo zitahakikisha kupatikana kwa wafanyakazi wazuri kwa ajili ya afisi”

Mhe. Spika, sasa hapa pana maelezo mengi mazuri, lakini hakuhusishwa mtu wala taasisi imesemwa tu kwa kufuatwa utumishi, lakini haikusemwa kwamba Idara ya Utumishi ndio itakayohusika au mwenyewe Ofisi ya Mkurugenzi ndio itakayohusika. Kwa hivyo, dhamana imetupwa katika ile mantiki tu ya wale wafanyakazi kwamba wataajiriwa kwa nini lakini hakutupiwa Ofisi maalum au mtu maalum sasa imeachwa inaning’inia hii. Lazima ingeekewa na mtu basi au taasisi kwamba uajiri utafanywa na taasisi gani pamoja na kwamba itafata utaratibu wote lakini taasisi gani ambayo itakuwa na uwezo wa kutoa hizi ajira.

Mhe. Spika, baada ya kutoa mambo hayo ya kuiuendeshaji ambayo niliyaona na baadae ni moja kwa moja katika sehemu hii ya pili ya mchango wangu kuhusu kuondoa migongano. Mimi nilihisi kwamba kwa sababu sheria hii inahusiana na mambo ya mashtaka na itahusiana na moja kwa moja na mambo ya Mahakama na vile vile mambo ambayo yatashughulikiwa na polisi kama ilivyo katika kifungu namba 9(c). Kifungu hiki kinasema kuelekezwa polisi na taasisi nyengine ya upelelezi wa makosa ya jinai kuchunguza taarifa yoyote na kutoa taarifa kwake haraka iwekezekanavyo.

Sasa kama ilivyotajwa na Mhe. Waziri Kivuli kwamba sisi tunapitisha sheria lakini kuna taasisi kama hizi ni za kimuungano na wenzetu katika nchi nyengine suala la polisi hata haliko katika suala la kinchi, ni suala la mamlaka ya miji. Mhe. Spika, katika nchi za wenzetu polisi ni sehemu tu ya ile manispaliti na wanaongozwa na Manispaa. Lakini sisi hapa polisi ni masuala ya Muungano na hili ni suala la Zanzibar.

Kwa hivyo, tuangalie toka mapema ni vifungu gani ambavyo vitaleta mgongano katika masuala haya na tuweze kuvipeleka katika lile kapu letu kuu la kero za Muungano, mapema iwezekanavyo kabla hatujatoa amri kwa polisi ikashindwa kutelekezwa, na ikiwa kapu kuu litashindwa basi Baraza nafikiri limeshaanza vizuri liletwe Barazani na tuombe litolewe kwenye *list* ya Muungano. Kwa sababu kama nilivyosema kwamba si jambo la ajabu polisi ni watu wanaolinda usalama tu hawahusiani na mambo ya nchi nzima katika nchi nyingi.

Kwa hivyo, hilo si jambo la ajabu kusema kwamba sasa polisi tuwaombe kwa sababu ya utendaji mzuri na kwa sababu ilivyofikia ili tuzuie kwamba wakati polisi wanasheria na huku Mkurugenzi wa Mashtaka anaunda utaratibu wake

na lazima haki ipatikane ili kusije kutokea migongano tuangalie na mapema *points* hizo ili tuweze kutatua na mapema.

Mhe. Spika, kifungu namba 10 tunaanzisha hii Ofisi, lakini kinachonishangaza hapa katika kifungu hiki kwa sababu wako wenzengu waliochangia. Mimi kinanishanganza kitu kimoja kwamba hii Ofisi ina Mkurugenzi na kwa mujibu wa Ofisi hii ina Naibu Mkurugenzi. Lakini hapa kaambiwa kwamba Mkurugenzi anaweza kwa taarifa itakayochapishwa na wanasheria wa serikali.

Sasa mimi nikasema wakati mwengine ikiwa hukusoma ile sheria inashangaza baadhi ya mambo mengine kwa sababu yeye ana msaidizi wake na *procedure* zote anazokwenda nazo yule msaidizi anatakiwa azielewe azijue, ni kwa nini atoke akamkabidhi mtu mwengine madaraka yale wakati ndani ya Ofisi yake kuna Naibu wake. Sasa hapa kidogo naomba ufafanuzi, kwa nini ikafikia hivyo kwa sababu nilisema kwamba hiki chambo mwanasheria wa serikali hayumo humu kwenye chombo, yuko wenye Ofisi ya serikali. Sasa kwa nini yeye mamlaka yake amkabidhi mwanasheria wa serikali asimkabidhi Naibu wake kwa maandishi.

Mhe. Spika, tukija katika kifungu namba 19 hizi tuhuma za kuvunja kanuni za maadili zaidi ya Mkurugenzi. Huyu Mkurugenzi kwa mujibu wa katiba Rais alipokwisha mteuwa alikuwa anatekeleza shughuli za kiserikali, tukubali basi tuhuma zende kwa Waziri au ziende kwa Waziri Kiongozi, kwa sababu watu hawa ndio wanaofatilia shughuli za kiserikali na Rais kazi yake ilikuwa ni kumteuwa na ikiwa Rais ataridhika kwamba hawezi tena kufanya kazi yake ni kufanya utaratibu akapatikana mtu mwengine. Lakini moja kwa moja tuhuma zile akafikishiwa Rais itabidi Rais yule yule azirudie ampe kazi mtu mwengine.

Lakini huyu anafanyakazi ya serikali tukubaliane kwamba ama tuhuma zile apewa Waziri na ikiwa cheo kile ni kikubwa basi apewa Waziri Kiongozi, ndie mwenye kushughulikia shughuli za serikali. Sasa Waziri Kiongozi atakavyoridhika kwamba sasa ni kesi ya kumpelekea Rais, laa ni mambo ambayo siya msingi wala nini atayabakisha huku huku. Lakini naona mimi kulichukuwa moja kwa moja ukalipeleka itakuwa hujamfanyia haki kwa sababu itakuwa imeingizwa wasi wasi wa Rais wakati haujathibiti.

Kwa mujibu wa taratibu, nahisi mimi ni kwamba unakuwa wewe huna kosa mpaka utakapothibiti kuwa una kosa na mtu akipelekwa Mahakamani anajulikana kwamba hana kosa mpaka ushahidi utakapothibiti kwamba ana kosa. Kwa hivyo, tuhuma kupelekwa kwa Rais ni sawa kumfanya ana kosa na wala hajathibitika kwamba ana kosa. Kwa hivyo, mimi sihisi kwamba utaratibu huu ni sahihi. Naomba Mhe. Waziri uje utufafanulie ni kwa nini akapelekewa kwa Mhe. Rais moja kwa moja.

Mhe. Spika, nikija katika kifungu namba 23, mimi kwanza itabidi nielimishwe ni kazi ya kamati, ni nini Kamati ya Mashauriano, kwa sababu kama kamati hii ilikuwa ijadili hali inavyokwenda nahisi kuwaweka mbele wale wanaoendesha pia nayo haikuwa sahihi. Kwa sababu wanaoendesha shughuli hizi ni Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakama ndio zinazoendesha shughuli hizi za kesi. Kwa hivyo, watu wawili hawa kuwaweka mbele katika hizi shughuli za mashauriano, pia si sahihi kwa sababu wao watakuwa wanajijengea ile hifadhi yao. Mtu pekee ambae angestahiki kuwa Mwenyekiti ni wakili wa kujitegemea ambae anaheshimika.

Lakini ukimpeleka mtu wa Mahakama atakwenda ku- *defend* Ofisi yake. Lakini hili ni suala la mashauriano kwamba haya ni mambo yetu yanakwenda uzuri katika hali inayotakiwa. Kwa hivyo, kuwa na mtu *independent* asiehusika na vyombo vya sheria na mwenye uwezo ndie angepaswa ku- *share* kikao hiki cha mashauriano. Mhe. Spika, nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Naomba kumpongeza Mhe. Waziri kwa jitihada kubwa alioifanya kuleta mswada huu ambao katika kipindi kizuri ambacho kwa lengo la kuweka Utawala Bora.

Mhe. Spika, kabla sijaingia kwenye mswada nitakuwa nautangulizi mdogo katika mswada huu. Mhe. Spika, Utawala Bora ni sehemu kubwa na imekuja Utawala Bora kwa lengo la kuweka mambo yawe sawa katika nchi kama zilivyo nchi nyengine duniani. Na sisi tunaipongeza serikali yetu kwa kuleta hili. Lakini katika kazi iliyofanywa mimi kwa mawazo yangu ningedokoa kidogo tu na suala la Utawala Bora ni refu na tumezungumza kitu cha Mahakama na inanza katika njia refu.

Mahakama kwanza lazima atokee muhalifu apitie njia ya polisi papite upelelezi na kama ana kosa apelekwe Chuo cha Mafunzo ni mambo manne kwa matano yanayoongozana. Lakini ukitizama mambo haya matatu bado hayajafikia kwenye kiwanngo kama hili lililofanywa leo kuletewa sheria hapa ili kurekebishwa liende uzuri.

Mfano kwanza serikali ilikuwa na jukumu kupitia wizara hii kutoa taaluma kwa wananchi iliyo safi ili yapunguke makosa ya aina mbali mbali kwa jamii hiyo ilikuwa ni kazi moja ya msingi ifanywe ili wananchi waelewe kwamba ukiiba kuku wa mtu ni kosa, ukimpiga mtu kibao bila ya ridhaa ni kosa. Sasa yako makosa madogo madogo yanafanya kwa kutokuelewa tu, sasa ni jukumu la wizara pia na huko kuangalia kwa kutoa taarifa mbali mbali kwa magazeti pengine na vipeperushi ama TV au redio kuelimisha jamii nini kosa ambalo linaweza kumtia hatiani.

Lakini pili akeshakamatwa sasa ni jukumu la wizara kutoa taarifa mbali mbali kwa magazeti na vipeperushi au TV ama redo kuelimisha jamii nini kosa ambalo anaweza kumtia hatiani.

Lakini akeshakamatwa kwenda kituo cha polisi na polisi nae aangalie upelelezi na kuandika *statement*. Utakuta bado na hilo halijawekewa mkazo, kesi nyingi zinababaishwa Polisi. Za haki zinaachwa zilizokuwa si za haki zinasonga mbele. Sasa na hili pia ni tatizo tunaiomba wizara ichukue jitihada ya kushiriki katika kuangalia njia gani za kufanya ili na Polisi nao wakapata taaluma ya kuweza kuyasimamia haya mambo kwenda vizuri mpaka yakafikia pale tunapopataka.

Lakini ikishakwenda Mahakamani pia utakuta bado Mahakama zetu ni finyu. Mahakama ya Wilaya utakuta kesi zikiwa tatu, basi wote kwanza wasubiri nje aende mmoja mpaka imalizike ndio aingie mwengine, utakuta bado tuko katika karne za mbali sana. Kwa hivyo, bado Mahakama zetu hazijafikia kiwango kile ambacho kinatakiwa, bado finyu, vifaa vya kizamani, majaji wachache. Sasa hili pia liongozana katika kutengeneza la mbele ili na huku nyuma nako kukae sawa. Hii itakuwa sawa sawa na kuvaa kanzu nzuri, koti lakini unatembea miguu chini, inakuwa ile kanzu hukuithamini.

Sasa upande wa Mahakama bado marekebisho yapo kimajengo, kivifaa na kitaaluma. Naomba na hili wizara kama tuna nia hiyo ya utawala bora basi na Mahakama ziimarishwe ili lilingane na haya huku tunakokwenda.

Mhe. Spika, la mwisho katika hili ameshafungwa mtu kaenda Chuo cha Mafunzo lakini bado mpaka leo watu wanatumia ndoo, anayewahi ndio anayekwenda kumwaga. Hivi sasa wenzetu wamepiga hatua kubwa unakwenda Mahakamani mtu anatoka na degree na kaenda kwenye kujifunza. Sasa ile kujifunza italeta maana ya Utawala Bora, lakini hapa kwetu kila akaenda mtu Chuo cha Mafunzo anarudi kuwa asi zaidi na mengine anafanyia huko huko ndani. Utakuta tumechota kitu kimoja tunakiimarisha lakini vyengine vitakuwa bado katika hali si nzuri. Mhe. Spika, wizara ina nia nzuri hili moja imeliona lakini haya mengine yaendelezwe ili tufikie lengo lililokusudiwa la Utawala Bora.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo nije kwenye mswada ukurasa wa 149 ambao wenzangu wamechangia lakini na mimi nina haki ya kutoa mawazo yangu juu ya suala hili. Sehemu ya Pili inasema “Uanzishaji na Uendeshaji wa Afisi”. Hapa tumeambiwa inaanzishwa rasmi kisheria Afisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka. Nakubali kwamba Afisi hiyo ipo na hivi sasa inakaribia

tena mwaka wa saba. Amepewa majukumu mbali mbali ya kuweza kuyasimamia katika utekelezaji.

Kwa hivyo, katika ukurasa huo huo kifungu cha 5 (1) hapa chini tunaambiwa "Muundo wa Afisi" naomba ninukuu:

> "Mkurugenzi atakuwa na dhamana ya utendaji wenye ufanisi katika Afisi". Hili halina tatizo.

Lakini kifungu cha 5 (2) kinasema:

> "Mkurugenzi atateua wakuu wa vitengo kwa masharti atakayoona yanafaa na kwa kuzingatia muundo wa utumishi wa afisi"

Kifungu cha 6 (1) kinasema:

> "Uajiri wa wafanyakazi wa afisi, walio wataalam na wa kawaida, utafanywa kwa kufuata Kanuni za Utumishi Serikalini, isipokuwa kwamba katika hali yoyote, taratibu za uajiri zitaandaliwa ambazo zitahakikisha kupatikana wafanyakazi wazuri kwa ajili ya Afisi"

Mhe. Spika, nadhani Mkurugenzi amekuwa na kazi nyingi sana, nadhani nyengine yeye angependekeza tu wakafanya watu wengine. Ushauri wangu kwamba katika suala la ajira kwa kuwa iko taasisi ya kuajiri basi yeye angependekeza tu kwanza akatangaza kwamba mimi hivi sasa nataka mtu mwenye *degree* ya pili ya fani ya sheria, *degree* ya kwanza fani ya utawala, halafu kule kunakohusika wakatangaza zile tenda ili wale wanaopatikana akapelekewa.

Lakini tena Mkurugenzi huyo huyo asimamie Afisi, aajiri, naona tunampa majukumu makubwa. Ushauri wangu suala la ajira atangaze, kitengo kinachohusika kiajiri halafu apokee kwa mujibu wa yale maombi aliyoyataka. Nadhani tutampunguzia kazi na ataweza kufanya kazi zake kwa vizuri. Suala hili likizingatiwa nadhani litasaidia katika kuendeleza mswada huu.

Mhe. Spika, nakuja ukurasa wa 150 kifungu cha 7 "Kazi za Afisi". Ziko nyingi lakini mimi nitakuja kwenye (d) nitasoma halafu nitoe ushauri wangu. Naomba ninukuu.

Kifungu (d):

> "Kushajihisha, kudhamini na kuhimiza tafiti, midahalo na mambo mengine kwa madhudmuni ya kuimarisha usimamizi wa sheria ya jinai kwa jumla na hasa usimamizi wa mashtaka"

Sasa katika kazi hizi anasema kwamba atashajihisha, kushajihisha ni kama kuhamasisha watu. Kudhamini ina maana kama pana gharama yeye atalipa. Kama sivyo Mhe. Waziri utakuja kuniweka sawa. Kuhimiza tafiti, kufanya midahalo, yaani atapita maeneo mbali mbali kufanya midahalo ya kutoa taaluma juu ya hizi kesi za jinai. Nadhani si suala baya lakini naona kutakuwa na gharama kubwa juu ya suala hili.

Sasa naomba baadhi ya mambo yangepunguzwa ingebakishwa labda kushajihisha, kuhimiza tafiti, midahalo na mambo mengine. Lakini kudhamini naona kidogo kwa mawazo yangu mimi tungeliondoa litampa matatizo, la kama limekaa vizuri Mhe. Waziri atakuja kunieleza nikifahamu mimi sina matatizo.

Lakini kazi nyengine inafuatia hapa kifungu (e) inasema "Kutoa mafunzo katika nyanja zozote za sheria za umma na hasa sheria za usimamizi wa jinai"

Hatukatai kama ni taaluma yake hiyo kutoa mafunzo lakini mafunzo hayo atayatolea wapi, ana chuo, atafanya semina au makongamano na kwa taasisi zipi. Namuomba Mhe. Waziri anipatie ufafanuzi juu ya suala hili.

Mhe. Spika, niendelee na ukurasa huo huo "Fedha na Bajeti ya Afisi" kifungu cha 3 (a) na 3 (b), naomba ninukuu.

Kifungu cha 3 (a):

> "Fedha za Afisi zitajumuisha: fedha zinazopitishwa na Baraza la Wawakilishi katika kila mwaka wa fedha kwa matumizi ya Afisi"

Hizi hazina tatizo zinapitia wizarani zinafanyiwa bajeti na sisi tunaidhinisha kutumia.

Lakini kifungu cha 3 (b) anasema "Misaada, michango ya fedha nyengine zitakazopelekwa na Afisi kutoka vyanzo vyengine vinavyokubalika. Mimi nadhani Mhe. Spika, kwa kazi hii na umuhimu wake zingewekwa fedha zinazotosha katika bajeti kwa sababu huku kwengine ni kutega na kutega ni kubahatisha. Ningeomba wakapatiwa fedha za kutosha kupita kwenye bajeti na

haya mengine yakawa mengineyo, akipatikana mfadhili, kuuza magazeti, kuuza vijarida, hiyo iwe kama nyongeza.

Lakini fedha zitafutwe za kutosha zitiwe kwenye bajeti tupitishe hapa ili Afisi iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kuliko kutegemea tena mikopo, kuomba itakuwa lile lengo halikufika. Kwa sababu kuomba nako kuna matatizo yake, pengine anayetaka kukupa ana masharti yake, mkibishana kidogo tu na yeye anaweka ngumu. Sasa naomba kama kitu tunacho cha uhakika tufanye makisio kiwizara ije hapa tupitishe ili tuweze kutekeleza jukumu lililokusudiwa.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu ambao si mkubwa sana maana si mwanasheria nataka ufafanuzi kidogo tu, nije ukurasa wa 153 kifungu cha 3

> "Kukasimu kazi ya Uendeshaji Mamlaka" anasema "Mkurugenzi anaweza kufuta amri ya kukasimu mamlaka aliyotoa kwa taasisi yoyote kwa sababu atakazohisi zinafaa kufanya hivyo"

Mhe. Spika, mimi hapa kidogo nilikuwa na utata nataka nipate maelezo zaidi. Kwa mfano Mkurugenzi katoa jukumu kwa mtu afanye kazi fulani, baada ya kuifanya pengine karudi hakuridhika.Kwa hivyo, anafuta yale waliyokwisha kufanya. Mimi nadhani kimtazamo wangu na mawazo yangu huku ni kujitaza wenyewe, kama unampa mtu jukumu afanye halafu urudi ufute tutakuwa tunafanya kazi ambayo haieleweki.

Ningeliomba kama kuna maana nyengine zaidi niliyoisema mimi naomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho basi anifahamishe ili niweze kuelewa na niweze kuukubali mswada. Hapa nina mashaka hayo tu kwamba nimepewa jukumu kwa niaba yake lakini baadaye yale niliyofanya mimi anakuja anayafuta. Kama nimefahamu sivyo naomba maelekezo zaidi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije ukurasa wa 154 sehemu ya nne "Uwajibikaji wa Uwazi". Hapa imeelezwa kwenye kifungu cha 17 kwamba kutakuwa na uwajibikaji wa uwazi. Kifungu 17 (b) kinasema:

> "atatoa taarifa kwa umma juu ya mambo yanayohusiana na uendeshaji wa mashtaka"

Sasa utoaji huu hapa haikueleza kwa sababu sentensi imekuwa kama haikufikia mwisho. Taarifa hizo atazitoa kutumia TV, redio ama chombo gani. Nadhani ingewekwa wazi akasema tu atatumia redio, TV ama magazeti katika utoaji huu wa taarifa, mtu yeyote akisoma itakuwa haiwezi kumshughulisha, akiangalia kwa haraka anaweza akatambua kipi kimekusudiwa katika mswada huu.

Mhe. Spika, nadhani kwa kuwa si mtaalam wa sheria na mimi nilikuwa na nia nitoe mchango wangu kidogo katika mswada huu. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini naukubali mswada huu baada ya kupata maelezo ya Mhe. Waziri. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia machache katika mswada huu muhimu sana. Mhe. Spika, kama alivyoanza Mhe. Ali Abdalla Ali, kwa kweli na mimi nakubaliana naye kwamba uendeshaji wa mashtaka ni jambo muhimu sana katika ujenzi wa Utawala Bora. Bahati nzuri au mbaya uendeshaji wa mashtaka haujitegemei wenyewe peke yake, unaweza kuwa na waendeshaji mashtaka wazuri sana katika nchi, lakini kuna mambo mengine sasa yakawa yanakwaza *efficiency* ya Ofisi ile.

Sasa Mhe. Spika, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa jitihada zake za kuiimarisha Ofisi hii. Pia, niwapongeza watendaji wa Ofisi yenyewe kwa kweli wanafanya kazi kubwa.

Mhe. Spika, bahati nzuri mimi nikiwa nina muda ni msikilizaji mzuri wa kesi Mahakamani, sio lazima mimi nimeshtakiwa lakini huenda tu kule Mahakamani kuangalia uendeshaji wa kesi hata kama hazinihusu. Sasa kupitia hiyo, nimeona kuna mambo ambayo Mhe. Waziri angeyasimamia ili kuisaidia nchi kidogo. Mimi naona tuna matatizo katika nyanja tatu zifuatazo:

Kwanza kama alivyosema Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, kwamba hatuna sera ya taifa ya usimamizi wa Sheria ya Jinai, hii ni kasoro yetu kubwa. Tunatunga sheria hivi sasa lakini tumezoea kwamba kwanza tupitishe sera halafu ndio tunatunga sheria. Sasa bahati mbaya tumekuja mbele kabla ya sera yenyewe.
Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri pamoja na kwamba ziko sheria ambazo zimepitishwa kabla ya sera lakini hili ni jambo muhimu kwamba tuwe na sera ya taifa ya usimamizi wa Sheria za Jinai.

Lakini la pili unapokwenda Mahakamani utaona tuna tatizo moja kubwa katika nchi yetu na hili lazima tulitafutie ufumbuzi. Washtakiwa wengi ni wale ambao wako katika nguvu kazi. Sasa unapokwenda unamuona mtu ambaye angeweza kufanya kazi ya kuisaidia nchi lakini kila siku yuko Mahakamani, hili ni tatizo. Ikiwa ndio *trend* ya Mahakama zote vile kwamba vijana kuanzia miaka 20 hadi 35 wao ndio wanaokwenda Mahakamani kila siku na kurudi, hawafanyi kazi nyengine za kuisaidia nchi, hili ni tatizo. Mhe. Spika, suala hili lazima Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora iliangalie kwa upana zaidi.

Mhe. Spika, siku hizi kidogo mambo yamerekebishwa, lakini huko nyuma tulikuwa na wale *DPP* wa Polisi unamjua hasa kwamba huyu taaluma yake ndogo, hivi sasa wana taaluma lakini uzoefu mchache. Sasa hili ni tatizo ambalo linatusumbua. Kwa hivyo, pamoja na kwamba tuna vijana wamemaliza *degree* Tunguu na kwengine wameajiriwa katika Ofisi hii ya *DPP* lakini wanahitaji ujuzi na hili ni jambo muhimu sana.

Kwa hivyo, ushauri wangu pamoja na kwamba wameajiriwa watolewe kidogo waende katika nchi ambazo zinashughulika na uendeshaji wa mashtaka angalau kidogo wapate uzoefu, ili wakija huku wawe na kasi ya kuendesha mambo kwa haraka.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ni la ajabu kabisa linachelewesha uendeshaji wa kesi ni Mkemia Mkuu wa Serikali mtihani kidogo. Yaani unakwenda pale kesi inapigwa *date* unafika unaambiwa jibu halijatoka katika Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, unakwenda ukirudi siku chungu nzima. Linapokuja jibu mara unaambiwa bangi ilikuwa majani ya mbaazi, unga ulikuwa unga wa sembe. Sasa hili ni tatizo jengine ambalo linachelewesha, sisi tutafika pahala ama tutamshutumu hakimu, jaji au Mwendesha Mashtaka kama ndio sababu ya ule ucheleweshaji.

Mhe. Spika, mara moja niliwahi kutoa mfano hapa, lakini na leo kwa umuhimu naomba niutoe tena. Mhe. Spika, siku moja nilipata safari ya kwenda Japan, mama watoto nyumbani akaona huyu anakwenda mbali na safari ni safari, sasa wacha nimtayarishie chakula cha njiani au akifika, mtu anajua anakotoka siko anakokwenda. Kwa hivyo, akanitayarishia vile visheti vinavyoliwa matangani au harusini zamani vinavyotiwa shira huku juu kule Pemba, Mhe. Zainab Omar Moh'd anavijua sana.

Kwa hivyo, akanifungia vingi kidogo nikavitia katika mfuko nikaanza Nairobi, nikaenda Bombay, Hong Kong, nikaingia Tokyo na visheti vyangu lakini viko katika ndege. Kufika pale nikaona bao limeandikwa Said Ali Mbarouk *report to custom*, nikasema toba nimeshafanya nini. Basi Mhe. Spika, wakati nalichukua lile bao lililonambia kwamba niripoti *custom* huku nyuma kuna kijana akaniita Said Ali Mbarouk, nikamwambia *yes*, akanambia *come*. Akanambia mzigo wako ule bahati mbaya umesahaulika Hong Kong.Kwa hiyo, tumeuzuia utakuja na ndege nyengine utaufuata hoteli.

Mhe. Spika, nikaondoka pale shingo upande maana yake lile vunge la visheti ndio limo mle na sijui huko ninakokwenda. Nikaenda hoteli niliyofikia nikawapa *address* na kila kitu, baada ya muda mfupi tu wakanipigia simu wakanambia kuna wageni wako mapokezi, kufika ni vijana wawili mmoja

polisi na mmoja wa *custom*, wakanambia mzigo wako umefika hakikisha kama ndio. Nikaupekua nikaona uko sawa nikawaambia nawashukuru.

Sasa kufungua katika lile vunge nikakuta karatasi ambayo haikuwemo imeandikwa Kijapan, nikaichukua ile karatasi nikarudi pale mapokezi wakanambia hii ni karatasi ya *Central Laboratory of Tokyo*, wameuchunguza huu mzigo wakaona hauna madhara, sio *cocaine*.

Kumbe Mhe. Spika, ule mzigo haukupotea isipokuwa wao katika *screen* zao waliona ule unga, wakasema jamaa pengine anaingiza *cocaine*. Kwa hivyo, katika kipindi kile cha saa moja waliuchukua ule mzigo wakaupeleka maabara wakapata majibu wakanirudishia mimi kama niko safi. Mhe. Spika, nilichokuwa nakusudia kusema kwamba tuna tatizo na Mkemia Mkuu wa Serikali na huduma zake za maabara, sisi tunachukua muda mrefu na hili kwa kweli linachelewesha kwa ujumla shughuli za uendeshaji kesi. Sasa Mhe. Spika, hili ni suala muhimu ambalo kama tunataka kuwa *efficient* katika *prosecution* ya kesi za watu wetu lazima tulifanyie kazi.

Mhe. Spika, jengine ni Vyuo vya Mafunzo, mzee wetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwa makusudi aliondosha suala la Magereza kuwa Vyuo vya Mafunzo, lakini lengo bado tuna safari kubwa kufikia hatua hii. Badala ya watu wetu kuwa *reformed* tunawafanya masugu. Sasa hii ni kazi ambayo kama tunataka kuisaidia nchi lazima jambo hili tulishughulikie.

Mhe. Spika, ningemshauri Mhe. Waziri ajielekeze katika mambo manne. La kwanza ni uimarishaji na uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka jambo hili anafanya kazi vizuri na anakwenda vizuri, bila shaka kupitishwa kwa mswada huu utasaidia katika changamoto hii.

Lakini kuna mambo matatu zaidi. La kwanza, kama alivyosema mwenzangu Mhe. Ali Abdalla Ali ni uzuiaji wa makosa. Haina maana tu kukazana katika uendeshaji wa makosa lakini ni vizuri kuzuia makosa.Hii itafanyika kwa maoni yangu kwa mambo mawili. La kwanza jamii kushirikishwa na kuelimishwa. Lakini la pili, doria za polisi na vifaa kama vile gari mitaani, hili ni tatizo. Kuna wakati unapiga simu polisi kama huku kuna wizi unaambiwa hatuna gari.

Suala jengine ni uendeshaji wa kesi Mahakamani. Mhe. Spika, Mahakama zetu zina matatizo mengi. Kama alivyosema mwenzangu nafasi ya vyumba vya Mahakama hivi sasa zimekuwa chache, wakati mwengine tunakwenda pale Mahakamani tunaambiwa kesi iko *chamber*. Sisi tumekuja kusikiliza kesi tunaambiwa iko *chamber*, maana yake ni kwamba vyumba vyengine vyote vimekuwa hamna nafasi. Sasa sisi wasikilizaji ndio basi tunarudi wanakwenda mshtakiwa na mashahidi wake wawili.

Mhe. Spika, kidogo siku hizi hali ni nzuri lakini bado upatikanaji wa Mahakimu na majaji. Kule Pemba huwa tunasubiri Jaji wa Mahakama Kuu muda mrefu na hili ni jambo ambalo pia ni tatizo.

Mhe. Spika, suala jengine upatikanaji wa mashahidi ni tatizo kubwa. Anaweza kuwepo hakimu, *DPP*, mshtakiwa lakini mashahidi hawapo kesi ikawa inapigwa *date*. Kwa hivyo, hili ni jambo ambalo hata kama *efficiency* ya *DPP* ni nzuri lakini kama mashahidi hawakuja kesi ama itakuwa haiendi inacheleweshwa au ina matatizo mengine.

Mhe. Spika, hoja nyengine ni urahisishaji wa taratibu za uwakili, hili jambo pia linatakiwa lifanyiwe kazi. Kuna watu wengine hawajui kujitetea, hawana uwezo wa kutetea.Kwa hivyo, hili ni jambo ambalo linatakiwa liwepo na *public* ijue.

Mhe. Spika, suala la mwisho ni namna ya kurekodi kesi mara faili halionekani limepotea, mara linapatikana.

Mhe. Spika, sasa baada ya maelezo ya jumla, naomba niende katika mswada nina vifungu vichache. Kwanza ni kifungu cha 4 (6) kuhusu Naibu Mkurugenzi atashika nafasi kwa muda wa miaka mitano na baadaye anaweza kuchaguliwa tena. Nilikuwa najiuliza. Je, Naibu Mkurugenzi anaweza baada ya miaka kumi akachaguliwa kuwa Mkurugenzi sasa au ndio atakuwa yeye basi. Naomba kujua hilo.

Mhe. Spika, kifungu cha 6 (2) naomba kunukuu:

> "Kwa madhumuni ya kulinda uhuru wa kikatiba na uadilifu wa Afisi, hakuna mfanyakazi atakayepewa uhamisho kwenda au kutoka katika Afisi, bila ya ridhaa ya Mkurugenzi isipokuwa kama ni kwa uteuzi wa Rais"

Sasa ukiangalia *definition* ya mfanyakazi huku ni pamoja na wahasibu na watu kama hao. Maoni yangu ni kwamba watu wanaofanya kazi katika *account section* hawa wanasimamiwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali na huwa wanapata uhamisho mara kwa mara kulingana na mazingira ya kazi pahala pale au pahala pengine.

Sasa katika wafanyakazi hawa mimi sidhani kama sawa kwamba uhamisho wao uwe kwa ridhaa ya Mkurugenzi. Kwa sababu leo tuna Mkurugenzi mwadilifu, lakini kesho tunaweza kuwa na Mkurugenzi mbadhilifu, yeye akawa anashirikiana na Mhasibu wa Afisi ile kuharibu fedha za serikali.

Kwa hivyo, ikiwa Mhasibu Mkuu wa Serikali awe hana *mandate* ya kumhamisha mpaka kwa ridhaa ya *DPP* ambaye ni mbadhilifu wakati huo kwa kweli hii itakuwa ni tatizo. Mimi ningeshauri kwamba wale wafanyakazi ambao wako katika kada ya Sheria iwe ni sawa, lakini hawa ambao wanatoka katika Uhasibu ni bora tumuachie Mhasibu Mkuu wa Serikali kama ilivyo utaratibu wa serikali aweze kumhamisha kulingana na mazingira tofauti.
Mhe. Spika, suala jengine ambalo naomba kuelimishwa ni kifungu cha 9 (2) (d) kinasema kwamba:

> "kutoa maelekezo juu ya aina ya makosa ambayo mashtaka hayatafunguliwa dhidi ya mtuhumiwa bila ya idhini yake"

Sasa hapo kidogo hii dhidi ya mtuhumiwa bila ya idhini yake imenichanganya, maana yake anakusudia bila ya idhini ya mshtakiwa au bila ya idhini ya *DPP*. Naomba ufafanuzi pamekusudiwa nini.

Mhe. Spika, jengine ambalo naomba nilitolee wasi wasi kidogo ni kifungu cha 12 (3) naomba kunukuu:

> "Sera ya uendeshaji mashtaka na miongozo itakayotolewa italazimika kufuatwa kama utaratibu utaongoza namna mamlaka ya Mwendesha Mashtaka yatakavyotekelezwa na namna ya kusimamia uhusiano baina ya taasisi za upelelezi na Waendesha Mashtaka"

Sasa mwanzoni mwa maelezo yangu nilieleza hatuna sera ambayo tumeipitisha. Lakini kifungu cha 12 (3) kama nilivyokifahamu ni sawa kinaeleza kwamba hivi sasa sera hatuna, lakini baadaye sera itakayotungwa na Mwendesha Mashtaka iweze kufuatwa kama utaratibu utakaoongozwa. Mimi ningeshauri kwamba tusitoe *blank cheque* namna hii, wacha kama kuna sera ije Barazani tuipe baraka, tuirekebishe kidogo halafu baadaye ndio itumike kama ambavyo Mwendesha Mashtaka atafanya maamuzi.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo naomba ufafanuzi ni kifungu cha 16 (1) (a):

> "kuendesha mashauri yanayohusiana na maombi ya kusafirisha washtakiwa wa nchi nyengine waliopo Zanzibar"

Mimi nilikuwa nataka kufahamu hivi Zanzibar tunayo *deportation authority?* Kama ipo naomba kuelimishwa.Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho naomba ufafanuzi ni kifungu cha 26 kuhusu:

"Sheria ya Mwenendo wa Jinai, namba 7 ya 2004 inarekebishwa kwa kufutwa vifungu vya 96, 98 na 101"

Hapa mkononi mwangu ninayo sheria hii ya *Criminal Procedure Amendment Act No. 7* ya 2004. Sasa kifungu cha 96 *"The fourth schedule to the decree is amended as follows. Item 6 is related and replaced as follows.* Sasa hapo kuna vifungu ambavyo katika hii sheria ambayo tunasema vimefutwa, vimefutwa lakini vyenyewe vimekuwa *replaced*. Kwa mfano *office of Tanzania People's Defence Force, National Security Department. Item 8 is deleted and replaced as follows. Private Secretary to the President of Zanzibar.* Halafu item 9 *"All Principal Secretaries. Item 10 is amended by deleting the word legal.*

Sasa katika kifungu hiki tunaambiwa inafutwa. Je, kufutwa kwenyewe hakuna *replacement*, ikiwa hakuna *replacement* kwa nini tunachukua maamuzi ya kukifuta.

Mhe. Spika, halafu kifungu cha 98 nacho kinafutwa. Lakini katika hii sheria mama ambayo ninayo inasema *"Criminal Procedure Decree chapter 14 is here by repelled.* Halafu na humu tunaambiwa nacho kinafutwa. Sasa sijui ni *positive* na *positive* au *negative* na *negative* sijui inakuwaje. Huku tayari kimefutwa lakini 98 tena inafutwa. Sasa sijui mambo ya kisheria naomba muongozo wa Mhe. Waziri.

Huku imekuwa *repelled* halafu na kifungu cha 98 kinakuwa *repelled*, sasa sijui kama hii *repelled* iliyofanywa na sheria hii inafutwa na *repelled* hii au inakuwaje. Isijekuwa tuna *repel* hii tunai-*restate* hiyo iliyokuwepo. Naomba ufafanuzi huo.

Halafu kifungu 101 kinasema kinafutwa lakini humu pia Mhe. Spika, kifungu 101 hakimo.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba mswada huu ni muhimu sana na utekelezaji wake unahitaji mambo mengi ikiwemo bajeti kubwa kwa sababu mzigo waliopewa ni mkubwa. Sasa katika hili mimi ningeshauri kwamba serikali ijitahidi kuona kwamba Afisi hii inawezeshwa kutekeleza majukumu yake, lakini nayo ijitahidi katika baadhi ya mambo ambayo mimi ningeyasisitiza matatu.

La kwanza *exposure* ya vijana wapya hili naomba tena nilisisitize. La pili *scheme of service* ni muhimu kwa sababu vyenginevyo vijana watachukua rushwa. Lakini la tatu ni *promotion* na *grade* kalisema mwenzangu Mhe. Rashid Seif Suleiman kwamba tuna tatizo kubwa Zanzibar. Kwa wenzetu Bara

ukienda pale afisini kwao utakuta huyu ni *Prosecutor Grade I, Prosecutor Grade II, Prosecutor Grade III* na huyu ni *Senior Prosecutor.*

Kwa hivyo, wana utaratibu wa kuwa-*grade* wale vijana kwa mujibu wa uzoefu wao, taaluma yao na *efficiency* yao. Kwetu sisi Zanzibar katika jambo ambalo hilo ni donda ndugu ni utaratibu wa *promotion* katika *scheme* ya *civil service.* Hili ni tatizo ambalo sijui tumejikwaa wapi. Ningeshauri sana Afisi hii ya *DPP* ijifunze kwengine iangalie namna gani inawa-*grade* na inawa-*promote* hawa *Public Prosecutor* ili *efficiency* yao na *promotion* yao iweze kujenga matumaini yao na waweze kutufanyia kazi vizuri. Mhe. Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru kwa kazi nzuri ambayo tunaendelea kuifanya. Sasa naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni ambapo Waheshimiwa Wajumbe wa kwanza kuwasikiliza watakuwa Mhe. Mohamed Ali Salim na atafuatiwa na Mhe. Juma Duni Haji. Tujitahidi tufike wakati huo ili tuendelee na kazi hiyo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11: 00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nashukuru kwamba tumerudi salama kwenye kikao chetu cha jioni, katika kipindi cha asubuhi pale mchana tuliachia kwamba tukiingia jioni tutaanza kumsikiliza Mhe. Moh'd Ali Salim naona yupo, naomba nimkaribishe sana na baadae itakuwa ni zamu ya Mhe. Juma Duni Haji. Karibu Mhe. Moh'd Ali Salim.

Mhe. Moh'd Ali Salim: Mhe. Spika, nakushukuru kwamba toka tuanze mkutano huu, saa za mchana huwa ndio ninayefungua dimba. Kwa hivyo, nadhani nina bahati nao wakati huu.

Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wetu na ambaye anastahiki kushukuriwa kwa kutujaalia wakati huu tukakutana kwa kujadili mambo yenye maslahi kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi sio mwanasheria, lakini pia simo katika kundi la Mhe. Said Ali Mbarouk wanaokwenda wakisikiliza kesi Mahakamani. Kwa hivyo, kutakuwa na mambo mengi ambayo nitahitaji nipatiwe ufafanuzi kwa

kutokujua kwangu mambo haya. Kwa hivyo, naomba nisionekane kuwa niko nyuma sana, naona bora nikiri kabisa kuwa mimi ni mjinga wa habari hii ya sheria hii.

Mhe. Spika, nikianza michango niliyoikusudia katika mswada huu. Kwanza naomba nianze kwa kifungu cha 4, ambacho kinazungumzia kuwa Rais anaweza kuteua Naibu Mkurugenzi kama atakavyoona inafaa.

Mhe. Spika, hapa pamenipa wasi wasi, nadhani wasi wasi huu umekuja kwa kutokuelewa kwangu. Mhe. Rais kama akipenda nilivyofahamu, atachagua Naibu Mkurugenzi, lakini kama hapendi hatochagua Naibu Mkurugenzi. Kwa hivyo, kama ndivyo nilivyofahamu basi nina mashaka kuwa anaweza akatokea Rais akaona kuwa hakuna haja ya kuweka Naibu Mkurugenzi, lakini je, itakapotokea hivyo, hizi kazi alizokwishapangiwa huyu Naibu Mkurugenzi atazifanya nani. Wakati sheria imempangia Naibu Mkurugenzi kazi, sasa kazi hizi ikiwa Rais hakumteua Naibu Mkurugenzi ni nani atakayezifanya kazi hizi.

Kwa sababu katika kifungu hicho hicho cha 5(2) kapewa madaraka Mkurugenzi wa kuteua, yeye hakuambiwa anaweza kuteua, Mkurugenzi kaambiwa atateua. Sasa kuna tafauti baina ya kile kifungu cha 4 na hiki cha 5. Kule anaweza kuteua akipenda, huku atateua, inaonekana katika hii ya Mkurugenzi hiki ni lazima ateue, lakini cha Rais akitaka anaweza hataki basi ni hiyari yake. Kwa hivyo, mimi nilikuwa nafikiria kuwa na hiki cha Mhe. Rais naye labda angeambiwa kwa njia ya busara, kuliko ya kuachiwa uhuru wa kupenda na kutokupenda ya kuwa na yeye ateue Naibu Mkurugenzi. Kwa sababu Naibu Mkurugenzi ana umuhimu wake katika shughuli za Afisi hii.

Mhe. Spika, nikitoka katika kifungu hicho, naomba niingie katika kifungu cha 6(3). Kifungu hiki kinaelekezea kuwa miongoni mwa wafanyakazi wa Afisi hii ni pamoja na wanasheria wa serikali. Sasa kwa mujibu wa uelewa wangu, wanasheria wa serikali wako katika sehemu mbali mbali. Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuna wanasheria wa serikali katika mawizara, kuna wanasheria wa serikali katika mashirika, kuna wanasheria wa serikali. Hapa wanasheria waliokusudiwa wa serikali ambao watakuwa ni miongoni mwa wafanyakazi wa Afisi hii ni wote hao. Au kuna wanasheria wa serikali maalum waliokusudiwa kuwa ni wa Afisi hii ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kwa sababu kwa mujibu wa kifungu cha 6(3), kinasema kwa madhumuni ya sheria kifungu hiki wafanyakazi wa Afisi ni pamoja na wanasheria wa serikali. Sasa wanasheria wa serikali ndio kama hao niliowataja ambao wako katika sehemu mbali mbali, sasa ikiwa na hawa wote wako chini ya Afisi yake yeye, basi naomba hili nijulishwe.

Halafu Mhe. Spika, labda niende mbele zaidi kwenye kifungu cha 8(c) kwenye huduma za ushauri, tumeambiwa moja katika njia ya kupatia mapato Afisi hii ni huduma za ushauri. Kwa vile ninavyoona huduma ya ushauri ilikuwa igaiwe katika sehemu mbili kuu. Kuwe na huduma ya ushauri itakayokuwa bure, kwa sababu wananchi wetu wanaweza wakataka huduma ya ushauri, lakini wakawa hawana uwezo wa kulipa, sasa itakuwa huduma hiyo hawaipati. Kuna makampuni yatakayokwenda kwenye huduma ya ushauri wao watakuwa wanao uwezo wa kulipa. Kwa hivyo, ingebainishwa kuwa kutakuwa na huduma za ushauri za malipo na pia kutakuwa na huduma za ushauri zilizokuwa bure.

Mhe. Spika, hili nalo ni jambo jengine ambalo kwa kutokujua kwangu ningehitaji labda nipate mafahamisho zaidi ili nielewe na niondowe wasi wasi nilionao.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 11(2) kuna suala la kuteua waendesha mashtaka. Suala hili kwa kweli ni muhimu sana, suala hili litapunguza matatizo mengi ikiwa litachukuliwa hatua haraka. Hivi sasa wilayani bado waendesha mashtaka wako wale wale wa zamani. Kwa hivyo, sheria hii kwa sababu inampa madaraka Mkurugenzi kuteua waendesha mashtaka, hapa naomba nitowe ombi kuwa kazi hii naomba ifanywe haraka mara baada ya sheria hii kupita, vyenginevyo bado tutakuwa tuna matatizo yale yale licha ya kuwa tumepitisha sheria nzuri mwanana.

Mhe. Spika, katika kifungu hicho hicho cha 11(3), kuna suala la kumteua Wakili yeyote wa Mahakama Kuu kuwa Mwendesha Mashtaka. Hapa nina swali sijaelewa. Huyu Mwanasheria wa Mahakama Mkuu atakayeteuliwa kuendesha mashtaka atakuwa ni Mwendesha Mashtaka wa muda ule tu atakayeteuliwa pale au tena ndio atahamia katika Afisi hii ya Mwendesha Mashtaka awe ni wa kudumu, kazi yake ni kuendesha mashtaka. Kwa sababu hii inarudia pale pale nyuma, ikiwa waendesha mashtaka wote wa kila Afisi ni wafanyakazi wa Afisi yake hilo litakuwa halina matatizo. Lakini ikiwa ni wanasheria maalum watakaokuwa katika Afisi yake basi hapa ningehitaji kujua, je uteuzi huu utakuwa ni wa muda au utakuwa ni uteuzi wa kudumu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba niende kwenye kifungu cha 11(7), kinasema,

Kifungu cha 11(7):

> "Kila Mwendesha Mashtaka atawajibika kufuata maelekezo atakayopewa na Mkurugenzi na atawajibika kufuata Maadili ya Waendesha Mashtaka"

Hii mara nyingi huwa na-*comment* katika sheria. Kwa sababu ukisema Mwendesha Mashtaka atafuata maelekezo ya Mkurugenzi, basi ina maana lolote atakalomwelekeza Mkurugenzi atatakiwa alifuate. Nadhani lililokusudiwa hapa ni maelekezo yatakayohusiana na kazi yake, nadhani ni vizuri ikabainishwa tusimwachie tu Mkurugenzi kuwa aelekeze anavyotaka yeye vyovyote, haidhuru hivi sasa tuna Mkurugenzi mzuri sana, lakini inaweza ikatokea wakati akatokea Mkurugenzi mwenye ubinafsi kidogo akatoa maelekezo yaliyokuwa hayahusu mambo ya ile kazi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba niingie katika kifungu cha 12(1), kifungu hiki kinamtaka Mkurugenzi aandae sera. Kama walivyozungumza wenzangu itakuwa hapa katangulia kuku kabla ya yai. Hata hivyo pamoja na yote hayo, kwa kuwa tumekosa taaluma ya kutosha ya mswada wenyewe na kwa kuwa shughuli hii ina utaalamu mkubwa, basi kabla sera haijaletwa Barazani, Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Spika, wapate nafasi ya kupewa mafunzo. Maana nikisema semina, pengine Mhe. Waziri wa Fedha ataanza kuingia hofu, lakini wapewe mafunzo Wajumbe, ili waweze kuja kuichangia vizuri sera hiyo kwa sababu watakuwa wanaielewa vizuri baada ya kufundishwa. Vinginevyo kama italetwa tu hapa Barazani sera ya mambo kama haya bila ya mafunzo yoyote, kwa kweli inaweza ikapata mchango mdogo sana na pengine usiwe wa maana sana kama vile ilivyotarajiwa.

Mhe. Spika, nikitoka kwenye sera, naomba sasa nitumbukize mguu katika kifungu cha 15(1). Hapa kuna suala zima la kumuomba Mwendesha Mashtaka, kuombwa Mwendesha Mashtaka na mtu binafsi, yaani mtu binafsi anaweza kwa mujibu wa kifungu hiki akaomba anahitaji kesi yake iendeshwe na Mwendesha Mashtaka gani, kama nimefahamu ndivyo, hivyo ndivyo nilivyofahamu.

Pia, najua kuwa mtu ana haki ya kutia wakili katika kesi. Sasa swali langu liko hapa.Je, mtu ambaye kaomba kuekewa Mwendesha Mashtaka anayemtaka yeye na Mkurugenzi akakubali, atakuwa na haki pia ya kuweka na wakili, iwe Mwendesha Mashtaka wake na wakili wake. Suala hili ningeomba nipewe ufafanuzi nalo kwa sababu sijalifahamu hasa litakuwakuwaje kwa sababu kwangu mimi naliona kama ni jipya, nililozowea mimi ni kuweka wakili basi, lakini tena kuchagua na Mwendesha Mashtaka, sasa sijui kama likiweko hilo na wakili pia ana haki ya kuweka.Kwa hivyo, awe na Mwendesha Mashtaka na wakili wanashirikiana wote wawili katika suala la mtu huyo aliyechagua Mwendesha Mashtaka.

Mhe. Spika, kifungu cha 15(6) hapa kunaelezewa mambo ya mtu aliyeruhusiwa kufanya kazi ya kuendesha mashtaka katika hawa wanaoombwa, mtu huyu naye kapewa ruhusa ya kuwa anaweza akafanya yeye mwenyewe ile kazi

aliyoteuliwa au anaweza akamtaka wakili aifanye ile kazi. Sasa swali langu ni kwamba kwa nini basi asiteuliwe huyo huyo wakili tu moja kwa moja, kuwa mtu amteuwe mtu halafu na huyo aliyeteuliwa na yeye ateuwe mwengine. Kwa sababu maana yake ni kuwa huyo aliyeteuliwa kateuliwa lakini kazi yenyewe haiwezi, ndio maana akatafuta wakili sasa aifanye kazi ile ambayo kapewa yeye.

Sasa mimi nafikiri pengine ufahamu wangu mdogo lakini nina haja ya kuelewa je, huyu mtu sasa yeye kateuliwa awe Mwendesha Mashtaka wa kesi fulani, kwa nini tena yeye akateuwe wakili, kwa nini kazi hiyo asiifanye yeye aliyeteuliwa. Hivi wakala anaweza kuwakilisha?

Mhe. Spika, katika mambo ya Kiislamu ninavyosikia Masheikh wakisema, maana mimi sio sheikh lakini Masheikh nawasikia wakisema kuwa wakala hawakilishi. Sasa sijui katika sheria zetu hizi za kidunia kama wakala ataruhusiwa na yeye kuwakilisha.

Mhe. Spika, nikija kwenye kifungu cha 17(c), kifungu hiki kinaelezea moja katika majukumu ya Mkurugenzi wa Mashtaka atawashauri waathirika wa uhalifu. Hapa naomba nifafanuliwe, katika mambo haya nitakayoyauliza.

Waathirika wa uhalifu waliokusudiwa hapa ni wepi, waliofanyiwa uhalifu, waliofanya uhalifu au waliohukumiwa na wakatiwa makosani kwa uhalifu. Ni waathirika wapi wanaotakiwa na sheria hii awape ushauri. Hili naomba nifafanuliwe angalau na mimi niburudishe moyo wangu, kama yule Mtume alipotaka aoneshwe jinsi ya kufufua. Nabii Ibrahim. Alisema hapana sio kwa kuwa siamini Mola wangu, lakini kwa sababu *Liyatuma Innal Qalbi,* kidogo niuridhishe tu moyo wangu. Kwa hivyo, na mimi naomba hapa *Liyatuma Innal Qalbi* Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 17(d), hapa Mkurugenzi kwa mujibu wa sheria hii anatakiwa atowe taarifa. Sasa jambo ambalo silielewi na ambalo hapa halikuelezwa, taarifa hii anatakiwa aitowe wapi? Ni ile taarifa aliyoambiwa amwambie Waziri kila wakati au taarifa hii ya kifungu hiki kuna sehemu nyengine ambayo anatakiwa atowe taarifa. Hili nalo naomba nieleweshwe. Mimi leo mengi yangu yatakuwa ni maswali tu.

Mhe. Spika, nikija katika kifungu cha 18(1)(a), kuna swali hapa naomba ninukuu, nitaanzia hapo hapo kwenye (a) kwa sababu inaeleweka.

Kifungu 18(1)(a):

> "Hatoshughulikia kesi yoyote ambayo ana maslahi ya kibiashara ya mali au kifedha"

Mhe. Spika, swali langu. Je, fedha si mali, maana ikiwa fedha ni mali hakuna haja tena ya kuitaja tena hiyo fedha, la ikiwa fedha si mali basi iko haja ya kuitaja fedha, lakini ikiwa fedha nayo ni mali basi hakuna haja ya kuitaja, mali ingetosha. Lakini hapo hapo katika kifungu cha (b) kinasema,

Kifungu cha 18(1)(b):

> "Ataweka wazi maslahi aliyonayo katika kesi kama ilivyoelezwa katika aya (a) ya kifungu hichi au kesi yoyote inayomuhusu mke au mume wake au jamaa yake wa kurithiana"

Sasa hapa kuanzia au kwa nini nayo isiwekwe katika (a). Katika kesi ambayo hataishughulikia, kwa nini na hizi kuanzia au zisiwekwe pale nazo hizi asizishughulikie, hizi zikawekwe kwenye kujieleza tu, lakini kwenye kuzishughulikia anaweza kuzishughulikia. Kwa hivyo, sijui kama imewekwa hivi makusudi au ni kwa kusahau jicho kupitikiwa. Ikiwa imewekwa makusudi, basi mimi nadhani kuwa na hapa kwenye au napo ingeingizwa katika kifungu (a) halafu ikaingia vile vile katika kifungu cha (b).

Mhe. Spika, nikija katika kifungu cha 19(1)(a), suala hili mwenzangu Mhe. Fatma kalizungumza, lakini na mimi nataka nilitilie mkazo tu kwamba miongoni mwa mambo ya kuwa kutoheshimu ile habari ya kuwa mwanachama wa chama, basi hili lingewekwa mahala pengine, lisingewekwa kuwa ni moja katika mambo ambayo atakuwa hana heshima akilifanya hilo.

Mhe. Spika, sasa niende katika kifungu hicho hicho cha 19(4). Mhe. Spika, katika kifungu nilichokitaja Mkurugenzi wa Mashtaka kapewa nafasi ya kutunga kanuni za sheria hii. Mara nyingi huwa tunapitisha sheria na mawaziri huwa wanapewa nafasi ya kutunga kanuni za sheria tunazozipitisha, lakini hukaa mara nyengine miaka miwili au mitatu kanuni zile bado hazijatungwa. Naomba Mkurugenzi asifuate nyayo hizo, mara sheria itakapokuwa tayari basi na kanuni azitunge haraka haraka, ili utekelezaji wa sheria hii usiwe na matatizo.

Mhe. Spika, labda nikiacha vifungu vya mswada nije kidogo katika mambo ambayo katika utekelezaji wa uendeshaji wa kesi hizi, naona labda kuna matatizo na pengine Mkurugenzi atakuwa na njia ya kusaidia katika matatizo hayo. Katika utaratibu unaoendelea hivi sasa na inawezekana ukaendelea na baada ya sheria hii, ni kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka au Mwendesha Mashtaka aliyewekwa na Mkurugenzi, inapotokea kesi, mshtakiwa katika hali yoyote ile Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ikaona kuwa mshtakiwa huyu asingestahiki kupewa dhamana, kutokana na ama matukio ya nyuma yaliyotokea kumuhusu yeye au jambo jengine lolote ambalo Mkurugenzi kaliona akipewa dhamana litachafuka, bado Mahakama inatoa dhamana.

Kwa hivyo, suala hili linasababisha kesi nyingi ama zikwame au zife kabisa baada ya muda fulani kupita. Sasa suala hili sijui litachukuliwa hatua gani ya kufaa ili Mkurugenzi awe na nafasi ya kusema, huyu kutokana na matukio moja, mbili na tatu aliyoyafanya basi asingestahiki kupewa dhamana na hilo Mahakama ikapewa uzito wa kulichukua, kuliko utaratibu unavyokwenda hivi sasa.

Halafu Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo imebainika kuwa kuna watuhumiwa ambao Mwendesha Mashtaka anaomba wasipewe dhamana, Hakimu anawapa dhamana na baadae wanatoweka. Sasa unaweza ukafikiria aah hili lilifanywa kusudi au ni bahati mbaya au ni kwa sababu Mwendesha Mashtaka hakusikilizwa. Nafikiri suala hili kuna haja kubwa ya kuangaliwa vizuri ili wanaofanya makosa wasipate nafasi za upenyo wa kupenyuka. Waweze kufikishwa mbele ya Mahakama na wahukumiwe kwa mujibu yalivyoonekana.

Mhe. Spika, zaidi ni kuwa hao watuhumiwa wakishakimbia ndio basi tena, hakuna juhudi yoyote inayofanywa ya kuwatafuta, mtapishana nao njiani lakini huwa hakuna juhudi yoyote ya kuwatafuta pale ambapo hawahudhurii katika kesi zao.

Mhe. Spika, mswada huu ni muhimu sana. Kwa sababu ni mswada ambao utasaidia sana katika kulinda haki za watu, yaani haki za waliodhulumu na wale walidhulumiwa, pia wanaosingiziwa pamoja na wanaoonewa. Sasa kwa maana hiyo, mimi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja *(Makofi)*.

Pamoja na hayo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, aje anipatie majibu ya yale maswali ambayo kwa ujinga wangu siyafahamu *(Kicheko/Makofi)*.

Ahsante sana Mhe. Spika *(Makofi)*.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Spika, nami naomba nikushukuru kwa kuniruhusu kutoa mchango wangu kuhusiana na sheria hii. Kwa kweli sina mchango mkubwa isipokuwa nina maswali. Lakini mimi ni mmoja katika *victim* wa masuala haya. Kwa hivyo, masuala mengine nitakapouliza ninayo uzoefu nayo.

Kwanza naomba ufafanuzi kwa sababu wataalamu wapo kule pembeni watamsaidia Mhe. Waziri, hivi sasa tunajitahidi kuiweka hii sheria ya *Prosecutor*, lakini kuna sheria iliyoanzisha Jeshi la Polisi, niliwauliza wataalamu walisema ndio ile *caption three, two, two*. Kwa sababu Polisi ni Jeshi la Muungano na sheria hiyo au sura hiyo inaeleza hata taratibu za kukamata pamoja na mambo mengine, sasa sisi hapa tunatayarisha afisi ya *Prosecutor* pamoja na taratibu za kukamata.

Kwa hivyo, kwanza hii sisi sidhani kama Zanzibar tunayo kwa sababu ni ya Muungano, lakini je, hii sheria imeshaletwa kwa taratibu za kikatiba kuwa *adopted* hapa, yaani hii *caption three, two two*. Je, hakutakuwa na mgongano wa amri ya sheria hiyo na hii Afisi? Hilo ni swali ambalo naomba nisaidiwe.

Mhe. Spika, tunaishi Zanzibar na tunajua kwamba tunao polisi pamoja na vikosi vyengine, kama vile vya KMKM ambacho kimeanzishwa kwa sheria na kazi zake zinajulikana, kuna JKU, Valantia. Lakini kuna wakati vyote hivi huwa vinatukamata na mara nyengine unakuta KMKM anamkamata raia, kesi hizo zipo na hasa yanapoanza masuala ya uchaguzi, huwa hakuna bwana tena, isipokuwa bwana ni yule mwenye silaha (bunduki).

Kwa hivyo, nani mwenye dhamana ya kukamata mtuhumiwa, maana kuna hatari kwamba kila mmoja kwa sababu anayo bundiki anaweza kukamata, basi inaweza kusababisha vurugu na mara nyengine huzaa mapambano ambayo si ya lazima.

Kwa maana hiyo, nategemea muendesha mashtaka sina hakika kwamba ataweza kuwaambia kwamba jamani hii si kazi yenu wacheni, hasa tukilinganisha sheria hii na Mwendesha Mashtaka yuko kwenye wizara tofauti na vile vikosi, pengine labda mawaziri wanaweza kuzungumza. Kwa kweli hilo ni suala la msingi sana.

Mhe. Spika, jambo la tatu nadhani sisi wengine kama watu wanavyosema si wanasheria, lakini taaluma yetu ya *Management*. Tukiangalia kifungu Nam. 4 cha sheria kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa Afisi, baada ya maelezo machache pale inaanzisha Afisi itakayokuwa kadhaa, halafu imekwenda kumtaja Naibu Mkurugenzi katika sehemu ile. Mhe. Rais anaweza kuteua Naibu Mkurugenzi, uanzishwaji na uendeshaji wa Afisi.

Nadhani katika suala hili kama mimi ningetegemea hapa kutajwa kazi za Mkurugenzi kwanza, halafu zikatajwa kazi za Naibu Mkurugenzi. Lakini kazi za Mkurugenzi zimekwenda kutajwa kifungu Nam. 9 kwenye sehemu inayoitwa Udhibiti na Uratibu wa Uendeshaji wa Mashtaka. Kwa hivyo, atakuwa mtendaji mkuu wa afisi kwa kuzingatia kadhaa, kuelekeza polisi, yaani utaona kazi zake zimetajwa hapa na kule mwanzo zimetajwa kazi za Naibu Mkurugenzi.

Mhe. Spika, jambo jengine namuombea Mkurugenzi wa Mashtaka kwamba huyu Naibu ametajwa mafao yake, kwamba Naibu Mkurugenzi atalipwa mshahara pamoja na mafao mengine yakiwemo mafao ya kumaliza muda wa Naibu Mkurugenzi. Lakini niliposoma haya ya bwana mkubwa mwenyewe, yaani Mkurugenzi hakutajiwa mafao na nilipoulizwa wataalamu waliniambia labda kwenye Katiba, nilipoangalia Katiba hakuna maelezo hayo.

Kwa kweli ni vizuri katika kuitangaza hii Afisi na bahati nzuri kifungu Namba 5 kimeeleza kwamba atashirikiana na Idara ya Utumishi katika kuanzisha *structure* pamoja na utumishi. Sasa unapoanzisha *Scheme of Service* haihitaji kipande kipande, yaani inakuwa ni kitu kilichokamilika.

Kwa mfano Mkurugenzi, Naibu Mkurugenzi, labda *Prosecutor*, Idara ya Hesabu, *Internal Auditor* pamoja na wengine na halafu kila moja inatajwa majukumu yake na kueleza *Job Description*, halafu inataja na maslahi.

Kwa hivyo, Mkurugenzi wa Kuendesha Mashtaka kazi zake ni utaalamu pamoja na kusimamia utawala, lakini kila sehemu ya ile Afisi inakuwa tayari imetimia na inajulikana nani anafanya nini na wala haiwezi kuwa kipande kipande.

Kwa maana hiyo, katika *establishment of office*, itataja *Director of Prosecution* itataja kazi zake, maslahi yake pamoja na upatikanaji wake, yaani iwe ni kitu kamili. Maelezo ya humu kidogo yametajwa huku na kule, yaani bila ya mpangilio mzuri.

Mhe. Spika, hapa nilikuwa na swali ambalo Mhe. Mohammed Ali Salim alisema la kijinga, lakini nadhani la msingi. Polisi anaponituhumu ananishtaki mimi, lakini mimi namuona polisi amenidhulumu nataka kumshtaki, nakwenda kwenye *infront desk* la Polisi kituo X ,yule bosi anaogopa kuliandika lile suala kwenye *RB* kwa sababu aliyeshtakiwa ni mwenzake. Je, katika *procedure* hizo nakwenda moja kwa moja kwa *DPP* na tunayo mifano hai.

Hivi karibuni tulikuwa na mfano tunataka kumshtaki mtu ambaye ni sehemu ya utawala tumepata tabu sana Mhe. Spika, kwa sababu kila tunapokwenda polisi tunaambiwa mzee kwani hamuwezi kumaliza haya mambo. Baada ya kuona tunakataliwa basi twende juu na tulipokwenda kwa Mkuu wa Upelelezi na yeye alisema mzee sidhani kama kuna haja ya kwenda Mahakamani, subiri tulishughulikie, lakini halikushughulikiwa Mhe. Spika.

Kwa sababu anayetaka kushtakiwa ni sehemu ya watendaji wanaoshtaki. Sasa je, naweza kuja moja kwa moja au ndio ninyamaze na kumezea kukosa na watu unabugunya bila ya kumeza *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, kifungu Nam. 19 ambacho Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, asubuhi alikizungumza kwa urefu. Kwanza kulikuwa na suala la maana ya *Highest Intergrate*, kwa kweli *intergrate* maana yake ni uadilifu. Kwa hivyo, si kitu ambacho hakipo, kama inatafutwa tafsiri natoa mchango wangu huo. Sasa mtu anaweza kuniuliza uadilifu ndio nini nayo ninayo maana yake, lakini hapa si mahala pake.

Lakini sheria ile inasema kwamba Mkurugenzi asiwe *member* wa chama chochote. Kwa kweli ni vizuri lakini hata Sheria ya Vyama Vingi vya Siasa Nam. 5 imesema hivyo hivyo kwamba askari wasiwe *members* wa chama chochote.

Hivi sasa bado tunayo miaka 15 ya kufanya chaguzi na tunawaona askari polisi baadhi sisemi wote, unapomkuta mkereketwa Mhe. Spika hata umwambie kazi yako haikuruhusu kufanya hivi, tena mara nyengine na mavazi yake ya kazi. Sasa kama sheria Nam. 5 iliwekwa na kueleza hivyo, lakini bado tunayaona haya.

Kwa kweli hapa ametajwa yeye tu Mkurugenzi kwamba asiwe mwanachama, wala sheria haikueleza zaidi kwamba wale watendaji wake wote wawe hivyo. Nadhani ni vizuri ingekuwa watendaji wa Afisi ile wote wakawa sio watu wanaoshiriki siasa. Kwa sababu ukeshaanza kutia ushabiki, basi mwenye kosa atakuwa hana na mwenye nalo ataachiwa.

Mhe. Spika, jambo la mwisho ambalo nataka nilizungumze na baadaye nikae niwepe nafasi wenzangu. Kwa sababu sina matatizo na mswada huu na ninaunga mkono na kwa kweli ni muhimu hata kama haitakuwa nzuri kwa kuanzia, lakini kwa kuwa tumeanza ndio tunajenga.

Isipokuwa tatizo langu ni moja tu, nimeyaona Mhe. Spika, nimeyashuhudia na wala si vizuri kurudia, nimeshamuona mtu amekaa jela miezi sita na kesi ya kuku, ushahidi haujakamilika mpaka Mhe. Said Ali Mbarouk, alikuwa akitoa

mfano wa mkoba wake. Kwa kuwa kijana yule aliniuliza babu nifanye nini? Hivi sasa ni miezi sita, basi nilimuuliza kweli umeiba kuku? Aliniambia kweli nimeiba kuku, lakini sio kesi hii waliyonikamata. Sasa aliniambia kila nikienda naambiwa ushahidi haujakamilika.

Mhe. Spika, nistahamilie nilimshauri vibaya, lakini ilimsaidia. Kwa hivyo, nilimwambia utakapokwenda Mahakamani kwa mfano ukeshaulizwa Mhe. Juma Duni Haji, naam, unashtakiwa kwa kuiba kuku, nilimwambia kuanzia hapo usiseme nyamaza, aliniuliza itakuwaje, nilimwambia itakuwa hakuna kesi utarejeshwa ndani, nilimwambia utafanya? Aliniambia nitafanya.

Kwa hivyo, alipokwenda akafanya kama vile nilivyomwambia, basi Jaji alimwambia mbona husemi, aliambiwa mrejeshe ndani. Kwa kawaida baada ya wiki mbili unarudi tena, aliporudi aliniambia babu nilikwenda sikusema, basi nilimwambia ukienda tena fanya hivyo hivyo.

Mhe. Spika, alipokwenda mara ya pili kwa mfano Juma Duni Haji, naam, unashtakiwa umeiba kuku, alinyamaza kimya, basi Jaji alianza kuhamaki sasa wewe husemi na baadaye kurejeshwa ndani, aliporudi aliniambia babu sikusema, nilimwambia vizuri na nilimwambia utakapokwenda mara ya tatu fanya hivyo hivyo. Kutokana na hali hiyo basi mara ya tatu kesi ilifutwa *(Kicheko/Makofi).*

Sasa nilichokusudia Mhe. Spika, hakuna mpaka ya kusema zaidi ya hapa Polisi hatukuruhusu tena, hivi *investigation* hii ni *definite* na wewe jaji humuonei huruma huyu kwamba anangojea apate haki, kinachomfanya asipate haki ni uzembe wa polisi kutokufanya kazi yake. Jaji bado unamwambia rudi ndani. Mhe. *DPP* hakuna muda wa kusema inatosha.

Mhe. Spika, baada ya hayo, nakushukuru na unga mkono mswada huu *(Makofi).*

Ahsante sana.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuzungumza jioni hii ya leo. Kwanza kabisa kwa dhati ya moyo wangu napenda kutoa shukurani za dhati kwako wewe binafsi kwa pongezi nyingi ulizotupongeza pamoja na Wajumbe wote waliosimama hapa na kutupongeza, tunasema ahsante sana *(Makofi).*

Kwa kuanza na mchango wa kuhusiana na hoja ambayo ipo mbele yetu. Mhe. Spika, Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora ni wizara ngumu sana, ninaamini kwamba kwa juhudi hizi *inshaallah* tutafika.

Suala la kwanza ambalo nataka kulizungumza ni kuhusu masuala ya majengo ya Mahakama. Kwa kweli majengo haya ambayo yamejengwa wakati huo Zanzibar ilikuwa na population ya watu 200,000 mpaka 250,000. Leo wananchi wa Zanzibar wamekuwa ni milioni na baada ya miaka kumi watakuwa ni milioni na zaidi.

Kwa hivyo, majengo haya hivi sasa yamekuwa hayakidhi haya hasa ya kufanyakazi kama Mahakama. Kwa sababu ni majengo ambayo yanatumika kwa mfano Mwanakwerekwe, yaani ni majengo ambayo hayana hadhi wala sifa ya kuwa Mahakama, isipokuwa ni majengo ya kuingia watu na kufanyakazi zao. Kwa kweli majengo ya Mahakama naya sheria pamoja na hadhi zake.

Kwa mfano jengo la Mahakama liliopo hapa mjini Vuga limekuwa *congested*, yaani majaji wote wamo kwenye Afisi ndogo ndogo na katikati kuna uchochoro mwembamba, ambapo watu wakikaa wanaambiwa waondoke na wote wanataka kuingia huko kwa Jaji.

Wakati wanapokuja wageni na kutaka kuonana na Mrajis wa Mahakama, basi huyo *secretary* wake amekaa kwenye kichochoro ambacho ni kidogo sana. Kwa kweli ni sehemu ya kukaa watu watatu, basi anakaa *secretary* pamoja na wageni wote wanaokuja pale na suti zao kwa ajili ya kusubiri kuonana na Mhe. Mrajis wa Mahakama.

Mhe. Spika, hali kama hii na pahala ambapo wanakuja wageni mbali mbali kutoka ndani na nje ya nchi. Kwa hivyo, mtu yeyote anayekwenda kwenye Mahakama ambazo mipango yake iko kama hivyo, anahisi kwamba je, ah! Mimi nitapata haki yangu, pahala kama hapa na hali hii, kazi zinafanywa labda masikiti *(Makofi)*.

Kutokana na hali hiyo, napenda kusema kwamba ipo haja kwa hivi sasa kufikiri angalau mpango wa kujenga Mahakama nyengine ambayo kwamba itakidhi haja ya wakati tunaokwenda nao.

Suala jengine ni kuhusu mahabusu zetu vile vile nazo zimeshapitwa na wakati. Kwa kweli mahabusu zetu zinafanyakazi zile kabla ya Mapinduzi, kwa sababu mahabusu si pahala pakwenda kumtesa mtu. Isipokuwa ni sehemu ya kumuweka mtu kizuizini mpaka pale apate haki yake.

Kwa mujibu wa Haki za Binadamu chini ya Mkataba wa Kimataifa wa mwaka 1949, mtu yeyote duniani hawezi kuwa mkosa mpaka Mahakama kuu na ya dhahiri imuidhinishie kosa lake pamoja na hiyo hukumu.

Kwa hivyo, hata mtu akiwa rumande yumo kwenye adhabu na ikiwa ataambiwa hana kosa, basi tayari ameshaadhibiwa vya kutosha huko ndani. Mhe. Spika, pia ninaomba mahabusu zetu zibadilike. Kwa sababu mahabusu ni pahala ambapo kwamba si pakuomba mtu lakini yeyote yule anaweza kuingia, kwa mfano mimi au mwengine yeyote na Mwenyezi Mungu atunusuru. Kwa kweli hali ya mahabusu zetu zinatisha.

Mhe. Spika, vile vile, kuhusu ufanisi wa kazi za polisi. kwa mfano kwenye Mahakama zetu utakapokwenda utaona kesi nyingi sana zinaahirishwa tena mara kwa mara na watu wanarudishwa mahabusu.

Kutokana na hali hiyo, serikali inapata hasara kuwashughulikia wafungwa wengi ambao kesi zao zinaweza kumalizika kwa muda mfupi, lakini serikali inapata hasara kuwahudumia wale mahabusu. Sambamba na hilo, wanachelewa kupata haki zao, kwa sababu kutompa haki yake mtu ni kumdhulumu. Kosa la polisi ni kwamba hawawezi kuweka ushahidi bayana kwa makusudi au kwa uvivu tu. Kwa sababu kesi nyengine ziko *very clear*, lakini zinachukua muda mrefu na wala jaji hawezi kuhukumu, kwani kesi hizo hazipati ushahidi.

Lakini baya zaidi, kuna mahabusu wengine wanayo makosa ya wazi, wanafanya makosa kila siku ya kuwaibia watu, wanahujumu watalii, wanavunja maduka, maghala na baadaye wanapopelekwa kwenye Mahakama hawahukumiwi kwa sababu ushahidi haupatikani, kwa kuwa polisi hawafanyikazi zao.

Kwa hivyo, matokeo yake wanaachiwa huru, sasa wanapoachiwa huru ndipo utaona wananchi wanaanza kuchukua sheria mikononi mwao. Kwa mfano mtu anapigwa matofali mpaka anakufa au anajeruhiwa vibaya sana. Mhe. Spika, hali hii inatokana na kwamba polisi wetu bado hawajakuwa tayari kufanya upelelezi, ambao kwamba utampa madaraka Mwendesha Mashtaka au hakimu atoe hukumu kwa mujibu wa makosa aliyofanya mtu.

Mhe. Spika, nimeridhika sana na namna gani sheria hii ilivyojieleza katika ukurasa wa 158 mpaka 159 kifungu cha 24 kuhusu makosa na adhabu. Kwa kweli imedhibiti vizuri sana wale wote wanaoficha *documents* pamoja na ushahidi.

Tukiangalia kifungu Nam. 24 (3), (4), (5), (6) mpaka (7) ni vifungu ambavyo vimezingatia hali halisi ilivyo. Matumaini yangu vifungu hivi ikiwa vitatumika vizuri nadhani vitamsaidia *DPP* kufanyakazi zake vizuri zaidi. Isipokuwa ninaomba hiyo hukumu baada ya miaka mitatu iwe miaka mitano *(Makofi)*.

Mhe. Spika, tukiangalia ukurasa wa 149 kwenye waraka wa Kiswahili imetafsiriwa vizuri sana, Mhe. Spika naomba kunukuu ukurasa wa 149 kifungu cha (2) Waraka wa Kiswahili kinasema hivi:

> "Afisi itakuwa taasisi huru na yenye mamlaka ya kujiendesha ndani ya utumishi wa umma Zanzibar"

Lakini tukiangalia tafsiri ya Kiingereza ukurasa wa 209 Mhe. Spika, naomba kunukuu ukurasa wa 209 kifungu cha (2) Waraka wa Kiingereza kinasema hivi:

> "*The office shall be an independent and autonomous government agency in the Zanzibar public service*"

Mhe. Spika, hapa ndipo hii *autonomous* inaleta matatizo na bado hii ni *agency* ya serikali na itafanyakazi kiserikali.Kwa hivyo, utakuta mambo mengine huko mbele *DPP* tanayasababisha kutofanyakazi zake kiufanisi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, vile vile, naomba tuangalia ukurasa wa 209 hapo hapo kwenye waraka wa Kiingereza na ule wa Kiswahili 149, kwamba Rais ndiye atakayemteua *Deputy Director* kufanyakazi zake kama zilivyoelezwa kwenye waraka huu. Pia, Rais ndiye atakayemtengua au kumuondoa madarakani *Deputy Director*.

Kwa kutokana na hali hiyo, ninayo mawazo kwa nafasi hii tusingemuachia Rais kuteua *DPP*, Naibu na halafu yeye amuondoe tena. Kwa hivyo, hapa nadhani kama kutakuwa na *contradiction*. Kwa kweli, naomba huyu Naibu Mkurugenzi basi nafasi hiyo itangazwe na waombaji mbali mbali ambao watakuwa na vigezo ambavyo vimetolewa na *DPP* au Kamati yake ya Ushauri, kuona kwamba tunamtaka Naibu Mkurugenzi mwenye sifa mbili, tatu ama nne, tano, sita na hata saba.

Kwa maana hiyo, wale wote wenye sifa zile waombe nafasi ile. Hii itatoa fursa ya uwanja mpana zaidi ya kuweza kuchagua mtu bora kabisa ambaye atafanyakazi vizuri zaidi na ufanisi utapatikana mkubwa zaidi na kuliko kupendekeza mtu fulani.

Pengine katika watu 15 anaweza kupatikana mtu mmoja ambaye *qualification* zake zitazidi wote na atafanyiwa usaili. Kwa hivyo, baada ya usaili kwenye watu 15 watabakia watatu na watafanyiwa usaili tena na hatimaye atapatikana

mtu mmoja ambaye ni *best* atakayeweza kufanyakazi zake vizuri na kumsaidia *DPP* na kazi za sekta hii itakuwa za ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu kwenye ukurasa wa 157 kuhusu Kamati ya Mashauriano, naomba kunukuu ukurasa wa 157 kifungu cha 23 (1) kinasema hivi:

> "Kwa madhumuni ya kuendeleza ufanisi katika usimamizi wa sheria za jinai na uendeshaji wa mashtaka, inaanzishwa Kamati ya Mashauriano ambayo itakuwa na muundo ufuatao"

Kwa hivyo, itakuwa kama ilivyoelezwa pale. Sasa jopo hili ambalo litamsaidia *DPP* katika kazi zake, naona kwamba kazi za jopo hili ni chache sana. Nadhani kuna haja ya kuangalia kwamba jopo hili litamsaidia vipi *DPP* katika kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, baada ya kutoa mchango wangu huo, napenda kutamka rasmi kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naitakia kila la heri *(Makofi)*.

Mhe. Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja: Mhe. Spika, nashukuru nami kunipa nafasi, ili nikaweza kutoa mchango wangu mdogo. Kwa sababu nilikuwa na mengi ya kusema lakini kanuni inatuzuia tusirudie jambo ambalo limeshazungumzwa. Kwa hivyo, yale madogo yaliyobakia bakia ndio nitakayozungumza *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, kweli serikali imeamua kuingia kwenye Utawala Bora na kudumisha demokrasia nakumbuka miaka ya nyuma polisi ndio wakikamata, polisi ndio wakichunguza, polisi wakisimamia anakuwa mtu tofauti hapo ni Jaji tu. Kwa vile ilikuwa ni rahisi kwa polisi kupanga mtu anayempenda akaingia hatiani na asiyempenda akaweza kutoka hatiani. Lakini kwa utaratibu huu wa sasa hivi polisi ni kukamata na kuchunguza apeleke kwa DPP, halafu wao ndio wanapanga hizo kesi na inakwenda kwa mtu wa tatu ambaye ni Jaji. Hiyo ndio demokrasia ya kweli na ndio Utawala Bora.

Mhe. Spika, kuna kitu kingine mimi mpaka leo kinanikera kweli, kwamba polisi kujifanya Mahakimu. Mhe. Spika, hivi karibuni kuna jamaa mmoja alimbaka mtoto wa miaka 10 wazazi wake wakaenda polisi, walipokwenda polisi wakaenda kumtafuta huyo mtuhumiwa wakamkamata wakampeleka polisi.

Kwa hivyo, hapo sijui kilifanyika kitu gani kwani polisi waliwaita wazee wale wakamwambia yule mtuhumiwa huyu mtoto umuoe uliyemuharibu na mtoto

wenyewe ana umri wa miaka 10. Mhe. Spika, mtoto wa miaka 10 polisi wanasema aozeshwe mtoto huyo eti hiyo ni kutoa hukumu. Halafu inakuwaje mtoto wa miaka 10 aolewe, sheria ndio ilivyosema na mwisho wakaambiwa kama hamtaki basi nendeni zetu, hayo ndio yamekwisha.

Kwa bahati wale wazee wakarudi tena lakini kuna mwalimu wake wa chuoni yule mtoto ndio akawasiliana na mimi kunielezea ile hali ilivyo na mimi nikachukua juhudi nikasema lazima akamatwe apelekwe Mahakamani. Alikamatwa na akapelekwa Mahakamani, lakini alipopelekwa Mahakamani siku hiyo hiyo akapewa dhamana. Kwa hivyo, hapa naomba Mhe. Waziri hebu tusaidie mbakaji ambaye anambaka mtoto mdogo anamharibu au jambazi limetumia silaha kwa nini wapewe dhamana? Najua dhamana ni haki yake mtu, lakini kuna mambo mengine hayataki dhamana, hawa ni wauwaji ukimpa dhamana unampa nafasi nenda ukafanye tena uhalifu.

Mhe. Spika, pia, hivi karibuni katika Mkoa wa Kusini Unguja tulipata ujambazi, jamaa wamekwenda wameivamia hoteli, wamewanyanganya watu vitu wakakimbilia mwituni, polisi walijitahidi kuwatafuta.Pia, tukaomba msaada wa mbwa wa polisi wakapelekwa na hatimaye majambazi watano tumewakamata. Katika kuwahoji majambazi hao wawili walishiriki katika ujambazi uliofanyika hapa mjini na wamepewa dhamana, wamekwenda kufanya mwengine kule. Kwa hivyo, kwa nini watu kama hawa wapewe dhamana hapo ndipo panaponisumbua mimi.

Mhe. Spika, kuna kesi za kupewa dhamana kama aliyoisema rafiki yangu pale ameiba kuku, baiskeli haina taa, kengele, hizo ndio kesi za kupewa dhamana, lakini mtu anamharibu mtoto, ujambazi halafu anakwenda kupewa dhamana, hilo naona ni tatizo. Baada ya dibaji hiyo sasa nije kwenye mswada huu.

Mhe. Spika, kuna vipengele kidogo vinanisumbua. Kipengele cha 18(a) kinasema hatashughulikia kesi yoyote ambayo ana maslahi yake ya biashara au mali au ya fedha. Lakini kipengele hicho hicho (b) kinasema ataweka wazi maslahi aliyonayo katika kesi kama ilivyoelezwa katika aya yake, huku ataweka wazi maslahi huku hatakuwa na maslahi. Hapa kidogo inanipa shida lakini kama walivyosema wengi lugha za kisheria wengine hatuzijui, maana lugha za kisheria na lahaja wakati mwengine zinaweza zikakusumbua.

Mhe. Spika, kuna mtu mmoja kule Magomeni anaitwa fundi, siku hiyo akakumbana na jamaa yangu mmoja kutoka huko nyumbani anamwambia watu pia wanakwita fundi kuundu nini, fundi akahamaki akamwambia unanitusi, akamwambia sijakutukana ila nakuuliza umeunda nini. Kwa hivyo, ile lahaja yeye imemshinda kuifahamu akaona kama anatukanwa pengine na hapa pana maneno mazuri lakini mimi sikuyafahamu. Ningelimuomba Mhe. Waziri

kidogo anifahamishe. Mwisho anamalizia au mume wake au jamaa yake wakurithiana hapa ningeliomba aongezwe na rafiki maana urafiki ukiwa mkubwa nao unaweza kwenda mchomo.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo linanipa mashaka ni kwenye kifungu cha 19(2) anasema tuhuma za kuvunja kanuni za maadili dhidi ya Mkurugenzi zitawasilishwa rasmi kwa Rais baada ya kutafakari tuhuma zenyewe anaweza kuamua kuanzisha uchunguzi rasmi au kutoanzisha uchunguzi. Lakini hapa ndio panaponitia mashaka mimi kwamba katika hali yoyote hakuna uchunguzi utakaoanzishwa bila ya Mkurugenzi kutoa fursa ya kufahamu tuhuma dhidi yake na kupata fursa ya kutoa maelezo yake juu ya tuhuma hizo.

Mhe. Spika, kwa mfano sasa unatuhumiwa unataka kufanyiwa uchunguzi halafu unasema upewe taarifa kwamba bwana sasa tunakuchunguza, si utafanya maarifa uchunguzi huo ufeli. Kuna watu wanapelekwa Mahakamani na kesi inakwenda *DPP* anamwambia Jaji pamoja na kwamba ana haki ya kupata dhamana lakini tunaomba asitoe dhamana kwa sababu ataharibu uchunguzi.

Kwa hivyo, huyu anapewa taarifa kabisa kwamba unachunguzwa mambo haya ndio vipi, naona Mkurugenzi hapa kajipendelea kidogo. Haki ya kujitetea apewe lakini sio haki ya kuambiwa kwamba sasa tunakuchunguza bwana ukae tayari, nafikiri hii itakuwa sio sahihi.

Mhe. Spika, jengine kwa maana hiyo hiyo kifungu cha 6 kuvunja kanuni za maadili kunaweza kupelekea mhusika kufukuzwa kazi, kusimamishwa au kufutwa kwa uteuzi wa Mwendesha Mashtaka na atakapotokea kusimamishwa kufutwa kwa uteuzi kama Mwendesha Mashtaka, mtu huyo anaweza kubaki katika utumishi wa serikali lakini hatafanya kazi ya uendeshaji mashtaka kwa muda wote ulioelezwa katika amri ya kusimamishwa au kufutwa. Lakini huyu moja kwa moja anafukuzwa, anafutwa anaruhusiwa kufanya kazi pengine serikalini, lakini hata hiyo nafasi ya kupewa ajitetee hakupewa.

Kwa hivyo, nafikiri na huyu angepewa nafasi ya kujitetea sio kujuulishwa kwamba tunakuchunguza sasa ila apewe nafasi ya kujitetea. Mhe. Spika, nchi yetu sasa hivi fitina zimekuwa nyingi anaweza kutiliwa fitina Mkurugenzi zikamuingia akaona huyu hafai nimsimamishe. Lakini akimpa nafasi ya kujitetea basi atajua pengine zilikuwa tuhuma sio kweli.

Mhe. Spika, jengine ni katika haya marekebisho wanasema kumeongezwa kifungu kipya kitakachosomeka kifungu (e) ambacho kitasomeka kama ifuatavyo. Kubuni na kutoa mipango ya mafunzo yanayohusika. Pia, vifungu vyengine vinasema kwamba vitaathirika kwa kufuata utaratibu huu. Sasa kama

vitaathirika vina haja gani si wangesema vifutwe au wangetupa maelezo vitaathirika vipi. Kwa hivyo, hapa kamati kidogo haikutupa maelezo mazuri labda Mhe. Waziri kwa sababu pengine alikuwepo katika mjadala wa kamati anaweza kutusaidia.

Mhe. Spika, jengine katika kifungu cha 23 kwa madhumuni ya kuendeleza ufanisi katika usimamizi wa sheria za jinai na uendeshaji wa mashtaka inaanzishwa Kamati ya Mashauriano ambayo itakuwa na muundo ufuatao. Wengi wamesema hawajui kazi ya kamati hii itakuwa nini. Lakini huku mwisho aya inasema Wajumbe wengine watatu watakaoteuliwa na Waziri kuwakilisha jumuia au asasi zenye maslahi katika uendeshaji wa mashtaka. Hawakuelezwa hawa ni watu gani au wanatakiwa wawe na sifa gani au elimu gani.

Kwa hivi sasa Waziri ni mtu wa Uzini anaweza kwenda Uzini akamchukua mtu akamuweka akamwambia umehangaika kutafuta kazi basi njoo ukae hapa. Kwa hivyo, hapa kidogo zingelielezwa hizi sababu zao angalau sifa zake huyu mtu akajulikana ili Waziri asifanye upendeleo katika kutafuta mtu ambaye atasaidiana na kamati hii, lakini na hii kamati tungejuilishwa tukaijua.
Mhe. Spika, mengi yameshasemwa na sitaki niyarudie rudie.Kwa hivyo, nashukuru na naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru na mimi kuniona jioni ya leo kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu.

Mhe. Spika, mswada huu unaohusiana na kuanzishwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Mimi nina fahari kubwa juu ya suala hili pengine na mwenzangu Mhe. Abubakar Khamis Bakary, sisi tulikuwa ni Wajumbe wa Kamati ya Mwafaka ile iliotiwa saini tarehe 9 Juni, 1996 na moja katika kazi yetu kubwa ilikuwa kuangalia vyombo hivi vyenye mhimili wa serikali. Kwanza vyombo vya Mahakama, Sheria ya Uchaguzi pamoja na Katiba.

Mhe. Spika, kwa niaba ya vyama vilivyotuteua tulifanya kazi hii kwa uadilifu mpaka tukamaliza kazi. Moja ya mazao ya kazi hiyo ni kuangalia katika upande wa Mahakama na mapungufu tuliona kuwa chombo hiki hakipo na tulipendekeza kuwa taasisi hii ianzishwe ili kuwe na Utawala Bora. Kwa hivyo, Mhe. Spika, leo kuijadili, mimi naona fahari kuwa ni moja kati ya matunda ambayo na mimi nilichangia katika historia ya siasa ya nchi hii. Mhe. Spika, najipongeza kwa hilo na nampongeza Mhe. Waziri kuleta mswada huu.

Mhe. Spika, serikali imeleta mswada huu katika lengo lile lile la kukamilisha dhamira ya Utawala Bora nasikia Wajumbe hapa wakiilalamikia serikali kuwa askari ndio waliokuwa wakikamata na wakihukumu hapo hapo na haki ilikuwa

haifanyiki. Hata hapo ilipokuwa ikifanyika hiyo haki watu walikuwa hawaridhiki kwa sababu na sisi tuko katika ulimwengu wa kisasa wenye Utawala Bora ndio tukakubaliana kuanzisha Afisi hii. Mhe. Spika, tulianzisha sheria mama na hii ni ya pili inayoweka utaratibu mzuri wa kisheria katika kufanikisha au Afisi hii iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, nawashukuru watendaji wa Afisi hii hasa Mwendesha Mashtaka na wasaidizi wake kwa mswada huu ambao umefanywa kwa lugha nyepesi inayofahamika. Bahati nzuri mimi nimeshawahi kupitia kwa kuusoma, lakini pia ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza hili, tumeupitia wote na tumeukubali.

Mhe. Spika, jambo lililonisimamisha hapa ni kwamba wananchi wangu wa Jimbo la Koani na mimi wanisikie kuwa na mimi nimezungumza ndani ya Baraza hili na kabla sijaendelea basi nitamke kuwa mimi naunga mkono hoja hii.

Mhe. Spika, jambo ambalo nataka kulichangia la mara moja kwanza ni katika kifungu cha 6(1) cha mswada huu katika ukurasa wa 149 hapa imeelezea wafanyakazi wa Afisi na uajiri wao. Mhe. Spika, wakati nikiwa kwenye kamati nimetilia mkazo kuwa Mhe. Waziri atupie macho kwa wafanyakazi wa eneo hili kwa sababu kazi wanazozifanya ni nyeti, mazingira magumu na ambazo zinatishia maisha ya watu. Kwa hivyo, tunamtaka Mhe. Waziri wafanyakazi hawa mbali ya kuwa ni wanasheria lakini kuhakikisha wanaangaliwa wawe watu ambao watakuwa na uwezo wa kutosha kwa kuzikabili kazi za Afisi hii.

Mhe. Spika, pia kipengele hiki kinasema kuwa watumishi hawa watakuwa wanahifadhiwa na kanuni za utumishi serikalini. Kwa hivyo, tunajua sote kanuni zetu za utumishi serikalini na hasa posho zinazotolewa na mishahara na uwezo wa wataalamu wa Afisi hii. Mimi Mhe. Spika, nina hofu kutokana na uzito wa shughuli hizi pia na majukumu yaliyopo na watu wa aina hii sasa hivi wana soko kubwa hasa wakati huu kwani tunaingia katika soko la kimataifa.

Mhe. Spika, watu wa fani hizi za sheria wanahitajika sana na hasa wanaotoka visiwani ni watu wenye tabia nzuri. Kwa hivyo, watu hawa watakuwa wakitakiwa sana katika soko hili. Mimi nahimiza kuwa watazamwe mbali ya hizo posho zetu za utumishi, lakini ziwe za kuvutia zaidi tusiwafanye wapunguze kazi au kuhama hama. Kwa hivyo, kwa mantiki hiyo waajiriwa wa Afisi hii watupiwe macho zaidi ili wasije wakababaika.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kwamba kuna mamlaka ya Afisi ya Mwendesha Mashtaka yameelezwa hapa. Haya yatasaidia manung'uniko kwa wananchi, lakini kazi kubwa itakuwa ni ya kutoa taaluma namna ya kutumia fursa

zilizowekwa na Afisi hii kwa mwenye kushtaki kwa sababu hii ni haki lazima wananchi waweze kujua namna ya kutumia. Mhe. Spika, tumezoea mwananchi akaenda polisi faili likipotea huwa ndio basi lakini sheria hii kwa upande wetu wa Zanzibar tunampa mamlaka hayo kupeleka kesi kwenye Mahakama au kutopeleka tunampa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kwa hivyo, tunatoa wito kwa wananchi sheria hii ni yao pahali popote watakaponyimwa haki ya faili hili kuzuiwa na polisi, basi anayo ruhusa kwenda kulalamika kwa mwendesha mashataka na Mwendesha Mashtaka tunampa uwezo kwa sheria hii kulitaka faili hilo litafutwe popote lilipo ili mwananchi huyo apate haki. Mhe. Spika, hili ni jambo la kupongezwa kwani hapo nyuma wananchi walikuwa wanatafuta wapi waende.

Kwa hivyo, sheria hii imeweka wazi kwamba mwananchi anaponyimwa haki ya lalamiko lake ni kukaliwa kitako katika Idara ya Upelelezi wa Polisi au kwenye chombo chochote cha polisi basi anayo haki kwenda kwa Mwendesha Mashtaka wa serikali na kupeleka lalamiko lake, na Mwendesha Mashtaka tumempa mamlaka ya kumtaka Mkuu wa Polisi kutafuta taarifa zake na kuweza kupatiwa ufumbuzi.

Lakini haitoshi pale Mwendesha Mashtaka ambapo ametoa hukumu kwamba kesi hii haifai kwenda mashtaka, basi hii sheria inampa haki mwananchi apate maelezo ya kutosha na ya mridhishe yule ambaye kesi yake haitapaswa kwenda Mahakamani. Fursa hiyo amepewa pia kama hakutosheka basi taarifa ile atapewa na anaweza kwenda nayo Mahakamani huko mwananchi anaweza kuridhika. Mhe. Spika, hizi zote zimeweka haki kumsaidia mwananchi asipoteze haki yake na kuona serikali hii itamtendea haki mwananchi.

Mhe. Spika, jambo jengine katika kifungu cha 11 (1) hapa Mkurugenzi wa Mashtaka amepewa nafasi ya kuchagua mwanasheria yoyote kumpa mamlaka ya kuwa Mwendesha Mashtaka. Bahati nzuri hapa pameelezwa katika Mahakama za Wilaya na Mikoa. Hapa nimesahau kuuliza wakati nilipokuwa katika kamati. Je, katika kesi zile ambazo zinahusu Mahakama ya Kazi utaratibu wake uko vipi, Mwendesha Mashtaka naye pale atapeleka mtu au kutakuwa na utaratibu gani utakaotumika.

Pia, fursa zilizotolewa kwa wale waliopeleka kesi zao. Je, huku kama karani ameikalia kesi hiyo mlalamikaji atakuwa na haki kwenda Afisi ya Mwendesha Mashtaka akaweza kutatuliwa tatizo lake. Hili nitamuomba Mhe. Waziri anisaidie kwa sababu wakati wa kamati nilisahau kuliulizia.

Mhe. Spika, humu katika mswada yamewekwa mazingira ya utekelezaji wa kazi zake Mwendesha Mashtaka haya yamewekwa wazi. Lakini kwenye

kifungu cha 16(1b) hiki kinampa Mwendesha Mashtaka kushiriki katika mashauri ya uchunguzi ya vifo vya ghafla katika mazingira atakayoona inafaa kufanya hivyo. Hapa kidogo Mhe. Waziri anisaidie ni katika mazingira yepi Mwendesha Mashtaka ataweza kutekeleza majukumu ambayo yamo katika kifungu cha 16(1b) na kazi hii ataifanya peke yake au atashirikiana na nani ili hiyo kazi iweze kuleta matunda hayo.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi naridhika na yote yaliyomo kwenye mswada pamoja na mabadiliko yaliyofanywa. Pia, mimi naipongeza serikali hasa katika kifungu cha 23 (1) juu ya kuundwa hii kamati ya mashauriano, hii itasaidia sana.

Mhe. Spika, waliotajwa humu kwanza ni Jaji wa Mahakama Kuu, Mkurugenzi wa Mashtaka, Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo, Naibu Mkurugenzi wa Jinai, Mrajis wa Mahakama Kuu, Mkemia Mkuu wa Serikali, Daktari Mkuu na Mwakilishi wa Chama cha Wanasheria.

Mhe. Spika, hili litaondosha tatizo na nafikiri kamati hii itakapofanya kazi vizuri itasaidia sana kusukuma kesi, kwa sababu hivi sasa kuna matatizo hasa kesi zinazohusu upande wa mambo ya serikali. Serikali inapopeleka malalamiko inakuwa dhaifu kupata mashirikiano ya ushahidi na mara nyingi serikali huwa inashindwa kwani mashahidi hawajitokezi. Mimi ningetoa wito zile adhabu ambazo zimewekwa kwenye sheria ya adhabu basi nafikiri hazitoshi kwa watumishi ambao hawataki kujitokeza katika kutoa ushahidi Mahakamani.

Ipo haja ya wafanyakazi wa serikali ambao watahusika kutoa ushahidi na hawakufika adhabu zao Mhe. Spika, ziongezwe. Kwa sababu kwa kesi za serikali hao ndio wataohusika zaidi ndio waitwe, kesi ya ardhi anaweza kutakiwa Afisa wa Ardhi au mpimaji, inaitwa mara tatu hapiti, sasa kwa mujibu wa kanuni kesi itabidi itupiliwe mbali, ni wakati haki itapotezwa.

Kesi za kubaka mtoto daktari ataitwa mara sita hafiki ana kazi, wazee wanalalamika mtoto wao kama alivyozungumza Mhe. Mkuu wa Mkoa hapa ameathirika, lakini daktari hataki kufika. Sasa Mhe. Spika, kwa mnasaba huo, mimi nasema mbali ya kazi zilizotajwa basi ingeweka kanuni hasa kwa watumishi wa serikali kupewa adhabu maalum kwa kushindwa kwenda mahkamani kutoa ushahidi kuwasaidia mawakili wa serikali katika utetezi wa mambo yake.

Mhe. Spika, baada ya mchango huo narejea tena kusema kuwa mimi mswada huu nauunga mkono na wewe nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika jioni hii kwenye kikao cha Baraza na kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, vile vile, sina budi kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuwa mchangiaji jioni hii, lakini vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na uteuzi aliyoufanya wa wenzetu Waheshimiwa
Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka chama cha upinzani kwa mujibu wa Katiba na mara baada ya maridhiano yaliyofanywa na Mhe. Katibu Mkuu wa *CUF* na Mhe. Rais.

Kwanza kwa kumtambua Mhe. Rais na kuitambua serikali na kama unavyosikia michango yetu kwamba kila Mjumbe anayechangia basi anakubali au kuunga mkono hoja. Hayo ni mafanikio makubwa Mhe. Spika.

Pia, nataka niwapongeze wenzetu hao walioteuliwa na kusema kwamba tutashirikiananao katika Baraza hili kwa yale yote ambayo tunawajibika kushirikiana nao pamoja.

Mhe. Spika, nikianza na mchango wangu kwanza nataka nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Mkurugenzi wa Mashtaka na Afisi yake kutokana na kuleta mswada wake huu wa sheria. Kimsingi mimi nakubaliana nao mia kwa mia kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chaani ambao wamenichagua.

Nianze katika mchango wangu, nilikuwa napata tabu kidogo na mchangio ambao ulitolewa asubuhi sijui kama na Mhe. Mohammed Ali Salim au yeyote yule, nikawa najaribu kuangalia kile kipengele ambacho amekizungumza, lakini bahati nzuri sikukiona pengine kutokana na muda mfupi niliouangalia.

Mhe. huyo alipokuwa akichangia alisema kwamba, ana wasi wasi kuona mshtakiwa au mwenye kushtaki kuwa na uhuru wa kuchagua jaji ambaye ataendesha kesi ambayo inaendeshwa zidi yake.

Mhe. Spika, ninachokumbuka mimi kama sikosei katika utaratibu kama huu mshtakiwa ama mtu ambaye ana mashtaka mahkamani anaweza akapeleka maombi yake pengine kwa Mkurugenzi wa Mashtaka iwapo atakuwa haridhiki au hana imani na jaji ama hakimu anayeendesha kesi. Lakini kuchagua pengine nihukumiwe na jaji fulani hii naona iko kinyumenyume. Sasa sijui kama Mheshimiwa alikuwa anazungumzia hilo au vipi, lakini kwa sababu wataalamu

wetu wapo ambao wameleta mswada huu pamoja na Waziri wa Katiba na Utawala Bora basi nafikiri tutafikia mahala pazuri kuona ni kipi kilichokusudiwa.

Jengine ninalotaka kulichangia katika yale ambayo nimeya-*note* ni kifungu cha 4(4) cha mswada huu kinachozungumzia uteuzi wa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka. Mhe. Spika, kwanza mimi nakubaliana moja kwa moja na mswada wenyewe kuhusu uteuzi wa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, lakini pia nilikuwa natilia mkazo yale mengine yaliyozungumzwa na Wajumbe iwekwe wazi basi katika sheria kuonekana kwamba hapa isiwe ile labda inaweza ama hapana, iwekwe kwenye sheria kuona kuna ulazima wa kuteuliwa kwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka.

Jengine nataka nilitolee pongezi lile eneo lililozungumzwa kuwa wengine walikuwa na mashaka kusema labda kujiuzulu huyu Naibu Mkurugenzi. Suala la kujiuzulu kwa mtu yeyote katika nafasi yoyote ile ni suala ambalo lipo kwa mujibu wa sheria na mtu yeyote anaweza kutegemeana na hali halisi ambayo yeye mwenyewe anayo. Aidha, kwa kutokumudu kazi yake pengine kwa ugonjwa ama hata kutokupenda baada ya kuteuliwa. Haki hiyo anayo kwa hivyo, sioni tatizo kama mtu atajiuzulu.

Lakini vile vile, naomba niipongeze Afisi ya Mkurugenzi kwa lile eneo ambalo wamelizungumza la kuhusu yule ambayo amejiuzulu kwa njia moja au nyengine. Kwa sababu kabla ya hapo alikuwa ni mfanyakazi wa serikali katika vitengo vya sheria, kubakia na kazi yake ile ambayo ameajiriwa awali na mpaka muda wake utakapomalizika basi akawa amestaafu kwa mujibu wa sheria. Hili nataka nilipongeze kwa dhati kabisa kwa sababu Mhe. Spika, itakuwa imejengea himaya na mustakabali mzuri wa maisha ya yule mtu ambaye ameteuliwa na baadae akajiuzulu kwa utaratibu wowote ule ambao umejitokeza.

Sambamba na hilo, mimi nilienda mbele zaidi nikasema hii isitokee kwa Naibu Mkurugenzi tu, lakini hata Mkurugenzi mwenyewe wa Mashtaka linapotokea suala kama hilo, basi na yeye aweze kwenda katika nyanja kama hizo ambazo nimetangulia kuzizungumza.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu uajiri katika kifungu cha 6(1), kinazungumza uajiri kwa watu ambao wataajiriwa katika Afisi ya Mkuruegnzi wa Mashtaka. Imeelezwa kwamba hawa watafuata taratibu zote za serikali.

Mimi nakubaliana moja kwa moja na hiyo hoja, labda cha msingi tu na ninafikiria hicho wenyewe pia Afisi watakuwa wanakizingatia kuona kuwa yule mtu ambaye wanamuajiri watakuwa na vigezo vyao ambavyo

vinawafanya wao waweze kumuajiri. Nafikiri hawatoajiri mtu tu ambaye hatakuwa na zile sifa ambazo wanazihitaji.

Kitu chengine ni kwamba nataka niipongeze Afisi pale ambapo imesema kuwa miongoni mwa kazi za Afisi hiyo zimetajwa pale, kama sikosei zitakuwa karibu *items* kama tisa. Lakini mimi ningezungumzia moja tu.

Mimi nataka nizungumzie ile ambayo imetolewa na ambayo kila siku ndani ya Baraza letu tunaizungumza, umuhimu wa kupatiwa mafunzo kwa wafanyakazi ambao wanaajiriwa. Nataka nilipongeze hilo kwamba wameliona mapema kuwa wale watu ambao wanaajiriwa wasitoshelezeke tu kwamba tayari wamewaajiri na sifa walizokuwanazo, lakini pia unapopatikana wasaa au muda basi wahakikishe wanawapatia mafunzo mbali mbali ili kuweza kumudu vyema kazi zao lakini pia kuongeza ujuzi.

Kwa misingi hiyo hiyo, kutakuwa na uwezekano pengine wa kupanda daraja hadi daraja yaani nafasi ambazo aliyeajiriwa ataajiriwa katika nafasi fulani lakini baada ya kupata mafunzo zaidi anaweza kupanda daraja mbali mbali hadi kufikia lengo ambalo mwenyewe amejiwekea yule mfanyakazi au uwezo ambao atakuwanao.

Mhe. Spika, sambamba na hilo basi niungane na wale wote ambao wamependekeza kuwa na maslahi bora ya wafanyakazi katika Afisi hii. Ushauri huu ambao umetolewa na Wajumbe naungana nao kwamba wenzetu wanaofanya kazi katika maeneo haya imeelezwa hapa kuwa wanatakiwa wawe watu ambao moja katika sifa zao kubwa basi kuwa waadilifu.

Sasa uadilifu wakati mwengine unakuja kwa nyanja mbili, mwengine anazaliwa ni muadilifu, lakini mwengine anakuwa muadilifu baada ya kujengewa mazingira mazuri zaidi au bora ya sehemu anayofanyia kazi, pamoja na vitendea kazi na mambo mengine. Kwa hivyo, yanapopatikana maslahi bora zaidi basi tunamfanya yule mtu awe muadilifu. Sasa ningeomba kuona kwamba mazingira haya wanayofanya kazi wenzetu kutokana na unyeti wake basi kukawa na hali nzuri ya maslahi.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kulizungumza liko katika kifungu cha 8(3) kinachohusiana na upatikanaji wa fedha. Imeelezwa wazi kwamba fedha ambazo zitapatikana ni miongoni mwa zile fedha ambazo zinapitishwa na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika Bajeti Kuu ya Serikali. Lakini pia kumetajwa misaada na michango mbali mbali na kukatajwa kuwa kuna fedha ambazo zitapatikana katika vianzio mbali mbali. Sina wasi wasi nayale maeneo mengine mawili ambayo Bajeti ya Serikali na vile vianzio ambavyo vipo kwa mujibu wa utaratibu.

Nilikuwa nataka kupata ufahamu tu kwa mfano tunapozungumzia misaada, misaada tunayokusudia hapa ni ile ya taasisi mbali mbali za nje ambayo inatolewa kwa nchi zetu mbali mbali zinazoendelea ili kuimarisha suala zima la Utawala Bora, ndio misaaada inayokusudiwa kuletwa katika chombo chetu hiki au vipi.

Halafu kuhusu michango kidogo nalo linanipa tabu au liko katika hiyo hiyo tunayoiita misaada inayotolewa na wahisani ama washirika wa maendeleo. Kama ni hivyo, basi nafikiri sina tatizo kwa sababu ni masuala ya kawaida kwa nchi zetu zinazoendelea kupata michango na misaada mbali mbali kutoka kwa wenzetu ambao wanahitaji kuona nchi zetu zinaendelea na kufanya vizuri katika masuala mazima ya kuendesha nchi pamoja na kujenga Utawala Bora ambao unahitajika katika nchi zote duniani.

Jengine ni suala ambalo Mhe. Ali Abdalla Ali alilizungumza. Nafikiri hapa kuna misemo au hadithi mbali mbali zilizotoka katika Baraza hili kuona kwamba hizi sehemu za Vyuo vya Mafunzo au wenzetu wengine wanaita Gereza. Sisi tunaita Chuo cha Mafunzo, bahati nzuri Chuo cha Mafunzo kila mtu anajua mafunzo maana yake nini, basi kiende sambamba na hili jina lenyewe.

Mhe. Spika, katika Vyuo vya Mafunzo jambo ambalo pengine sisi kama Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi hatupendelei sana kuliona lipo linaendelea ni upungufu wa vyoo. Mtu anayekwenda katika vyuo vile maana yake anakwenda kujifunza kutokana na yale makosa aliyoyafanya, sasa vile vile anatakiwa baada ya kurudi pale awe raia mwema na aweze kushirikiana na raia wengine katika kujenga taifa letu, sasa iwapo tutampeleka mtu pale na mazingira yake yakiwa machafu maana yake tunaweza kumpeleka mtu pale akiwa mzima, lakini akarudi katika hali ya ugonjwa kutokana na mazingira yaliyokuwa si mazuri na hasa masuala ya choo.

Mhe. Spika, choo sisi zamani wale ambao tulikuwa hatujaona vyoo ambavyo vimo katika vyumba vinavyoitwa *self container* tulikuwa tunapinga sana choo kukaa ndani ya chumba. Kwa sababu tunahisi choo kama vile vyoo tulivyokuwa tunavitumia sisi, lakini kumbe choo kinaweza kuwa chumbani na wewe mwenyewe usikereke ukafurahi na ukaona vizuri zaidi kuwa na choo chumbani. Kwa sababu unapokwenda chooni basi unaweza kwenda hali ya kuwa ndani mna watu hata kama 200 lakini wasijui kwamba wewe umekwenda chooni wakati gani na umetoka wakati gain?

Sasa hii inaonesha kwamba kuna umuhimu wa kuwa na vyoo bora katika sehemu mbali mbali Mhe. Spika, sitaki kusema labda kwenye Vyuo vya

Mafunzo kuwe na *self container* yaani choo kiwe ndani ya chumba hapana, lakini angalau basi viwe na mazingira yanayoridhisha.

Mhe. Spika, sisi Wajumbe wako, mimi mwenyewe binafsi pamoja na Wajumbe wenzangu tulipata nafasi ya kutembelea Gereza la Segerea, ambalo lilijengwa na Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Ali Hassan Mwinyi. Tulikwenda pale baada ya maombi ambayo tumeleta ya kwenda kujifunza mambo mbalimbali, moja ambalo tumejifunza kule Mhe. Spika, ni kwamba Gereza la Segerea ni kubwa ambalo linakaa watu wengi, lakini mazingira yake ndani ya gereza lile yanaridhisha sana.

Mhe. Spika, yanaridhisha kwa maana ya kwamba kwanza wale wafungwa waliomo mle ndani wametengwa vizuri, wanawake wanahudumiwa na magereza wa kike na wanaume wanahudumia magereza wa kiume. Lakini kama hiyo haitoshi pia mazingira yenyewe ndani ya lile gereza vyoo vyao viko vizuri vya *flash*. Huwezi kuamini kama kweli mle ni gerezani kutokana na vile vyoo, lakini vizuri zaidi kwamba lile eneo la kinamama limehifadhiwa vizuri zaidi.

Pamoja na kwamba Mhe. Mkongwe Nassor Juma, alipoingia pale hakuweza kustahamili alilia na tukajaribu kumuuliza, akasema kilichomliza kumuona mama mmoja ambaye ana mtoto wake ananyonyesha na anasema kwamba kabla ya hapo alifungwa akiwa mjamzito na mpaka wakati ule amejifungua na yule mtoto ana karibu miaka mitatu au minne hivi bado yuko gerezani. Kwa hivyo, hicho ndicho kilichomliza, lakini si mazingira mabaya ya lile gereza ni hicho tu kuona yule mtoto nae yuko kule gerezani na mama yake pamoja.

Mhe. Spika, baada ya hilo nafikiria pamoja na yale mengine niliyoyazungumza basi mimi nafikiri tungeelekea huko kuona kwamba tunafika huko. Kwa sababu kama ilivyosema kwamba tumetoa mifano mbali mbali hapa ya viongozi wa nchi mbali mbali ambao walikuwa wanaongoza katika maeneo mbali mbali, wengine wakipinga bajeti labda ya mambo ya ndani yanayohusiana na magereza na mambo mengine, lakini ilipofika muda wakaingia wao kule gerezani wakaona hali halisi basi waliona kwamba kumbe ile bajeti wanayopewa pale ni ndogo hata ile ambayo kaiomba waziri husika.

Kwa hivyo, pamoja na hayo, haya yote yatawezekana Mhe. Spika, iwapo tutaongeza bajeti kwa eneo hili, sio tuzungumze kwa maneno, lakini tuongeze na bajeti kadiri itavyowezekana. Nafikiria Mhe. spika, serikali yetu imekuwa sikivu na kuona kwamba kila pale ambapo tunapata chochote kinachoongezeka, basi tumekuwa tukiongeza bajeti katika maeneo mbali mbali ya wizara zetu. Kwa hivyo, nafikiri ni jambo jema.

Mhe. Spika, jengine ambalo asubuhi pia lilizungumzwa na Mhe. Said Ali Mbarouk, yeye alijitolea mfano mwenyewe wakati alipokwenda Japan na kuona umuhimu wa suala zima la Mkemia Mkuu. Miongoni mwa Wajumbe ambao wamo katika kamati yetu basi Mkemia Mkuu nae yumo. Tumekuwa tukileta matatizo mengi au pengine kumsumbua sana mwenzetu huyu kutokana na yale yanayojitokeza kama alivyoendelea kuanza kuzungumzia Mhe. Said Ali Mbarouk kuhusu upatikanaji wa ushahidi wa mambo ambayo yanatokea hasa katika madawa ya kulevya na mambo mengine.

Lakini mimi nasema labda niungane naye moja kwa moja Mhe. Said Ali Mbarouk kwa njia moja au nyengine, kama tulivyoweza kufanya katika maeneo mengine. Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja imekuwa ikizungumzwa siku zote hapa kwamba imepiga hatua kubwa katika kupata vifaa mbali mbali vya matibabu pamoja na madawa.

Haya hayakuja wenyewe tu, lakini yalikuja baada ya juhudi kubwa za serikali pamoja na wizara husika kutafuta misaada mbali mbali ya kifedha, lakini pia juhudi ambazo zimefanywa kutembea nje kwa wenzetu washirika wa maendeleo kuona kuwa tunapata vile vifaa ambavyo vitasaidia kupunguza tatizo liliyopo.

Sasa na hii Mhe. Spika, mimi ningekubaliana sana na Mhe. Said Ali Mbarouk juu ya ushauri wake kwamba tutafute njia hizi ambazo tumezitumia kuweza kupata vyombo ambavyo vitaweza kugundua kitu ambacho kimeonekana. Kwa mfano katika madawa ya kulevya na mambo mengine kwa wakati mdogo zaidi.

Mhe. Spika, kama nilivyoanza ni vyema kwamba mwenzetu huyu ili tusimsumbue basi tuhakikishe tunapata huo uhisani kwa njia moja au nyengine kupata vyombo bora na kuweza kupata ushahidi uliokuwa mzuri ambao hautakuwa wa ubabaishaji.

Jengine katika eneo hili ni kuhusu kuwepo kwa sera. Mhe. Spika, jambo lolote ambalo zuri au linatakiwa liwe zuri basi ni vyema likawekewa utaratibu. Sera maana yake ni utaratibu ambao umewekwa wa kufuatwa kuwa lazima tupite njia hii. Sasa mimi napongeza hili kwa upande wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuwa na sera, bila ya kuwa na sera maana yake ni vurugu. Kila mmoja angeweza kufanya au kutekeleza wajibu wake huu kwa vile ambavyo anaona inafaa, lakini tunapokuwa na sera maana yake tunakuwa na muongozo, tunakuwa na dira, tunaona tunapokwenda ni hapa na tunatumia misingi hii na utaratibu huu.

Kwa hivyo, kuwepo kwa sera kwa kweli mimi napongeza na ni vizuri zaidi kukawa na utaratibu wa mara kwa mara kwa Wajumbe au wafanyakazi wa

taasisi hii kuona kwamba wanapata mafunzo mbali mbali, mbali yale ya nje ya kusoma lakini hata yale ya ndani ya kuwapa muongozo wa kufanya kazi zao vizuri. Pamoja na kwamba humu imetajwa kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa ndiye anayeongoza taratibu zote za pale na kutoa miongozo kazi gani ziweze kufanywa.

Vile vile, jambo jengine ambalo ningependa nilizungumze na kidogo nimefurahishwa nalo ambalo limezungumzwa katika mswada huu ni udhibiti wa wafanyakazi. Udhibiti wa wafanyakazi ni jambo muhimu, kwani tunaona matokeo mbali mbali ambayo yanaathiri wizara mbali mbali na taasisi za serikali. Aidha wizara itakua imechukua juhudi za kumsomesha mfanyakazi wake kwa muda mrefu kama hapa nchini au kumpeleka nje ya nchi na akafanya vizuri katika kusoma kwake na baadae akarudi kufanya kazi katika eneo hilo.

Lakini mara baada ya muda pengine kukawa na utaratibu wa kwamba kuna taasisi fulani imeona kuna upungufu wa kada ambayo anayo mfanyakazi yule basi wakaomba na kwenda kumchukua, wanapomchukua maana yake wanamuhamisha pale, sasa wanapomhamisha sioni kama ule ni utaratibu mzuri. Sasa wenzetu nafikiri wameliona hilo.

Nataka niwapongeze kwa sababu unapomchukua mfanyakazi ambaye tayari wenzako wametumia fedha na juhudi nyingi kuona wanakuwa na mtu kama yule halafu wewe ukamchukua kwa njia rahisi na kwenda kumtumia tu, kwa kweli ni jambo ambalo halipendezi sana. Ningeomba taasisi nyengine za serikali zote zikafuata mfumo huu.

Pia, niwapongeze kuwa wameona umuhimu vile vile katika hili itakapokuwa yule mfanyakazi ambaye wamemsomesha vizuri na pengine akaonekana na Mhe. Rais na akaamua kumteuwa basi hiyo wanaridhia. Mimi nakubalianana lo hili kimsingi kwa sababu lengo la taasisi au chombo chetu hicho ni kuona kwamba wanafanikiwa na kutoa nafasi nzuri zaidi kuonekana kama ni kigezo kwa Afisi hii kuwa wafanyakazi wake wamefanya kazi vizuri napengine wameonekana kuwa wanaweza kufanya kazi vizuri na kupata uteuzi wa Mhe. Rais.

Mhe. Spika, kama tunavyoelewa kwamba uteuzi wa Mhe. Rais ni nafasi adhimu na inabidi kila yule anayeipata aifanyie kazi vizuri na aienzi. Basi mtu anapopata nafasi hiyo ni vyema yule muajiri wake vile vile akubali kwamba hilo jambo ni jema na wenzetu hili wamelizungumza wazi wazi kusema kwamba, wao wanalikubali. Lakini kwa mazingira mengine tu ya kwamba mtu anamuondoa mfanyakazi huyo kumpeleka katika eneo lake ili kujenga mazingira

mazuri, hilo hawakubaliani nalo na mimi naungana nao vile vile, kwamba tusiruhusu mambo kama hayo kwa sababu tutakuwa hatufiki mahala pazuri.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Chaani tunaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja pamoja na marekebisho yake yote ambayo yatafanywa na Baraza lako tukufu Mhe. Spika. Ahsante sana.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, nami kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uanzishaji na Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwa kweli nitakuwa na mchango mfupi kulingana na mswada huu kuwa umeshachangiwa na wengi na vipengele vingi wameshavigusa. Kwa hivyo, mimi Mhe. Spika, kwanza ni kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea mswada huu hapa Barazani na kupata kuujadili na kuupa baraka zake.

Mhe. Spika, kuweko kwa Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka hili ni jambo jema sana na ni jambo zuri. Sasa kuwepo kwa Ofisi hii itamsaidia Mkugenzi wa Mashtaka kujipanga vizuri pamoja na watendaji wake ili kujadili mambo na kuyapanga mambo kwa mujibu kama vile vilivyopangwa. Na hili Mhe. Spika, katika nchi kuwepo Ofisi ya Mkurugenzii Mkuu wa Mashtaka pamoja na vianzio vyake ni kitu muhimu ambayo masuala haya yapo katika nchi nyingi tu dunia hii.

Mhe. Spika, ukiona nchi haina vyombo vilivyokamilika kama hivi basi misukosuko inakuwa haiondoki katika nchi ile, kwa mfano tutizame kama jirani zetu hawa wa Somalia kila leo nchi inakuwa haitulii, haitambulikani kila anaekaa sie na kila uongozi unaopangwa sio, kwa ukosefu wa kupata vyombo mbali mbali vilivyokuwa muhimu ndani ya nchi kama hivi tuliokuwa tunataka kuvianzisha. Mhe. Spika, kwa Afisi hii itasaidia zaidi kuipa hadhi nchi yetu na ulinzi na utulivu kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, kama inavyoeleweka Ofisi hii huwa inahitaji masuala mengi tu. Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Waziri akaiangalia kwa kima katika kuipungizia makero ya mahitaji yanayohitajika ndani ya Ofisi hii ili na wao wakaendelea na kazi vizuri kwa kushirikiana na taasisi nyengine zinazohusika katika Ofisi hii.

Mhe. Spika, nije katika suala la mtuhumiwa, hapa kuna malalamiko mengi ya baadhi ya wananchi wetu ambao wanaokutana na matatizo ya kutuhumiwa,

wakati mwengine utamtuhumu mtu kitu pasipo kukifanya au kukikosa, lakini kwa chuki tu ya baadhi ya wapelelezi waliokuwa sio waadilifu na si waaminifu wanamtuhumu mtu yule bila ya kumfanyia uchungunzi au upelelezi na baadae kumtia ndani ya kosa na kupata adhatu na kuwekwa Sero kama wanavyosema wenyewe kwa muda usiopungua kama siku tatu au nne. Kwa hivyo, utakuta pale umemdhalilisha na umempa adhabu mtu yule bila ya kuwa na kosa kwa ukosefu wa upelelezi na uchunguzi katika kosa.

Mhe. Spika, ningeomba Mhe. Waziri katika watu hawa wanaohusika na upelelezi na uchunguzi wa watuhumiwa wakawa na kozi maalum au masomo ya kutosha ili kabla hawajaanzishwa kazi wakafanyiwa mtihani wakajulikana kuwa mtihani ule wamefuzu na wanaweza kuifanya kazi ile kuliko kuwatoa watu ukawakurupua tu kamchukuwe mtuhumiwa fulani tunashaka na jambo fulani bila ya kumfanyia uchungizi na kumchukuwa kumuweka ndani. Kwa hivyo, matokeo yake inakuwa malalamiko kwa watu kama wale ambao hawana kosa na wameshapewa adhabu ambazo zilizokuwa hazistahili.

Kwa hivyo, ,Mhe. Waziri hapa ningeomba hawa wanaohusika na upelelezo wakawa na kazi za kutosha ili kufanikisha kazi hii ya upelelezi ili mtu akifika Mahakamani au kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ikathibitishwa kile kitendo walichokifanya kimeshakuwa na muelekeo kwa kweli alishiriki na kulifanya kosa lile. Mhe. Spika.Kwa hiyo, Mhe. Waziri kwa maoni yangu hapa ningependa itolewe kozi ya kutosha kwa watu kama hawa ili kuondosha usumbufu.

Mhe. Spika, suala la kuchukuwa dhamana, hii ni muhimu na haki yake kwa kila raia au binaadamu pindipo amepelekwa Mahakamani baada ya kutolewa maamuzi ya Mahakama kuwa wapewe dhamana ni haki yako kama pindipo kesi yako bado haijapata uchunguzi na ufafanuzi.Kwa hiyo, kwa upelelezi uchukuliwe dhamana. Mhe. Spika, hili ni jambo zuri sana, lakini tatizo limejitokeza utakuta watu hawa wameshapewa muda wa kuchukuliwa dhamana kama muda wa wiki au wiki mbili, kwa ukorofi wa wachache tu, hakimu keshaamua achukuliwe dhamana kwa muda wa wiki mbili ili afanyiwe uchunguzi na upelelezi zaidi.

Lakini wachache tu watazunguka kwa uenyenji au kwa kutumia uyakhe! Na kuzungusha dhamana ile ili isifikie ile siku na kutolewa muhalifuu yule kabla ya ile siku iliyopangwa na hakimu ili kupoteza ushahidi. Kwa hivyo, hili Mhe. Waziri nalo liangaliwe sana lisije kuleta usumbufu kwa sababu kuna wahalifu wengine wamezoea kazi ya uhalifu, lakini matokeo yake wakipelekwa ndani kwa kuchunguzwa na kufanyiwa upelelezi hutoka watu kujifanya ndugu au rafiki kumpa dhamana kabla ya siku ya kutolewa dhamana na hakimu kufika.

Kwa hivyo, hii inaleta usumbufu hata kwa wale wananchi wema ambao waliokuwa wametoa ushahidi au kutoa picha kamili kwa mtuhumiwa yule.Kwa hivyo, akitoka nje anatoka kwa jeuri na kuwapa usumbufu wale waliokuwa wamemtolea ushahidi kuwa juhudi yao yote waliochukuwa ni bure yeye ameshatoka nje. Kwa hivyo, hapa Mhe. Waziri tutataka Wakurugenzi wetu na watendaji wetu wapaangalie sana.

Mhe. Spika, tuna masuala tunasema kuwa hakimu katika kutoa maamuzi yake asiingiliwe hii ni utaratibu mzuri kwa kuwa hakimu akiamua kutoa hukumu zake au maamuzi yake asiingiliwe. Lakini sasa utakuta kuna matatizo mengine yamejitokeza baadhi ya Mahakimu wetu akithibitisha mtu kafanya kosa basi kafanya kosa, kuna makosa mengi tu makubwa ya jinai ambayo yakumpotezea mtu maisha ya uhalifu na miaka ya nyuma kulitokea mauaji huko Mazizini na waliofanya uuaji huo wakakamatwa wakawekwa ndani na wengine wakakutikana na silaha.

Lakini utakuta wale watu wanaachiwa na wako huru na wala hukusikia kesi ile maamuzi yake yameamuliwa vipi. Kwa hivyo, utakuta hii inavunja moyo kwa wananchi pindipo hakimu kwa kuwa umepewa uhuru usiingiliwe. Mhe. Spika, lakini leo utakuta wahalifu wanafanya vitendo viovu, halafu wanakuwa huru kipindi kifupi tu. Mhe. Spika, hii kwa kweli inavunja moyo, kama kuna mtindo huo unaendelea Mhe. Waziri uondoshwe au ufutwe moja kwa moja ili kuondosha usumbufu kwa wananchi wetu.

Mara nyingi ukipita mitaani huwa unalalamikiwa mtu kafanya uhalifu mkubwa, lakini haifiki mwezi au mwaka kaekwa ndani anatolewa bila ya kujua hukumu gani iliyofanyika anakwenda kusikiliza kesi kwa kipindi kifupi tu baada ya muda anaambiwa kuwa kesi ile imetupiliwa mbali hakuna ushahidi na wakati mtu huyu kakutikana na silaha au na vitu vya uhalifu.Kwa hivyo, hili linaleta usumbufu. Mhe. Spika, kwa kuwa kumeletwa mswada huu wa masawazisho na matayarisho mbali mbali.Kwa hivyo, ningeomba na hilo liangaliwe kabla mswada huu haujaanza kazi rasmi.

Mhe. Spika, nakuja ukurasa wa 152 kifungu cha 13 utaratibu wa upelelezi kwa Afisa Mkurugenzi wa Mashtaka pindi anapotaka kufanyiwa upelelezi wa mtuhimiwa aliefanya kosa la jinai.Kwa hivyo, hili nalo liangaliwe kwa kima kama nilivyozungumza mwanzo kuwa mtu huyu afanyiwe uchunguzi wa kutosha sio apelekwe tu, tumetuma wapelelezi kwenda kumchukuwa.Kwa hiyo, tumchukuwe bila ya kumpeleleza na bila kuchunguza hili suala alilolifanya tusukume tu atakwenda kuamua mwenyewe Mkurugenzi wa Mashtaka. Kwa kweli hili linaleta usumbufu.

Kwa hivyo, ni vyema watenda makosa hawa kukatumia uchunguzi wetu wa kutosha kufanya upelelezi ili kuhakikisha mpaka anafikia kule angalau ana asilimia fulani ya makosa yale aliyoyafanya ambapo pakupatikana uthibitisho wake.

Mhe. Spika, nakuja ukurasa wa 150 kifungu cha 8, kinachosema fedha na bajeti ya Afisi. Mhe. Spika, hii kuna haja sana ikaangaliwa na ikafanyiwa kazi na Mhe. Waziri wakati wa bajeti yako Ofisi kama hii ya Mkurugenzi wa Mashtaka na vitengo hivi vya Mahakama na mambo ya vituo vya Polisi kuna haja ya kuwaongezea bajeti.

Kwa sababu kuna usumbufu mkubwa unatokezea pindipo baada ya kukamatwa muhalifu au mtuhumiwa unakwenda kwa Mkurugenzi wa Mashtaka anataka kutoa gari kwa kwenda kufanyia upelelezi au uchunguzu unaambiwa gari hamna, au unakwenda kwenye kituo cha polisi katokea muhalifu anahujumiwa na wananchi ambao kwa tuhuma tu hajajulikana kama ni mkosa ama si mkosa hali imekuwa mbaya na ngumu unaleta ripoti kwenye kituo husika angalau kupatiwa usalama wa gari ya kwenda kuchukuliwa ili kumuokoa maisha yake na kumpeleka kwenye vyombo vya sheria kujua kama kafanya kosa au hakufanya kosa unakuta unaambiwa kuwa gari hapana au mafuta hakuna.

Kwa hivyo, hili linaleta usumbufu kwa baadhi ya wananchi wengi ambao wanatuhumiwa na makosa ambao kabla ya kufikishwa kwenye vyombo vya sheria hawajahukumiwa unakuta wameshapatwa adhabu ya kutosha kwa masuala madogo tu ya kukosa usafiri. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri katika bajeti zako uliangalie sana suala hili la kuwapa nyenzo au vifaa vya usafiri vitengo hivi.

Mhe. Spika, kwa kweli kama Ofisi hizi au vitengo hivi tutaviangalia vya kutosha na kuvipatia nyenzo za kutosha baadhi ya mambo mengi ya uhalifu na ya ukatili huenda yakapungua katika nchi yetu. Lakini kama nilivyoeleza kama kutakuwa na upungufu wa vifaa hivi utakuta uzembe mdogo unatokea kwa baadhi ya watu wetu kupoteza maisha pasipokuwa na kosa kwa ukosefu wa vifaa kama hivyo.

Mhe. Spika, kwa kweli mswada huu mimi nimeufurahia sana kuletwa hapa Barazani na kupata kuuchangia ili wananchi wetu wakatusikiliza kwa kina ili yale malalamiko wanayotupa mbali na kasoro ambazo zilizokuwa zinatendeka katika vyombo kama hivi. Kwa hivyo, leo tutapata ufumbuzi na wahusika watakuwa wanasikia.Kwa hivyo, *inshaalla* yatapungua.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi masuala haya ya mswada huu nayaunga mkono kwa kushirikiana na wananchi wangu wa Jimbo la Amani mia kwa mia, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza kabisa na mimi napenda kuchukuwa nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu wa sheria na kuweka masharti ya uanzishaji na uendeshaji wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na mambo yanatohusiana na hayo.

Mhe. Spika, napenda nianze na hadithi kidogo, Mhe. Spika, huwezi kujadili sheria au kutoa hukumu ya sheria kwa wale wataalamu wa sheria mimi si mtaalamu sana kama kwamba hujafanya *reference*. Kwa hivyo, na mimi napenda nitoe *reference* ya baadhi ya kesi ambazo zimetokea hapa nchini kwetu.

Mhe. Spika, zamani kesi zilivyokuwa zikihukumiwa ni tofauti na sasa hivi. Mara nyingi wakati kesi hizi zinavyokuwa zikihukumiwa mwakani watu walikuwa hawana *reference* ya kesi ambazo zilizokuwa zimepita nyuma. Nasikia zamani kulikuwa na mtu mmoja aliiba ndizi sehemu ya kati hapa Kiboje, lakini baada ya kuiba ndizi akapelekwa Mahakamani na akahukumiwa kwa bahati nzuri mtu yule akashinda kesi ile. Lakini baada ya kuiba Kiboje akahamia Kaskazini nako akenda kuiba kuku (Mkwajuni) kule kulikuwa na Jaji ambae sitaki kumtaja jina lakini baada ya kupelekwa Mahakamani, Jaji alimuuliza hivi wewe umeshawahi kuhukumiwa akajibu kwamba mimi tayari nimeshawahi kuhukumiwa, akamuuliza tena ulishinda au hukushinda akamjibu kwamba kesi ile mimi nilishinda. Jaji akamuhukumu basi akamwambia kama ulishinda huko hapa huwezi kushinda.Kwa hiyo jaji akamuhukumu akampeleka Gerezani.

Lakini pia, tunahadithiwa kwamba kulikuwa na Jaji Haji wa Haji ambae zamani alikuwa akihukumu, basi anakuhesabia ngazi zile ngapi na baadae anahisabu kumi basi na miaka yako 10. Kwa hiyo, nilitaka kesi hizi kuoanisha na sasa hivi tulipo. Lakini pia nina mfano halisi wa kesi nyengine pia nilitaka niitolee *reference* ambayo ilitokea hivi karibuni. Hivi karibuni katika jimbo langu kumevunjwa nyumba wakadai kwamba kuna mtu alikuwa na shamba lake na kwa bahati mbaya yeye alikuwa hayupo watu wakajenga katika shamba hili. Kesi ikaenda Mahakamani baada ya kwenda Mahakamani na Mahakama ikaamuru zivunjwe nyumba zile za watu waliojenga. Lakini wako ambao walihukumiwa waliitwa Mahakamani, lakini wengine kwa bahati mbaya au nzuri hawakuitwa Mahakamani na nyumba zao zikabomolewa.

Mhe. Spika, ninachotaka kukizungumza hapa ni kwamba nadhini haikuwa sahihi kuwavunjia wote wakati wengine hawajahukumiwa wala hawajaitwa Mahakamani. Kesi hii nadhani nitampelekea Mkurugenzi ili aweze kutoa maamuzi ambayo ni sahihi. Nilitaka nitoe mifano hiyo kwa sababu wataalamu wanasema huwezi kutoa maelezo au kuhukumu kesi kabla hujaijua kesi. Kwa hiyo hii ni mifano ya kesi ambazo zimetokea nyakati tafauti.

Mhe. Spika, nilichotaka kukizungumza hapa Mhe. Spika, ni kwamba sasa hivi wakati umebadilika tafauti na zamani kunahitaji tuwe na utaratibu mzuri kwa mwenendo wa kuendesha kesi zetu na bila ya kuwa chombo ambacho kitakuwa kinaongoza utaratibu mzima wa mwenendo wa kesi, basi nadhani hatutafikia hukumu ambazo zitakuwa zinatoa haki.

Jengine ambalo nilitaka nilizungumze sasa hivi dunia inazungumza Utawala Bora na baadhi au katika misingi ya Utawala Bora ,basi ni mambo kama haya ambayo yanafuata kwanza wanasema Utawala wa Sheria, lazima tuwe na Utawala wa Sheria ndipo ambapo tutaweza kuhakikisha kwamba tuna Utawala Bora. Lakini pia tunatakiwa tuwe na uwazi katika kuamua na kutoa hukumu ya mambo mbali mbali. Lakini pia tunatakiwa tuwajibike.

Mhe. Spika, kwa hivyo, misingi hii 3 nadhani ni moja ya sababu ya kuja kwa mswada huu ambao tunasema kwamba ni mswada wa kuanzisha ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na mambo mengine ambayo yanahusiana na hayo.

Mhe. Spika, ukitizama madhumuni na sababu ya mswada huu utaona kwamba kuna sababu ambazo zimepelekea kuja kwa mswada huu na moja ya sababu inaonekana kwamba kumekosekana kwa muundo au kuwepo kwa ofisi ambayo inaratibu mambo au mwenendo mzima wa kesi za jinai. Lakini pia, moja ya sababu nyengine ambayo imepelekea kuja kwa mswada huu ni kwamba zamani inaoenekana Mkurugenzi alikuwa akifaka kazi zake kwa ushirikiano na Mahakama lakini pia na polisi.

Lakini inaonekana uhusiano huu haukuwa wazi au kazi zao hazikuwa wazi kwa maana kwamba hazikuwa bayana nani anahusika na hili na nani anahusika na lile. Lakini pia imeelezwa katika sababu ni kwamba upeo wa uhuru wa uwazi wa kazi kama nilivyozungumza kwamba ulikuwa unakosekana.

Mhe. Spika, kama nilivyozungumza mwanzo ni kwamba tunahitaji kuwa na Utawala Bora na lazima tuwe na Utawala wa Sheria, tuwe na uwazi na tuwajibike. Kwa maana hiyo mimi binafsi naona kwamba sheria hii imekuja kwa madhumuni ya kuhakikisha mambo 3 haya ambayo ndio yatatupelekea kuwa na Utawala Bora. Bila ya sheria hii nadhani tungepata tabu bila ya kuhakikisha Utawala Bora ndani ya mwenendo mzima wa kesi za jinai, na

mifano kama hiyo niliyoitoa nadhani inathibitisha kwamba kuna kasoro mbali mbali ambazo zinajitokeza katika uendeshaji wa kesi zetu.

Mhe. Spika, kuja kwa mswada huu ninaamini kabisa kwamba utasaidia kwa kiasi kikubwa sana kuhakikisha kwamba sheria zetu zinalindwa, lakini pia watu wanapata haki zao kwa mujibu wanavyostahiki. Mhe. Spika, ukiangalia kazi za Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambayo tunataka kuianzisha sasa hivi moja ni kuhakikisha kwamba kumuwezesha Mkurugenzi kutekeleza kazi zake juu Katiba na Sheria nyengine husika. Mhe. Spika, hapa tutaona wazi kwamba Ofisi hii ina jukumu kubwa sana la kuhakikisha kwamba Mkurugenzi anafanyakazi zake kama inavyotakiwa kwa mujibu wa sheria zilizowekwa lakini pia ni kwa mujibu wa Katiba iliyopo hapa nchini ambayo hivi sasa inafanya kazi.

Mhe. Spika, nakusudia kusema ni kwamba kuja kwa sheria hii itatusadia kwa kiasi kikubwa kuona kwamba watu wanapata haki zao kama inavyostahiki. Kwa maana hiyo, kuwepo kwa sheria hii ni muhimu katika kuendesha nchi yetu, lakini pia ni muhimu katika kuendesha huo Utawala wa Sheria, lakini pia kuwajibika kwa watu mbali mbali ambao watakuwa na mamlaka ambayo watakuwa wamekabidhiwa na wananchi.

Mhe. Spika, napenda nikiri kwamba sheria hii itamfanya Mkurugenzi sasa awe na meno, kwa maana kwamba aweze kufanyakazi zake vizuri lakini pia aweze kuishauri serikali kuhusiana na mambo mbali mbali ambayo yatakuwa yanatokea katika nchi yetu. Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba kazi za Ofisi hii itampa uwezo mkuwa Mkurugenzi wa Mashtaka kuweza kuingilia kati masuala ambayo yatakuwa wanakwenda kinyume na utaratibu au na sheria. Kwa hivyo, napenda niwapongeze kwa kuleta sheria hii ambayo imekuja kwa wakati na kwa maana kwamba itatuwezesha sisi kuona kwamba watu wanapata haki.

Mhe. Spika, tukumbuke kwamba suala zima la Utawala Bora ni suala ambalo sasa hivi dunia nzima inalipigia kelele na kumekuweko na mikutano mbali mbali ya kimataifa ambayo yanahusisha au yamezungumzia masuala haya ya Utawala Bora, na nchi yetu na viongozi wetu wamekuwa wakisaini mikataba mbali mbali ya kimataifa kuhusiana na suala zima la utekelezaji wa Utawala Bora.

Kwa hivyo, hatuwezi kulikwepa suala hili kwa sababu tumo katika dunia na ni lazima twende sambamba na matakwa ya kimataifa ili tuweze kuendesha nchi yetu vizuri. Kwa maana hiyo kuja kwa mswada huu naamini kabisa unatekeleza hayo maazimio ya kimataifa ambayo yanataka kila nchi iweze kuwa na utaratibu mzuri wa kisheria na mwenendo mzima wa kuendesha

mashtaka katika nchi hiyo. Kwa hivyo, suala zima la kimataifa tutakuwa tayari tumeshalikabili kuona kwamba tunatekeleza yale matakwa ya kimataifa.

Mhe. Spika, katika mswada huu imeelezwa kipengele cha 9 kazi mbali mbali za mamlaka hii ya Mkurugenzi wa Mashtaka na moja kazi ambazo zimeelezwa ni kuelekeza polisi na taasisi nyengine ambayo inahusiana na upelelezi wa makosa ya jinai kuchunguza taarifa yoyote ya kujinai na kutoa taarifa kwake haraka iwezekanavyo. Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba itakapoanza kazi ,sheria hii ni dhahiri kwamba sasa tutakuwa na uharakishaji wa kesi mbali mbali za jinai. Kwa maana hiyo, itatusaidia kuponguza malalamiko makubwa ambayo yanajitokeza au yanaletwa kwa watu ambao inawezekana wakakosa haki zao kwa mujibu wa sheria.

Kwa hiyo, kama Mkurugenzi atafanya kazi zake vizuri, basi tunategemea sana kwamba malalamiko mbali mbali ambayo yamekuwa yakitolewa yataweza kupungua. Kwa maana hiyo, kuwepo kwa sheria hii pia kutasaidia wananchi katika kupunguza manung'uniko na malalamiko mbali mbali yanayohusiana na haki zao.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ni muhimu katika sheria hii ambalo mimi naliona limeweka uwazi ni suala zima la sheria na muongozo wa uendeshaji wa mashtaka. Mhe. Spika, bila ya sheria, bila ya muongozo, bila ya utaratibu mzuri hatuwezi tukaziendesha kesi zetu kwa utaratibu mzuri. Kwa sababu tayari Mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kuweka sheria, kuweka miongozo au kuandaa mipango mbali mbali ya uendeshaji wa mashtaka, ni dhahiri kwamba uendeshaji wetu wa mashtaka sasa utaboreka na kwa maana hiyo tutakuwa na ule Utawala Bora ambao tunasema utawala wa sheria, uwajibikaji na uwazi.

Mimi naamini kabisa kupita kwa sheria hii kutaiwezesha nchi yetu kuwa ni miongoni mwa nchi chache katika Afrika ambayo itakuwa na Utawala Bora katika dunia hii. Kwa maana hiyo, Mkurugenzi atawajibika kuona kwamba kutakuwa na sheria na mipango mbali mbali na miongozo ambayo itaiwezesha Mahakama lakini pia Polisi kuwajibika na kufanya kazi zake vizuri.

Mhe. Spika, sheria ndio ambayo inaandaa au inawezesha kupelekea kuwa na mikakati, bila ya sheria huwezi ukawa na mikakati. Kwa maana hiyo, kama Mkurugenzi ataweza kuwa na mamlaka ya kuweza kuweka sheria, kwa maana hiyo pia ataweza kuwa na mikakati ya kudhibiti mwenendo mzima wa hukumu ambazo zitakuwa zinatolewa.

Mhe. Spika, napenda niseme tu kwamba sheria hii imekuja kwa wakati muhimu ambapo sasa hivi nchi yetu ina mambo mbali mbali ambayo inahitaji kuyazingatia. Ninaamini kwamba kwa sababu tunaingia kwenye uchaguzi hivi

karibuni, kwa maana hiyo, sheria hii ikipitishwa itaweza kutatua matatizo au migogoro mbali mbali ambayo itajitokeza. Kwa sababu tumekuwa na uzoefu mkubwa mara tu baada ya uchaguzi kutokea migogoro mbali mbali, watu kukosa haki zao na kudhulumiwa.

Ninaamini kabisa kama tutaipitisha sheria hii itawezesha kukabiliana kwenda na uchaguzi ambao ni huru na wa haki. Kwa maana hiyo, tayari tutakuwa tumeshamuwekea Mkurugenzi wa Mashtaka kuweza kufanya kazi zake kwa uhuru, uwazi na uwajibikaji.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limejitokeza katika sheria hii ni kifungu cha 20 "Tathmini ya Utendaji". Nadhani Mkurugenzi wa mashtaka atakuwa ana uwezo wa kufanya tathmini kuhusu utendaji wa vyombo mbali mbali.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba kama hakuna utaratibu wa kutathmini utendaji, hatuwezi tukajua wapi tulipokosea. Kwa sababu katika sheria hii tayari katika kifungu cha 20 (1), naomba kunukuu.

Kifungu cha 20 (1):

> "Mkurugenzi ataandaa vigezo vya utendaji vitakavyopaswa kufuatwa na kufikiwa na kila kitengo cha uendeshaji mashtaka, iwe kitengo hicho kipo chini ya Afisi au vyenginevyo"

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba sasa hivi Mkurugenzi atakuwa na uwezo mkubwa wa kushauri mamlaka zinazohusika juu ya utendaji wa vyombo vyetu vya kutoa haki kwa sababu atakuwa na uwezo huu wa kufanya tathmini.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba utendaji wetu na ule uwajibikaji ambao tunasema ni moja ya msingi katika kuleta Utawala Bora, sasa hivi tutakuwa katika sehemu nzuri ya kuweza kutathmini hivyo vyombo ambavyo vinatoa haki.

Mhe. Spika, inaonekana kwamba kulikuwa hakuna utaratibu mzima wa tathmini ya vyombo hivi ambavyo vinatoa haki. Kwa sababu tu ya ukosefu wa sheria ambayo nani anawajibika kufanya tathmini, ni dhahiri kwamba sasa hivi kwa kuwa tumeshamuwekea mtu ambaye atawajibika kufuatilia utendaji wa vyombo.Kwa hivyo, utendaji na uwajibikaji utaboreka. Kwa maana hiyo, huo Utawala Bora ambao tunauzungumza utapatikana.

Mhe. Spika, mimi nadhani sina mengi lakini nilitaka nichangie hayo kidogo. Nadhani sheria hii ikipita basi itakuwa ndio dira yetu katika muongozo mzima wa uendeshaji wa mashtaka katika nchi yetu.

Mhe. Spika, ninaamini kabisa nchi inaongozwa na misingi ambayo ndio muhimu ya kuweza kuelekeza katika utoaji haki. Kwa hivyo, kuwepo kwa sheria hii itakuwa ni msingi madhubuti wa kuelekeza katika muongozo mzima wa utoaji haki katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo machache, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtoni, naunga mkono hoja hii ya kupitisha Sheria ya Uanzishaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naitakia kila la kheri sheria hii, Mhe. Rais aitie saini kabla ya uchaguzi.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nafikiri tumeita sana kutaka Wajumbe wachangie, inavyoelekea kwamba tumeridhika na kiwango ambacho Wajumbe wamepata nafasi. Sasa kwa muda uliobaki nadhani tungesitisha shughuli zetu hizi ili tumpe Waziri kwenda kujiandaa kwa kuja kufanya majumuisho kesho.

(Saa 1:40 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 22/01/2010 saa 3:00 asubuhi)